# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Sita – Tarehe 10 Aprili, 2018

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Tukae, Katibu.

**NDG. LINA KITOSI - KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Katibu.

**NDG. LINA KITOSI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na maswali tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 44

**Vituo vya Afya vya Kata za Mtwango, Mninga na Makungu**

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa Vituo vya Afya Kata za Mtwango, Mninga na Makungu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na ujenzi wa vituo vya afya awamu kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 kipaumbele kimewekwa katika ujenzi wa Kituo cha Afya Malangali kilichoko katika Jimbo la Mufindi Kusini ambao unahusisha ujenzi wa jengo la upasuaji, nyumba ya watumishi, maabara na jengo la wazazi kwa gharama ya shilingi milioni 400 ili kukiwezesha kutoa huduma za dharura za upasuaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi imetenga jumla ya shilingi milioni 40 kwa ajili ya umaliziaji wa Kituo cha Afya

cha Mninga. Fedha hizo zinatarajiwa kufanya umaliziaji wa jengo la wagonjwa wa nje *(OPD)* ambapo itatumika kiasi cha shilingi milioni 30 na shilingi milioni 10 za kuanzia ujenzi wa nyumba ya mganga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Vituo vya Afya Mtwango na Mninga umefikia hatua mbalimbali ambapo majengo ya maabara na nyumba ya mtumishi imefika hatua ya umaliziaji na vifaa vyote vya umaliziaji vimekwishafika *site*. Majengo ya upasuaji na akina mama yamefikia hatua ya kunyanyua kuta na vifaa vyote vya ukamilishaji vipo *site*, tunategemea kukamilisha kabla ya tarehe 31 Mei, kwa mujibu wa mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Kata ya Makungu hakuna ujenzi unaoendelea isipokuwa kuna kituo cha afya kinachomilikiwa na Kiwanda cha Karatasi cha Mgololo. Katika kituo hicho Serikali imepeleka Watumishi ambao wanalipwa mishahara na stahili zote kutoka Serikalini na kuchangia dawa pamoja na vifaa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mendrad Kigola swali la nyongeza.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa vile kwenye Jimbo la Mufindi Kusini Wilaya ya Mufindi, tuna ujenzi wa hospitali ambayo ni kubwa sana.

Je, Wizara ya TAMISEMI mnaweza mkatusaidia kupata ramani ambayo ni *standard* kwa ajili ya kujenga hospitali pale Jimbo la Mufindi Kusini?

Swali langu la pili, kama alivyoeleza kwenye majibu yako kwamba tuna ujenzi mkubwa sana pale Malangali Kituo cha Afya. Kwanza naishukuru Serikali kwa kutupatia zile milioni 400; lakini kile kituo cha afya tunategemea kifunguliwe na

mtu mkubwa sana. Je, Naibu Waziri uko tayari kutuunganisha na Waziri Mkuu aweze kufika pale Malangali kufungua kile kituo cha afya ili kianze kufanya kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Halmashauri kwa kazi nzuri waliyofanya kuhakikisha kwamba kituo cha afya kile kinakamilika na ni miongoni mwa vituo vya afya ambavyo vimejengwa kwa ustadi mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya suala la ujenzi wa hospitali ya Wilaya hitaji lake kubwa ni upatikanaji wa ramani, naomba nimhakikishie kwamba Wataalam wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Wataalam Wizara ya Afya, wako mbioni kukamilisha ramani ambazo zitatumika katika ujenzi wa Hospitali za Wilaya hizo 67 ikiwemo ya kwake ya Mufindi. *(Makofi)*

Swali lake la pili anaomba Ofisi ya Rais, TAMISEMI imuunganishe uwezekano wa Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa miongoni mwa watu watakaoenda kuzindua kituo chake cha afya. Naomba nimhakikishie utaratibu unaandaliwa chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tutaanza vituo 44 vyote vile ambavyo vimejengwa na kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatarajia pale Mheshimiwa Rais kwa nafasi yake na jinsi atakavyoridhia kutakuwa na uzinduzi ambao utafanyika nchi nzima tukianzia na hivyo vituo 44; sina uhakika sasa kwa nafasi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ataweza kwenda kuzindua kwake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ignas Malocha, swali la nyongeza.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika,

ahsante sana. Kwanza nishukuru Serikali kwa jitihada zake za ku-*support* ujenzi wa vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jimbo langu la Kwela tunavyo vituo vya afya ambavyo vimeanza kujengwa toka mwaka 2004 na wananchi wamejenga mpaka jengo la *OPD* kukamilika, lakini vituo hivyo mpaka sasa vimesimama kwa sababu havijapata fedha tena. Vituo hivyo ni Kituo cha Ilemba, Kahoze na Muze.

Je, ni lini Serikali itatoa fedha ku-*support* wananchi juhudi zao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anauliza ni lini Serikali itapeleka pesa kwa ajili ya kumalizia vituo vya afya ambavyo vimeanzishwa na wananchi muda mrefu.

Kwanza naomba nimtaarifu kwamba nia njema ya Serikali ya kuhakikisha kwamba huduma ya afya inafika kila mahali ikiwa ni pamoja na Wilaya yake, katika hospitali 67 ambazo zinaenda kujengwa za Wilaya na Wilaya yake ni miongoni mwa hospitali ambazo zitaenda kujengwa. Hiyo ni nia njema ya Serikali kuhakikisha kwamba huduma inapelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na hivyo vituo vyake kama nilivyojibu kwenye swali la msingi pale pesa inapopatikana hakika naomba nimhakikishie na hii itakuwa miongoni mwa vituo vya afya ambavyo vitaboreshwa ili viweze kutoa huduma tunayoitarajia.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Grace Victor Tendega sasa aulize swali lake.

Na. 45

## Mikopo ya Kujenga Nyumba kwa Walimu

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:-

Kuna uhaba wa nyumba za kuishi walimu licha ya juhudi za wananchi kujenga nyumba za walimu wa shule za msingi na sekondari; walimu hao pia wanahitaji kujenga nyumba zao wenyewe za kudumu.

Je, ni lini Serikali itaweka utaratibu wa kutoa mikopo kwa walimu ili wajenge nyumba zao binafsi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwa upo uhaba wa nyumba za walimu katika shule za msingi na sekondari ndiyo maana imekuwa ikijitahidi kila mwaka kujenga nyumba za walimu. Katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 Serikali kwa kushirikiana na wananchi, imekamilisha ujenzi wa nyumba 274 za walimu na hivyo kufikisha idadi ya nyumba 14,640 kati ya nyumba 67,711 zinazohitajika kwenye shule za sekondari. Aidha, nyumba 290 za walimu zimejengwa kwenye shule za msingi na hivyo kufikisha idadi ya nyumba 45,638 kati ya nyumba 175,930 zinazohitajika. Takwimu hizo zinabainisha kwamba familia za walimu 52,071 katika shule za sekondari na familia za walimu 130,300 kwenye shule za msingi zinaishi kwenye nyumba za kupanga au nyumba zao binafsi. Ni wazi kwamba mahitaji ya nyumba za walimu ni makubwa mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imedhamiria kuendelea kuweka kipaumbele cha kujenga nyumba za

walimu za kuishi familia mbili, nne au sita ambazo ni za gharama nafuu kulinganisha na gharama za kujenga nyumba za kuishi familia moja. Kipaumbele cha juu kitaendelea kuwekwa kwenye maeneo yenye mazingira magumu ya kupata nyumba za kupanga hasa maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa mikopo kwa ajili ya Walimu kujenga nyumba zao binafsi ni kama ulivyo kwa watumishi wengine wa Serikali, ambapo mtumishi anaruhusiwa kukopa kwenye taasisi au benki yenye mkataba maalum na mwajiri kwa kujaza fomu ili akatwe marejesho ya mkopo kutoka kwenye mshahara ambapo makato ya mkopo hayatakiwi kuzidi theluthi mbili ya mshahara na mkopo wote kulipwa kwa kipindi cha kati ya miezi 36 (miaka mitatu) hadi miezi 300 (miaka 25) kulingana na masharti ya taasisi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa taasisi zinazotoa mikopo ya nyumba kwa watumishi wa Serikali wakiwemo walimu ni Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)*, Kampuni ya Nyumba za Watumishi *(Watumishi Housing Company),* Benki ya Afrika *(Bank of Africa – BOA)* kupitia mpango wake wa WEZESHA, mabenki kadhaa mengine kama NMB, CRDB, Azania na kadhalika na kampuni nyingine kama vile *T-Mortgage* yanayolenga zaidi kuwakopesha watumishi wa kipato cha chini na cha kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili watumishi wakiwemo walimu wapate mikopo ya kujenga nyumba binafsi kwenye maeneo watakayochagua wao, inatakiwa Wakurugenzi wa Halmashauri wawasiliane na taasisi zinazokopesha ili waingie makubaliano maalum yatakayowawezesha watumishi wa Halmashauri wanaotaka mikopo ya kujenga nyumba binafsi wakiwemo walimu kupata mkopo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Grace Victor Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza:

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kabisa yanaonyesha jinsi ambavyo walimu wetu wamekuwa wakikosa nyumba za kuishi, walimu wa sekondari 52,000 hawana mahala pa kuishi na walimu 130,300 wa shule za msingi hawana nyumba za kuishi. Tumesema tunataka kuwa na elimu bora katika nchi yetu na hatufahamu walimu wanaishi wapi.

Je, Serikali sasa haioni ni wakati muafaka sasa wa kuamuru Jeshi la Polisi liweze kujenga nyumba hizi za walimu kama walivyofanya kwa Mererani kuzuia ile migodi yetu, tatizo hili ili liweze kuisha kwa haraka?

Swali la pili, walimu wamekuwa wakikosa udhamini katika mabenki mbalimbali kwa kutokuwa na mali za kudhaminiwa na taasisi alizozitaja Mheshimiwa Naibu Waziri ni hizo ambazo huwezi kudhaminiwa kama huna dhamana ya vitu visivyohamishika kama viwanja, magari na vitu vingine na tunatambua hali za walimu wetu zilivyo.

Je, sasa Serikali haioni haja kwamba ni wakati muafaka Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iweze kuwa dhamana kwa walimu wetu wakati bado wakiwa kazini na siyo baada ya kustaafu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nisisitize kwamba katika jibu langu la msingi ile takwimu niliyoitaja kwa faida ya Bunge lako tukufu haikumaanisha kwamba walimu hao hawana makazi kabisa. Nimesema kwamba walimu hao wanaishi katika aidha, nyumba za kupanga au nyumba zao binafsi, hilo ndilo jibu langu la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kwanza ya swali lake kwamba kwa nini Serikali isiamuru Jeshi la Polisi kujenga

nyumba za walimu nchi nzima, hilo ninaomba sana majeshi yetu yana kazi zake maalum ambayo yamepewa kufanya na waliojenga ukuta wa Mererani siyo Jeshi la Polisi ni Kitengo cha Ujenzi cha Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Tumekuwa tukiwapa kazi nyingi sana, SUMA JKT kujenga nyumba za walimu kujenga nyumba za walimu katika mahali pengi. Hata kwake kule Iringa tumewapa sehemu nyingi tu SUMA JKT kujenga nyumba na tutaendelea kuwapa mikataba ya kujenga nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema kwamba ujenzi wa nyumba ambao unafanywa na Serikali utaendelea kuwa kidogo kidogo kwa sababu unategemea sana bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, napenda nimuondoe wasiwasi kuhusu dhamana. Karibu mabenki yote na taasisi zote zinazokopesha hakuna dhamana zaidi ya mshahara wa mtumishi. Kinachotakiwa tu ni kwamba mtumishi asiwe anadaiwa mikopo mingine hilo ndiyo jambo la msingi, kama mtumishi hadaiwi mikopo mingine anao uwezo wa kukopa na ataamua mwenyewe, je, akope kwa kurejesha miaka mitatu au akope kwa kurejesha miaka 10 au akope kwa kurejesha miaka 25 ni yeye mwenyewe katika makubaliano ya fomu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kuwasisitiza watumishi wote nchi nzima na Wakurugenzi wa Halmashauri ambao wako chini yangu nataka niwaambie kwamba mikopo hiyo ya watumishi ipo, waingie makubaliano maalum na hizo taasisi na mabenki ili kusudi watumishi waweze kukopesha waweze kujenga nyumba zao binafsi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa James Mbatia, swali la nyongeza.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa maendeleo ya Taifa lolote lile yanatokana na mifumo yake ya elimu inayojali utu wa binadamu; na kwa kuwa Walimu ni sehemu muhimu sana katika uzalishaji wa maendeleo endelevu katika Taifa letu.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutenga fungu maalum la fedha hata kama ni kukopa ili kuondoa kero hizi katika sekta ya elimu ikiweko nyumba za walimu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbatia ambaye ni mkereketwa mkubwa sana wa sekta ya elimu napenda nimhakikishie kwamba mawazo yake ni sawa tu na mawazo ya Serikali. Hivi karibuni tumekamilisha kukokotoa gharama zinazohitajika kuweza kukamilisha miundombinu inayohitajika katika sekta ya elimu ili tuanze utekelezaji kwa asilimia 100 wa Sera yetu ya Taifa ya Elimu ya mwaka 2014, hilo analoliongea ni mojawapo ya yale ambayo tumeyaingiza katika hizo gharama na gharama za awali katika rasimu inaonyesha wazi kwamba tunahitaji takribani trilioni 13 ili kuweza kukamilisha miundombinu yote inayohitajika.

Naomba Mheshimiwa Mbatia na Bunge lako Tukufu liweze kuwa na subira, tutakapokamilisha tutafanya majadiliano maalum ili tuweze kupata fedha zinazohitajika kwa sekta ya elimu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 46

**Kukarabati Bwawa la Lukuledi**

**MHE. CECIL D. MWAMBE** aliuliza:-

Bwawa la Lukuledi ambalo huhudumia Kata za Lukuledi, Mpanyani na Chikinja ni muhimu sana kwa wananchi.

Je, Serikali itafanya lini ukarabati wa bwawa hilo kwa sababu kiwango cha maji kinapungua kwa kujaa mchanga?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Jimbo la Ndanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali kupitia Wakala wa Uchimbaji Visima na Mabwawa *(DDCA)* inaendelea na kazi ya usanifu wa kina wa miundombinu ya Bwawa la Lukuledi lililojengwa mwaka 1954 ambalo ukarabati wake utakapokamilika litahudumia wananchi wapatao 11,544 kwenye vijiji vya Lukuledi A, Lukuledi B, Mraushi, Mkolopola, Ndomoni na Naipanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, usanifu huo unahusisha mabwawa mengine mawili yenye uwezo wa kuhudumia wananchi 15,746. Mabwawa hayo ni Bwawa la Mihima litakalohudumia vijiji vya Mihima, Muungano na Mpanyani na Bwawa la Chingulungulu litakalohudumia vijiji vya Chingulungulu, Namatutwe na Namalembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la usanifu huo ni kubaini gharama zitakazohitajika kukarabati mabwawa hayo matatu yenye uwezo wa kuzalisha na kusambaza huduma ya maji kwa wananchi wapatao 27,290.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza ningependa kutambua kazi inayofanyika kwenye Kata ya Mwena, Chikundi pamoja na Chigugu ya

kusambaza miundombinu kwa ajili ya maji na Mheshimiwa Waziri wa Maji ametoa ushirikiano mkubwa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, bwawa hili la Lukuledi tunalolitaja hapa sasa hivi kwa mara ya kwanza kabisa lilichimbwa mwaka 1955 lakini mpaka sasa hivi limekauka zaidi ya mara tano kwa sababu linategemea tu maji ya mvua kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuiongezea nguvu Mamlaka ya Maji Safi Masasi *(MANAWASA)* kwa kazi nzuri inayofanywa na *Engineer* David ili waweze kufikisha maji Kata ya Lukuledi na vijiji vyake vyote maji safi na salama badala ya kuendelea na huo mradi wa bwawa?

Swali la pili, pamoja na nia njema kabisa ya Serikali kutaka kuweka mabwawa kwenye maeneo waliyoyataja hapo ya Chingulungulu, Mihima pamoja na Mpanyani lakini tu niseme wanachokisema hapa sasa hivi, mwaka huu wametenga kazi ya usanifu.

Je, nini nia ya Serikali kuhakikisha wanawaondolea wananchi hawa taabu ya kupata maji kwa siku zijazo kwa sababu bajeti ya mwaka huu inaonesha tu ni kazi ya usanifu peke yake? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kwanza ya swali lake ni kweli kwamba bwawa hili limekuwa linapata matatizo makubwa ya kukauka kwa sababu mbalimbali, lakini miongoni mwa sababu hizo ni kujaa mchanga na matatizo mengine yanayosababishwa na kutotunza mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo lake kwamba tuwaambie *MANAWASA* wapeleke maji katika maeneo hayo badala ya kutegemea bwawa lile, naomba sana nimshauri

tusubiri usanifu wa kina ukamilike, usanifu huo utatushauri kama chanzo hicho kitatosheleza mahitaji ya maeneo hayo na kama usanifu huo utashauri kwamba chanzo hicho hakitatosheleza basi tutaona njia nyingine ya kupata chanzo kingine ikiwemo hiyo ya kuchukua maji kutoka kwenye chanzo kilecha Mbwinji ambacho ndiyo kinategemewa na *MANAWASA,* kwa sasa hivi naomba sana tusimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutachukua maji kutoka Mbwinji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wito wangu kwenye sehemu hii ya swali la kwanza, ninamuomba sana usanifu utakapokamilika, kama utakaposhauri kwamba wananchi watunze mazingira na wengine watapisha katika eneo la mita 500 kutoka kwenye chanzo kwa ajili ya utunzaji wa mazingira ya bwawa basi naomba sana ashiriki kuwaelimisha wananchi wakubali hatua hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ya swali ameonesha wasiwasi kwamba mwaka huu tuna bajeti ya kufanya usanifu peke yake, ndiyo tumetenga shilingi milioni 60 ili tufanye usanifu wa kina na ukamilike na *DDCA* wamepewa hiyo kazi wakamilishe usanifu mwaka huu wa 2017/2018. Watakapotupatia gharama sasa hapo ndiyo tutapanga lini utekelezaji utaanza kwa kushirikiana na Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuondolea wasiwasi kwamba suala hili kwa sababu sasa limeletwa katika utaratibu wa vipaumbele, asiwe na wasiwasi awahakikishie wananchi kwamba tutatekeleza mradi huu ndani ya mwaka mmoja.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa swali hili la Ndanda la Bwawa la Lukuledi

linafanana kabisa na bwawa lililopo Mbulu Vijijini, Bwawa la Mangisa ambalo linahudumia Kata ya Yaeda Ampa, Bashay na Gidihim na hali yake kwa kweli inaelekea kuisha kabisa kwa sababu linakauka.

Je, Serikali itatusaidiaje ili hili Bwawa la Mangisa liweze kupatiwa ufumbuzi ili vijiji nilivyovitaja viendelee kupata huduma ya maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kufanya *clarification* vizuri katika maswali yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la Mbulu kweli kuna changamoto kubwa ya hili bwawa ambalo Mheshimiwa Flatei analizungumzia, lakini naomba nikiri wazi kwamba miundombinu ya mabwawa katika maeneo mbalimbali imeendelea kuathirika siku hadi siku na kushindwa kuhakikisha uwezo wake unapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali hiyo changamoto kubwa ni suala zima ambalo hata Naibu Waziri hapa amezungumza, uharibifu mkubwa wa mazingira katika vyanzo vya maji, watu wanapenda katika maeneo ya mabwawa kuweka mashamba, kinachotokea ni kwamba mvua inavyonyesha udongo unatiririka kutoka mashambani unaenda kujaza katika mabwawa na mabwawa haya yanakufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Flatei tumeisikia hoja yako tutawatuma wataalam kwenda kufanya uhakiki kuangalia nini kinachotakiwa kufanyika pale. Hata hivyo, naomba niwasihi viongozi wote katika maeneo mbalimbali hasa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, wahakikishe kwamba katika suala la vyanzo vya maji hasa mabwawa kuzuia vitendo vya shughuli za kibinadamu hasa

kilimo, kwa sababu jambo hilo linaharibu miundombinu ya mabwawa katika nchi yetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Aisharose Ndogholi Matembe, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 47

**Kuimarisha Elimu na Huduma ya Uzazi wa Mpango**

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE** aliuliza:-

Takwimu zinaonesha kuwa mwaka 2015/2016 wanawake 85 Mkoani Singida walipoteza maisha kutokana na vifo vya uzazi. Aidha, inaelezwa kitaalam asilimia 35 ya vifo hivyo vinaweza kuzuiliwa iwapo huduma za uzazi wa mpango zitazingatiwa na kuimarishwa.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha elimu na huduma za afya ya uzazi wa mpango kwani utumiaji wa huduma hizo kwa sasa unatekelezwa kwa asilimia 19 wakati wastani wa kitaifa ni asilimia 27?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aisharose Ndogholi Matembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu rasmi za sensa mwaka 2012 zinaonesha vifo vitokanavyo na uzazi katika Mkoa wa Singida ni 468 kwa kila wanawake 100,000. Kwa mujibu wa utafiti wa viashiria vya afya na Malaria Tanzania za mwaka 2015/2016 *(Tanzania Demographic Health Surveys*

*2015/2016)* matumizi ya uzazi wa mpango katika Mkoa wa Singida yalikuwa asilimia 38.4 wakati wastani wa Kitaifa ni asilimia 32.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo ya afya katika Mkoa wa Singida wameweza kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo watoa huduma 77 katika kipindi cha mwaka 2015 na idadi watoa huduma ilikuwa 121 kwa mwaka 2016 ili waweze kutoa huduma sahihi za uzazi wa mpango kwa kuzingatia miongozo ya utoaji huduma za uzazi wa mpango zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali inaendelea kutoa elimu juu ya uzazi wa mpango kwa kutumia simu za viganjani, huduma hiyo hujulikana kama *m4RH* na ili kupata elimu hiyo, mhusika anatakiwa kutuma ujumbe wa *m4RH* kwenye namba 15014 na hapo mtu yeyote ambaye ana umri wa miaka 15 hadi 49 wanaweza kupata ujumbe wenye elimu ya uzazi wa mpango. Katika Mkoa wa Singida wateja waliopatiwa huduma ya uzazi wa mpango kwa mwaka 2015 walikuwa 198,822, mwaka 2016 walikuwa wateja 209,511 na mwaka 2017 walikuwa wateja 173,587.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali imeendelea kuboresha huduma za dharura za uzazi ikiwemo upasuaji wa kutoa mtoto tumboni katika Mkoa wa Singida ambapo vituo vya afya vinne vya Ndago katika Halmashauri ya Iramba, Ihanja katika Halmashauri ya Ikungi, Itigi katika Halmashauri ya Itigi na Kinyambuli katika Halmashauri ya Mkalama vimeweza kupata kila kimoja kimepata fedha zaidi ya milioni 500 kwa ajili ya ukarabati wa vituo hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aisharose Matembe swali la nyongeza.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa takwimu zinaonesha Mkoa wa Singida ni miongoni mwa mikoa inayoongoza kwa mimba za utotoni na moja ya sababu ni kutokuimarishwa kwa elimu ya uzazi wa mpango.

Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kuanzisha kampeni ya kitaifa ili kuwawezesha wanafunzi na hasa wa kike kuanzia shule za msingi hadi sekondari kuweza kujitambua na kuepukana na mimba za utotoni? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa hospitali za Mkoa wa Singida pamoja na vituo vya afya vina uhaba mkubwa wa wataalam na vifaatiba. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha hospitali na vituo vya afya vya Mkoa wa Singida vinapatiwa wataalam na vifaatiba vya kutosha ili kuziwezesha hospitali hizo kufanya kazi kwa ufanisi na kuokoa vifo vya akinamama wajawazito na watoto? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Aisharose Matembe kwa kuwa mpiganaji mkubwa sana wa masuala ya afya ya akina mama na watoto katika Mkoa wa Singida na kwa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kwamba tuna changamoto kubwa sana ya mimba za utotoni na takwimu ambazo tunazo zinaonyesha kwamba wastani wa asilimia 27 ya vijana ambao wapo kati ya miaka 15 mpaka 19 aidha, wameshapata watoto au ni wajawazito, hii idadi ni kubwa sana na baadhi ya Mikoa inakaribia asilimia 50. Kwa kutambua hilo, Serikali imeweka mkakati na Wizara tumeanzisha kampeni inayoitwa "Mimi ni Msichana, Najitambua, Elimu Ndio Mpango Mzima." Hii kampeni tayari tumeshaizindua na inaendelea kusambaa nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, ndani ya Wizara sasa hivi tunakamilisha kuandaa mkakati wa afya ya uzazi kwa vijana, ambao itatoa dira na mwelekeo wa nini tunahitaji kufanya hususan katika yale maeneo ambayo mimba za utotoni zimeshamiri. Sambamba na hilo, tumeanzisha *club* katika maeneo mbalimbali hususan katika shule za sekondari kuwajengea uwezo vijana wetu hususan mabinti wa kike kujitambua na kuhakikisha kwamba wanapata elimu ya kutosha kuhusiana na elimu ya uzazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, tafiti zimethibitisha kwamba tunapomnyanyua mwanamke kiuchumi vilevile tunazuia uwezekano wa wale mabinti kupata mimba za utotoni, sambamba na hili kuna miradi ambayo tunaifanyia upembuzi yakinifu sasa hivi ambayo itatoa fedha kidogo kuwajengea uwezo wale mabinti *especially* wale ambao wapo nje ya mfumo wa shule kuweza kujikimu kimapato na hii ni moja ya mkakati ambao tumeuona umekuwa na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka huu wa fedha tumeweza kuongeza bajeti ya mpango wa afya ya uzazi kutoka shilingi bilioni tano mpaka shilingi bilioni 18. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ameuliza nini mkakati wa Serikali kuongeza wataalam na vifaatiba. Katika mwaka huu wa fedha, bajeti ya dawa, vitendanishi na vifaatiba ni bilioni 269 na nimeongelea hapa bajeti ambayo tumeiweka katika *family planning* kutoka bilioni tano mpaka bilioni 18. Tatizo siyo fedha, tatizo niwaombe Waheshimiwa Wabunge watusaidie ni kuwahimiza waganga wetu wa Mikoa na Waganga Wakuu wa Wilaya kuhakikisha kwamba wanaagiza vifaa na dawa ambazo zinahusiana na masuala ya uzazi wa mpango.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa ni tabia ya baadhi ya watoa kutoagiza vifaa hivi kwa sababu wanaona kwamba havina tija au havitoki haraka katika hospitali zao, lakini ni sehemu ya tiba muhimu na dawa muhimu sana

hususan katika upande wa uzazi wa mpango, lakini Serikali itaendelea kutoa elimu hiyo na kuhamasisha watoa huduma kuhakikisha kwamba wanaagiza dawa hizo na sisi kama bohari ya dawa tunazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo ni kweli tumekuwa na changamoto ya uhaba wa watumishi na tunaamini kwamba kadri vibali vinapopatikana tutakuwa tunaongeza wigo wa watoa huduma katika hospitali hizi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Msabaha swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi naomba nimuulize Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Hospitali za Mikoa ya Dar es Salaam, kwenye wodi za akina mama kumekuwa na msongamano mkubwa sana wa mama wajawazito, wengine wanalala wawili na wengine wanalala chini.

Je, Serikali ina jitihada gani za maksudi kuhakikisha hizi wodi za akina mama zinakuwa na mpangilio maalum, mama mjamzito anavyofikishwa hospitalini apate kitanda cha peke yake, kwa sababu wako wawili na kulala watu wawili pia inachangia kuambukiza maradhi?

Je, Serikali ina mkakati gani...

**NAIBU SPIKA:** Umeshauliza swali Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunachokifanya Serikali ni kuhakikisha kwamba tunaboresha mnyororo wa utoaji wa huduma za afya kwa kuboresha mifumo ya rufaa na moja ya mikakati ni hii ambayo

tumeendelea kuisema na nimeigusia hapa kuboresha vituo vya afya, hospitali za Wilaya na hospitali za Rufaa za Mikoa ili ziweze kutoa huduma za uzazi salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema jana, kwangu siyo faraja sana kusikia kwamba wakina mama 100 wamezaa katika Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili. Tunachotaka kuona pale Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili ni *case* zile ambazo zipo *complicated*, kesi nyingine zote sasa hivi tumejenga uwezo katika vituo vyetu vya afya, hospitali zetu za Wilaya na Hospitali za Rufaa za Mikoa ili ziweze kutoa huduma. Nitoe rai kwa wananchi kuzitumia hospitali zetu hizi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munira swali fupi.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashuhudia wanawake wengi wakati wanapojifungua wanapata maradhi ya *fistula,* je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha wanawake hawa wanaojifungua wanaepukana na maradhi haya ya *fistula?(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa swali zuri ambalo ameuliza Mheshimiwa Munira.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanamke kupata *fistula* maana yake ni kwamba hakupata huduma nzuri wakati alipokuwa anakaribia kujifungua na hiyo ndiyo tafsiri yake kubwa ya msingi, kwa sababu *fistula* haipaswi kutokea kama mwanamke alipata uangalizi mzuri wakati anajifungua. Katika changamoto hiyo tumeiona, tunaendelea kuboresha utoaji wa huduma, kutoa elimu kwa watoa huduma wa afya,

vilevile kuhakikisha kwamba tunazisogeza huduma za dharura za kumtoa mtoto tumboni karibu zaidi na wananchi ili hali ile ambayo inatokana na mwanamke kukaa *labor* kwa muda mrefu tuondokane nayo.

Na. 48

**Mpango wa Kutoa Dawa za Ugonjwa wa Kisukari Bure**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza:-

Kuna ongezeko kubwa la wagonjwa wa magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo kisukari ambapo matibabu yake ni ya muda mrefu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa dawa za ugonjwa wa kisukari bure kama ilivyofanya kwa ugonjwa wa kifua kikuu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Afya ya mwaka 2007 inatambua uwepo wa wagonjwa wasio na uwezo wa kuchangia gharama za huduma za afya ikiwa ni pamoja na wale waliokuwepo katika makundi maalum ya kijamii, wazee walio na umri wa zaidi ya miaka 60 ambao hawana uwezo wa kipato, watoto wa umri wa chini ya miaka mitano, watoto walio katika mazingira hatarishi, wanawake wajawazito na watu wasiojiweza kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kundi hili pia wapo wagonjwa wenye magonjwa sugu kama saratani, wanaoishi na virusi vya UKIMWI, kisukari, magonjwa ya moyo, pumu, selimundu, kifua kikuu, ukoma na magonjwa ya akili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Chama cha Wataalam wa Ugonjwa wa Kisukari Nchini, inaendesha Programu ya Kitaifa ya Kisukari ambayo inajulikana kama *National Diabetic Program,* ambapo imeanzisha vituo vya matibabu ya kisukari vipatavyo 169 katika Hospitali za Wilaya, Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Rufaa za Kanda na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Aidha, jumla ya madaktari na wauguzi 1,925 wamepatiwa mafunzo maalum ya kutoa huduma kwa wagonjwa wa kisukari. Lengo ni kuwapatia wagonjwa wote wa kisukari huduma bora na za bure za matibabu kama ilivyoainishwa katika Sera ya Taifa ya Afya. Hadi hivi sasa Serikali imetoa matibabu na dawa ya bure kwa wananchi wapatao 5,386.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iko katika mchakato wa kuainisha idadi na mahitaji ya wagonjwa wa kisukari nchini. Pindi kazi hii itakapokamilika Serikali itatoa mwongozo utakaosimamia vizuri zaidi matibabu ya wagonjwa wa kisukari nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa kwenye jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri ameonesha kwamba huduma hizi sasa zinaanza kutolewa kuanzia Hospitali ya Wilaya, na ni ukweli usiopingika kwamba wananchi wetu wengi wapo vijijini.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha huduma hizi katika vituo vya afya ili kupunguza adha ya wananchi wetu kutembea kwenda Hospitali ya Wilaya?

Swali la pili, miongoni mwa magonjwa yasiyoambukiza ni pamoja na kisukari, hivi sasa kuna ujenzi unaoendelea wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini kule

Mtwara, amesema kwamba hospitali za rufaa za kanda zitatoa vilevile huduma hii katika ngazi ya kanda.

Je, Serikali imejiandaaje sasa itakapofunguliwa Hospitali ya Kanda ya Kusini ambayo inajengwa Mtwara, kwamba huduma ya saratani pia itatolewa katika hospitali hiyo ili kuwapunguzia adha Wanamtwara kwenda Hospitali ya *Ocean Road* iliyopo Dar es Salaam? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Abdallah Chikota kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaendelea kuifanya na kwa kuwapigania wananchi wake wa Jimbo lake na Mkoa wa Mtwara katika masuala yote yanayohusiana na afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kwamba kumekuwa na ongezeko kubwa sana la magonjwa yasiyoambukizwa, siyo tu kisukari, lakini hata vilevile kiharusi, masuala ya *pressure*, magonjwa ya figo. Serikali inaendelea na utaratibu wa kujenga uwezo katika mnyororo wake wa utoaji wa huduma, sasa hivi tuko katika ngazi ya Wilaya lakini tunaendelea kuboresha kushuka katika ngazi ya vituo vya afya na mwisho tutashuka mpaka katika *dispensaries.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme tu kwamba huduma za awali kwa magonjwa kama haya ya upimaji wa sukari, upimaji wa *pressure*, yote yanafanyika katika ngazi zote za mnyororo, lakini dawa kwa mfano, *insulin* ambazo zinahitaji utaalam zaidi zinapatikana katika ngazi ya Wilaya. Lakini tutaendelea kuboresha utaratibu huu kadri tutakapokuwa tunajenga uwezo katika mnyororo wetu wa utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ameuliza, je, Serikali itakuwa tayari kuanzisha huduma za saratani katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ambayo inajengwa

Mtwara. Kwa mujibu wa taratibu katika ngazi hiyo ya Rufaa ya Kanda, moja ya huduma ni pamoja na upatikanaji wa huduma za saratani. Kwa hiyo, pindi hospitali hii itakapokuwa tayari huduma hiyo nayo tutaiweka. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dunstan Kitandula, swali la nyongeza.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza:

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa letu linakabiliwa na tatizo kubwa ambalo kimsingi ni janga la utapiamlo na lishe iliyopitiliza, hii lishe iliyopitiliza ndiyo chimbuko sasa la magonjwa kama kisukari na magonjwa ya moyo.

Je, Serikali ipo tayari kwa maksudi kabisa kuandaa semina kwa Bunge zima ili Wabunge hawa wakielimika iwe chachu ya kutoa elimu kwa jamii nchini?*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Kitandula ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge, Masuala ya Lishe, kwa kusimamia vizuri masuala ya lishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tumekuwa na changamoto kubwa sana ya utapiamlo pamoja na suala la lishe iliyopitiliza ambayo kwa lugha ya kitaalam tunaita viribatumbo *(obesity)* na sisi kama Serikali tumeweka mkakati ambao ni jumuishi na ambao ulizinduliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka jana, ambao unashirikisha sekta zote kuhakikisha kwamba tunajenga Tanzania yenye lishe. Wizara tupo tayari kutoa semina kwa Wabunge ili kuwajengea uwezo na uelewa na wao kwenda kusemea masuala ya lishe na viribatumbo katika jamii wanazotoka.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hivyo viribatumbo utuletee hiyo semina kwa sababu huo ni msamiati mpya kabisa.

Tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Prosper Joseph Mbena, Mbunge wa Morogoro Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 49

**Uundaji wa Vyombo vya Kusimamia Matangazo Kwenye Vyombo vya Habari**

**MHE. PROSPER J. MBENA** aliuliza:-

Kutokana na kuongezeka kwa matangazo ya biashara kwenye vyombo vya habari, upo uwezekano wa baadhi ya matangazo hayo kuwakera na kuleta hisia tofauti kwa baadhi ya watu na hasa watoto kutokana na maudhui mabaya ya baadhi ya matangazo haya.

(a) Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kuunda chombo cha kusimamia maudhui ya matangazo ya kibiashara ili kuweka na kusimamia taratibu na kanuni za matangazo?

(b) Je, ni idara gani ya Serikali inahusika moja kwa moja na malalamiko ya wananchi dhidi ya kampuni na taasisi zinazotoa matangazo yenye athari kwa jamii?

(c) Je, ni hatua gani zinachukuliwa dhidi ya kampuni hizo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prosper Joseph Mbena, Mbunge wa Morogoro Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tayari ina vyombo vya kusimamia maudhui ya vyombo vya habari nchini, yakiwemo maudhui katika matangazo. Vyombo hivyo ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* inayoundwa chini ya kifungu cha Sheria Na. 4 cha Mamlaka ya Mawasiliano Na. 12 ya mwaka 2003, ambayo ina Kamati ya Maudhui iliyoundwa chini ya kifungu cha 26 cha sheria hiyo na marekebisho yake katika kifungu cha 173 cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroni na Posta *(EPOCA)* ya mwaka 2010. Kamati hii ndiyo inayosimamia maudhui ya matangazo ya kielektroniki (redio, *television* na mitandao ya kijamii).

Mheshimiwa Naibu Spika, chombo cha pili ni Bodi ya Filamu Tanzania ambayo vilevile inasimamia maudhui katika picha jongevu zinazorushwa katika majumba ya sinema, hadharani vilevile katika michezo ya kuigiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Habari Maelezo ni chombo cha tatu ambacho kimehuishwa chini ya kifungu cha Sheria Na. 4 na Sheria Na. 5 vya Sheria ya Huduma ya Habari Namba 12 ya mwaka 2016 kinachosimamia maudhui katika machapisho mbalimbali yakiwemo magazeti, majarida pamoja na vipeperushi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali inapobainika bila kutia shaka kuwa kampuni, asasi au taasisi imechapisha ama kutoa tangazo lenye athari kwa jamii. Hatua hizo ni pamoja na kupewa onyo, kufungiwa kutoa huduma kwa kipindi kitakachotajwa au kufungiwa kabisa kutokujihusisha na utangazaji au uchapishaji wa habari pamoja na matangazo. Serikali inaendelea kuhimiza jamii nzima kuendelea kuzingatia sheria na taratibu zilizopo katika kusambaza habari mbalimbali kwa jamii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Prosper Joseph Mbena, swali la nyongeza.

**MHE. PROSPER J. MBENA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na ninachukulia

kwamba majibu haya yamezingatia mtoto katika kumhakikishia haki zake na kumlinda asidhalilishwe. Sitakuwa na swali la nyongeza. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Catherine Magige swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuna Kamati ya Maudhui, siku za karibuni tumekuwa tukishuhudia wasanii wetu wengi wakifungiwa nyimbo zao, wasanii ambao wamehangaika kutafuta pesa za kurekodi kwa shida na ukizingatia kuna uhaba wa ajira.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akatuambia Kamati hiyo ya Maudhui imeshindwa kazi, kwa sababu wamekuwa wanaachia mpaka nyimbo zinatoka ndiyo wanakuja kuwafungia wasanii wetu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kila Taifa lina utamaduni wake na lazima liulinde kwa udi na uvumba. Tunachokifanya sio kwamba tuna vita na wasanii wetu, hapana! Lengo letu ni kulinda maadili ambayo katika kipindi hiki cha utandawazi na maendeleo ya kasi ya kiteknolojia na habari, kuna mmomonyoko mkubwa sana wa maadili katika nchi yetu ni lazima tuchukue hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachokifanya hapa siyo kitu cha pekee duniani, kila mtu anafanya hivyo na hawa wasanii wetu tumeshawasamehe wasirudie tena. Nitoe mfano mmoja mdogo…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwanamuziki Rick Ross ambaye amepiga muziki pamoja na kijana wetu nyota wa muziki Diamond hapa, wimbo wao huu wa wakawaka, huyo mwanamuziki miezi michache iliyopita amepata matatizo Marekani kwa kuimba wimbo unaoitwa *U.O.E.N.O* ambao maudhui yake yanaleta picha ya kwamba anaunga mkono ubakaji. Marekani nzima akina mama walikuja juu, wimbo ukaondolewa kwenye *televisions* zote, lakini na yule kijana akaomba radhi kwa wanawake wote kwamba amewaudhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tumekuwa kokoro, tupokee kila kitu, kwa sababu hatuna utamaduni. Baba wa Taifa alisema mwaka 1962, Taifa lisilo na utamaduni wake ni Taifa mfu nasi hatuwezi kukubali kuwa Taifa mfu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yanayotokea Tanzania yanatokea duniani kote. Nitoe tu maelezo kidogo, maana Viongozi wetu hapa wanalalamika ni kwa sababu dunia pana hawajaielewa. Davido mwanamuziki maarufu duniani ambaye amepiga na kijana wetu Diamond hapa kafungiwa nyimbo zake mbili na *Nigerian Broadcasting Corporation* mwaka huu. Siyo huyo tu, Wizkid kafungiwa nyimbo zake, Nine Eyes kafungiwa nyimbo zake, sijasikia Wabunge wa Nigeria wakilalamikia sheria zao wenyewe, sisi ni Wabunge kazi yetu kubwa ni kuhakikisha jamii inaheshimu, inalinda sheria za nchi na tutaendelea... *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa mwisho, Koffi Olomide amepiga wimbo unaitwa Ekotite, huu wimbo ni marufuku kupigwa Congo *(DRC)...*

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba

Waheshimiwa Wabunge mnaosafiri kwenda Congo, unaambiwa tukupigie wimbo gani ukisema Ekotite watakushangaa! Huo wimbo ni matusi wameufungia. Sisi hapa Wabunge tunakuwa wa kwanza kuruhusu nchi yetu iwe kokoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, *BBC* ambayo iko Uingereza ambako ndugu zangu wanadhani ndiko mwanzo wa ustaarabu, wamefungia nyimbo 237 katika historia yao, hapa tunalalamika nyimbo mbili kufungiwa. Tutaendelea kufungia kulinda utamaduni wa nchi yetu. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, sasa aulize swali lake.

Na. 50

**Tathmini ya Utendaji Kazi wa Jeshi la Polisi Nchini**

**MHE. KHATIB SAID HAJI** aliuliza:-

Kuchelewesha haki ni kunyima haki.

Je, Jeshi la Polisi limejitathmini juu ya utendaji wake, hususan katika Idara ya Upelelezi wa Makosa mbalimbali kabla ya kuyafikisha mashtaka mahakamani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, upelelezi wa makosa ya jinai unafanywa kwa kuzingatia sheria mbalimbali kama vile Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya 20 Marejeo ya mwaka 2002, Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 Marejeo mwaka 2002 na Sheria ya Ushahidi Sura ya 6 Marejeo ya mwaka 2002, pamoja na kuzingatia kanuni za kiutendaji za Jeshi la Polisi *(Police General Orders)* na sheria nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya lengo la upelelezi wa makosa ya jinai ni kukusanya ushahidi utakaothibitisha kosa lililotendeka na kuripotiwa kituoni. Aidha, kuna baadhi ya makosa yaliyotendeka huhitaji muda mrefu ili ushahidi wake kuweza kupatikana, mathalani makosa ya mauaji na yanayofanana na hayo. Inapodhihirika kuwa kuna ushahidi uliopatikana unaweza kuthibitisha kosa, jalada hupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hatua za kusomwa na kuandaa mashtaka pale ambapo wanaona ushahidi umejitosheleza na kupeleka mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi hufanya tathmini ya kutosha katika utendaji wake kupitia Kitengo cha Ndani cha Tathmini na Uangalizi *(Internal Monitoring and Evaluation)* na kutoka kwa Waangalizi wa Nje *(External Oversight)* ambao hulisaidia Jeshi la Polisi kurekebisha kasoro mbalimbali za kiutendaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib Haji swali la nyongeza.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ufanisi na utendaji wa Mahakama unategemea ushahidi katika

utendaji wake, lakini imekuwa ni jambo la kawaida ukiwa katika Mahakama zetu mara baada ya kusomwa Shauri Namba, Waendesha Mashtaka kusimama na kuiambia Mahakama tunaomba Mheshimiwa Hakimu au Jaji uahirishe shitaka hili kwa sababu upelelezi haujakamilika, hivyo ni vitu vya kawaida sana.

Je, Serikali kwa kushindwa kupeleka ushahidi haraka katika Mahakama kwa kesi zinazoendelea ndiyo chimbuko la kusababisha mlundikano wa mahabusu katika Magereza yetu na jambo hilo ndilo linalosababisha wananchi wengi kukosa imani na Mahakama na kuona hazitendi haki, je, hamuoni kwamba kuchelewesha kupeleka ushahidi katika Mahakama mnasababisha lawama kwa Mahakama ambazo kimsingi siyo za kwao? *(Makofi)*

Swali la pili, katika nchi yetu lilitokea tukio kubwa na baya la ugaidi ambalo lilisababisha maisha ya watu wetu kupotea katika Ubalozi wa Marekani pale Dar es Salaam. Kuna watuhumiwa ambao walichukuliwa hapa kwenye nchi yetu na wakapelekwa Marekani kwa ajili ya mashtaka hayo na upelelezi wa makosa hayo, lakini haikuchukua zaidi ya miaka miwili watuhumiwa wale walionekana hawakuwa na makosa na wakaachiwa huru Marekani na Tanzania.

Je, ni kwa nini mpaka leo watuhumiwa wa ugaidi, Mashekhe wa Uamsho kutoka Zanzibar ambao hawakuua hata kuku katika mashtaka yao, mpaka leo mmeendelea kuwashikilia ilihali mmeshindwa kupeleka ushahidi. Mpaka lini Serikali mtaendelea kuwashikilia wazee wa watu wale na mmeshindwa kuthibitisha makosa yao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la upelelezi ni jambo la msingi ili kuhakikisha kwamba haki inatendeka. Lazima Jeshi la Polisi lifanye uchunguzi wa kina na kujiridhisha juu ya makosa ambayo yamefanywa na mtuhumiwa ili hatimae

mtuhumiwa yule aweze kutendewa haki. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Mbunge aelewe kwamba siyo dhamira ya Serikali wala Jeshi la Polisi kuchelewesha upelelezi, lakini kuna aina ya makosa ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi ya ziada ambayo yanahusisha taasisi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kunahitaji kufanyika utafiti kutoka katika vyombo na mamlaka nyingine, masuala ya mawasiliano kwa mfano *TCRA,* kuna masuala yanayohusu uhamiaji, masuala ya taasisi nyingine mbalimbali za ndani na nje ya nchi. Kwa hiyo, ili kuweza kuhakikisha kwamba mtuhumiwa yule anatendewa haki lazima Jeshi la Polisi lipate muda wa kutosha. Hakuna Serikali ama chombo chochote cha Serikali kinachohitaji kumkomoa mwananchi wake, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kuhusiana na suala la watuhumiwa wa Uamsho. Tuhuma ambazo zinawakabili watu hawa ni nzito, kwa hiyo basi ni lazima uchunguzi wa kina vilevile ufanyike ambao utahitaji muda. Kwa hiyo, naomba jambo hili kwa kuwa liko Mahakamani siyo busara kwa mujibu wa sheria za nchi na Katiba ya nchi hii kulijadili katika Bunge hili Tukufu, tuacha mamlaka husika na mhimili wa dola ufanye kazi yake.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, Mbunge wa Chemba, sasa aulize swali lake.

Na. 51

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi na Nyumba za Polisi Chemba**

**MHE. JUMA S. NKAMIA** aliuliza:-

Wilaya ya Chemba haina Kituo cha Polisi; je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Polisi na nyumba za askari?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Nkamia, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Jeshi la Polisi lina uhaba wa vituo vya polisi pamoja na nyumba za kuishi Askari kote nchini ikiwemo Wilaya ya Chemba. Ili kutatua changamoto hii Jeshi la Polisi linashirikisha wadau wa eneo husika pamoja na wadau wengine wa maeneo kwa maendeleo ili kufanikisha azma ya Serikali ya kujenga vituo vya kisasa vya polisi pamoja na nyumba za kuishi askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilayani Chemba Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, wananchi na wadau wengine wapo kwenye hatua za awali za kuanza ujenzi wa kituo cha polisi. Aidha, kwa sasa mchoro wa ramani ya kituo na gharama za ujenzi *(BOQ)* zimeshakamilika na ukusanyaji wa mahitaji ya ujenzi unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini jitihada hizi zitaungwa mkono na Mheshimiwa Mbunge ili kuhakikishia wananchi wake usalama wao pamoja na mali zao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Juma Nkamia swali la nyongeza.

**MHE. JUMA S NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema Jeshi la Polisi likishirikiana na wadau Wilayani Chemba wamekaribia kuanza ujenzi ningeomba anihakikishie ni wadau gani hawa ambayo yeye ana taarifa kwamba tayari wanaanza kushirikiana kujenga kituo cha polisi?

(b) Binafsi nimechangia kwa kiwango kikubwa sana katika ujenzi wa kituo kipya cha Polisi kule Kwa Mtoro na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani Komredi Mwigulu alinihaidi hapa ndani ya Bunge kwamba kutokana na mazingira ya Kwa Mtoro hadi Makao Makuu ya Wilaya ya Chemba ambao ni karibu kilometa zaidi ya 120 Serikali ingeweza kuwapatia askari wale gari la kuweza kuwasaidia kwa sababu wanapita kwenye Hifadhi ya Swagaswaga na kuna wanyama wakali.

Je, hilo gali litapatikana lini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimejibu katika swali langu la msingi nilieleza kwamba Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ikishirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo wananchi wameanza mchakato wa ujenzi wa kituo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusiana na swali lake la pili kwanza nimpongeze kwa juhudi zake za kuchangia maendeleo ya Jeshi la Polisi katika Wilaya yake, lakini kuhusiana na hali ya Mheshimiwa Waziri nataka nimhakikishie kwamba ahadi ya Mheshimiwa Waziri kama alitoa iko palepale tatizo linalokwamisha ni kwamba bado magari hayo hayajapatikana, naamini kabisa wakati ambapo tumepata magari ya kutosha basi ahadi hiyo itatekelezwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani Mbunge wa Uzini sasa aulize swali lake.

Na. 52

**Utekelezaji wa Mradi Mkubwa wa Bwawa la Kidunda**

**MHE. SALUM MWINYI REHANI** aliuliza:-

Serikali inatekeleza mradi mkubwa wa umeme wa Bwawa la Kidunda ambapo pia kutakuwa na miradi ya kilimo na ufugaji samaki.

(a) Je, kuna tathmini ya kitaalamu iliyofanyika ya kudhtibiti kemikali zinazotokana na utumiaji mkubwa wa dawa za kudhibiti magugu kwenye mashamba ya miwa na mpunga na utumiaji wa mbolea za SA ambazo husababisha uharibifu wa ardhi?

(b) Je, Serikali inaweza kuleta Bungeni ripoti ya tathmini pamoja na *Environmental Impact Assessment* juu ya mradi huo?

(c) Je, mradi wa umwagiliaji utachukua ekari ngapi na imepanga kulima nini katika mashamba hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani, Mbunge wa Jimbo Uzini, lenye sehemu (a) (b), (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kulinga na tathmini ya athari za mazingira iliyofanyika Bwawa la Kidunda halitakuwa na athari za kikemikali za kudhibiti magugu kwenye mashamba ya miwa na mpunga kwani mashamba hayo yatakuwa upande wa chini wa bwawa yaani *downstream* ambapo kemikali haziwezi kurudi nyuma kuingia kwenye bwawa. Ripoti ya mazingira imeainisha athari zote zinazotarajiwa na namna ya kukabiliana nazo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaweza kuleta

Bungeni cheti cha mazingira kilichotolewa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* kuhusu mradi wa Kidunda.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Bwawa la Kidunda ni mahsusi kwa ajili kuhifadhi maji kwa matumizi ya majumbani na viwandani. Hata hivyo, kiasi cha maji lita milioni 432 kwa siku sawa na mita tano za ujazo kwa sekunde, yatatumika kwa ajili ya umwagiliaji na shamba namba 217 la Mkulazi lenye hekta 28,000 zinazofaa kwa kilimo cha miwa na mpunga.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salum Rehani swali la nyongeza.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa kumuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza, tunataka tupate ripoti na siyo cheti kwa sababu cheti kinakuwa ni uthibitisho tu, lakini ripoti ndiyo kitu ambacho tunaweza kuona athari iliyopo au hakuna athari.

Pili, nilitaka kuelewa kwamba bwawa lile liko maeneo ya upande wa Morogoro, lakini wananchi wa pale wanategemea sana kuzalisha pamoja na mazao ya miwa na mpunga lakini na mazao mengine mbalimbali ambayo yako katika eneo lile.

Je, wasiwasi wangu uliokuweko maporomoko ya maji na mwelekeo wa maji ambayo yanashuka katika lile bwawa hayatoweza kuathiri mmomonyoko na uharibu wa lile bwawa pengine labda ikasaidia kuingia na kufanya *contamination* ya maji ambayo yatakuwa yanaingia katika maeneo yale.

Je, Serikali iko tayari kuweka utaratibu mzuri wa kilimo ambacho kitakuwa hakitumii kemikali ili kuepukana na athari za kikemikali katika maji yale ambayo wanatumia binadamu na kilimo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu kwa kifupi

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ameomba kwamba kile cheti cha *NEMC* kiwasilishwe Bungeni, lakini kwa mujibu wa swali lake aliuliza, je, Serikali inaweza kuleta Bungeni ripoti ya tathmini pamoja na *Environmental Impact Assessment* juu ya mradi huo. Tumesema ndiyo tunaweza, sasa kama swali la pili unataka tulete basi utuagize tulete tutaleta, lakini kwa mujibu wa swali lako tumeshajibu kwamba tunaweza tukaleta.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kama ilivyojibiwa kwenye swali la msingi na Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba ripoti ya *NEMC* ipo na imeweka tayari na *Environmental Management Plan.* Kwa hiyo, hakutakuwa na athari ya aina yoyote pale ambapo kutakuwa na athari basi ripoti ile itafuatwa wataweka utaratibu kuhakikisha kwamba madhara ya aina yoyote kuhusu kemikali hayatajitokeza, madhara kuhusu mmomonyoko pia hayatajitokeza. Kwa sababu utokaji wa maji kwenye bwawa utakuwa *controlled* kulingana na matumizi ya kupeleka maji kwenye mashamba pamoja na kupeleka maji Mto Ruvu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa mujibu wa majibu haya Mheshimiwa atapaswa kuwasiliana na Kamati yake ili taarifa hiyo ije kwa utaratibu wa Kibunge, siyo wa kutuletea hapa kwa sababu huwa hatuna utaratibu wa kuzipokea hapa ndani. Kwa hiyo, kama bado atakuwa anaihitaji hiyo ripoti afuate utaratibu uliopo Kibunge ili muweze kupeleka huko hiyo taarifa.

Waheshimiwa Wabunge, nimpe nafasi Mheshimiwa Omary Mgumba aulize swali fupi.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza kuhusu Bwawa la Kidunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu mradi huu mpaka sasa *accessibility* ya kufika sehemu ambayo inajengwa bwawa haifikiki kirahisi ni pamoja na utekelezaji huu, lakini kulikuwa na mpango wa kuiboresha na kuitengeneza barabara hii ili ujenzi huu uweze kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua katika upande wa Serikali, ni lini barabara hii itaanza kujengwa ili kurahisisha ujenzi wa bwawa huu kuanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mgumba kwa kuuliza swali ambalo ni la msingi, lakini jibu ni moja dogo kwamba katika mwaka wa fedha unaokuja tumetenga fedha, kwa hiyo utaiona hiyo fedha kwenye wasilisho la bajeti ya Waziri wa Maji ambapo tutaanza na ujenzi wa barabara ili kumwezesha Mkandarasi sasa awe na uwezo kwenda kujenga bwawa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa swali la mwisho, Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 53

**Mradi wa Maji wa Ntomoko - Kondoa**

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha mradi wa maji wa maporomoko ya Ntomoko Wilayani Kondoa?

**NAIBU WA WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa

Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Ntomoko ulilenga kutoa huduma katika vijiji 18 vya Wilaya ya Kondoa na Chemba lakini kutokana na uwezo mdogo wa chanzo kumesababisha kutokidhi mahitaji ya huduma ya maji katika vijiji hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwezi Novemba 2017 Wiraza kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI iliunda timu ya pamoja ya Wataalam kwa ajili ya kufanya mapitio ya usanifu wa kina wa mradi huo pamoja na kutafuta chanzo kingine mbadala ili kuongeza wingi wa maji utakaokidhi mahitaji ya wananchi katika vijiji hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mapitio ya usanifu wa kina timu hiyo ilibaini kuwa chanzo cha Ntomoko hakina tena uwezo wa kuhudumia vijiji hivyo. Ili kukidhi mahitaji ya maji kwa vijiji hivyo, Serikali imepanga kukarabati miundombinu iliyoko pamoja na kujenga bwawa lenye mita za ujazo milioni 2.8 kwenye eneo la Kisangali katika kijiji cha Mwisanga litakalotoa huduma kwa vijiji vyote 18. Usanifu wa bwawa hilo pamoja na bomba kuu kutoka kwenye chanzo hadi makutano ya kijiji cha Lusangi umeshafanyika. Ujenzi huo unatarajiwa kuanza katika bajeti ya mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto zilizojitokea awali juu ya ukarabati wa miundombinu ya mradi huo, Wizara ya Maji na Umwagiliaji imeiagiza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira *(DUWASA)* kutekeleza ukarabati wa mradi huo badala ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felister Bura swali la nyongeza.

**MHE. FELISTER A BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maporomoko ya

Ntomoko ni janga kwa wananchi wanaoishi kandokando ya maporomoko haya. Wananchi wa Wilaya ya Chemba vijiji kumi na vijiji vitatu vya Wilaya ya Kondoa wamesubiri mradi huu kwa muda mrefu sana na fedha zilishatolewa zaidi ya bilioni mbili kwa ajili ya kukarabati mradi ule, watumishi ambao walizembea mradi ule hawajachukuliwa hatua yoyote. Wananchi wanateseka na hakuna jibu lolote linaloonesha kwamba hivi vijiji vitapata maji hivi karibuni.

Je, watumishi waozembea na wakapoteza zaidi ya shilingi bilioni mbili na kufanya mradi huu ukasimama wamechukuliwa hatua gani?

Swali la pili, mradi huu umekwishatembelewa na viongozi wengi na tumekwishachangia mara nyingi na Wabunge wa maeneo yale mimi na Mheshimiwa Juma Nkamia na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji sasa hivi hatueleweki kwa wananchi.

Je, kuna mkakati gani wa haraka wa kuwapatia wananchi wa vijiji vile maji ili wasiendelee kuhangaika kwa sababu hata *DUWASA* wenyewe hawajapata fedha kwa ajili ya ule mradi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

**NAIBU WA WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nimpongeze Mama yangu Felister Bura kwa namna ya kipekee anavyowapigania wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa ambalo nashukuru sana ni taarifa ambayo amenipa kama Naibu Waziri wa Maji, nataka nimhakikishie fedha za Serikali haziliwi bure. Kama kutakuwa na watumishi ambao kwa kuzembea au kwa maksudi fedha zile zimepotea, tutafanya mawasiliano ya haraka na watu wa Kondoa katika kuhakikisha hatua za haraka zitachukuliwa kwa watumishi wale ambao wamefanya uzembe wananchi waweze kupata taabu.

Swali lake la pili, amesema huu ni mradi wa muda mrefu sana nataka nimuhakikishie sisi ni Wizara ya Maji na jukumu letu ni kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama yenye kuwatosheleza na ndiyo maana tumeahidi kwamba katika bajeti hii ya mwaka 2018/2019 tumeshatenga fedha ili katika kuhakikisha mradi ule uweze kukarabatiwa kwa haraka ili wananchi wake waweze kupata majisafi salama na ya kuwatosheleza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kumfahamisha Mheshimiwa Felister Bura kwamba kuna hatua za dharura ambazo tunaendelea nazo, tunachimba visima katika vijiji vyote eneo la Kondoa na tumeshaanza na visima 15 ili wananchi waendelee kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu, nitaleta kwenu matangazo tuliyonayo halafu baadae maelezo ya Mheshimiwa Spika.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na tangazo la wageni waliotufikia leo, tunao wageni waliopo Jukwaa la Spika japo naona wageni ni zaidi ya wawili, Makatibu Mezani mnisaidie kupata majina ya wageni wengine ninaowaona kule juu. Tunao wageni wawili wa kwangu ambao ni viongozi wa Taasisi ya Umoja wa *Amani Group Tanzania,* ambayo Makao Makuu yake ni Jijini Dar es Salaam, wageni hao ni Ndugu Wilson George Munguza ambaye ni Rais wa Taasisi ya Umoja wa *Amani Group Tanzania*, pili ni Ndugu Hassan Omary Dinya - Katibu Mwenezi wa Taasisi ya Umoja wa *Amani Group Tanzania,* karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine walioko Jukwaa la Spika hawa ni wageni ambao wengine wameambatana naye lakini huyu ni mgeni wa Mheshimiwa Spika ambaye ni Kaimu Balozi wa

Marekani nchini Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Inmi Patterson ambaye ameambatana na Maofisa wake kutoka Ubalozi wa Marekani, karibu sana Mheshimiwa Balozi Bungeni. *(Makofi)*

Lakini pia tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali tutaanza na wageni 26 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanamaombi wa Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Ndugu Angelina Sakarani, karibuni sana. Aidha, tunao pia wageni 25 wa Mheshimiwa Sonia Magogo ambao ni wanakwaya na wanamaombi kutoka Da es Salaam wakiongozwa na Mchungaji Ibrahimu Chegere, karibuni sana. Pia mgeni wa Mheshimiwa Dotto Biteko ambaye ni Naibu Waziri wa Madini ambaye ni Mtaalam wa Utafiti wa Madini Ndugu Farida Batenga kutoka Nachingwea mkoani Lindi, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Flatei Gregory Massay ambao ni Wanavitongoji na Wenyeviti wa Vijiji kutoka Mbulu Mkoa wa Manyara, karibuni sana, tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Joyce Sokombi ambao ni ndugu zake kutoka Mkoani Dodoma, karibuni sana. Pia wageni wawili wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambao ni ndugu zake kutoka Mkoani Mbeya, karibuni sana. Aidha, tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Cosato Chumi ambao ni wadogo zake kutoka Dar es Salaam, Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Anna Lupembe anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kutakuwa na Ibada katika Ukumbi wa *Pius Msekwa Chepel*, gorofa ya pili, leo siku ya Jumanne tarehe 10 Aprili, 2018, mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge Saa Saba mchana. Aidha, Mchungaji Chegere kutoka Dar es Salaam ata hudumu katika ibada hiyo Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria ibada hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia ninayo maelezo ya Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge naomba utulivu kidogo.

Ninayo maelezo ya Mheshimiwa Spika kuhusu tukio lililotokea Bungeni tarehe 9 Aprili, 2018

Jana Jumatatu tarehe 9 Aprili, 2018 takribani saa 1:20 usiku wakati Kikao cha Bunge kikiendelea kulitokea tukio la mlipuko wa kifaa cha kielektroniki cha kuchajia simu ya mkononi yaani *power bank.* Mlipuko huo ulisababisha harufu kali na kutanda moshi katika Ukumbi wa Bunge hasa upande wa kulia wa Spika.

Kwa mujibu wa maelezo ya askari wa Bunge waliokuwepo ukumbini *(Serjeant-At-Arms)* mlipuko huo ulitokea kwenye *power bank* iliyokuwa ina-*charge* simu mbili kwa pamoja kwenye *draw* ya meza ya Mheshimiwa Richard Philip Mbogo. *Power bank* hiyo iliteketea kabisa na wakati inaungua ilianguka chini na kuunguza sehemu ya *carpet* chini na pembeni ya kiti cha Mbunge huyo.

Katika tukio hilo hakukuwa na majeruhi isipokuwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walipata mshituko, baadhi yao walikimbia nje ya ukumbi wa Bunge na waliobaki ndani ya Ukumbi walipaliwa na moshi na kuanza kukohoa. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, hali hii ilisababisha Mwenyekiti wa Bunge Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kuahirisha kikao cha Bunge.

Waheshimiwa Wabunge hii ndiyo Taarifa ya Mheshimiwa Spika kuhusu tukio la jana ili Waheshimiwa Wabunge mjue nini kilitokea na nini kilisababisha moshi uliokuwa umetokea. Baada ya matangazo haya tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba msimame naandika majina yenu, kwa hiyo hamna haja ya kuzungumza. Sawa nimeshawaona mkae Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Vicky Kamata Likwelile.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. VICKY P. KAMATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nitaomba Mwongozo kwa Kanuni ya 68(7) sijui unaniruhusu nisome au kwa sababu ya muda niende moja kwa moja?

**NAIBU SPIKA:** Endelea Mheshimiwa.

**MHE. VICKY P. KAMATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mwongozo wangu ni kwenye swali la 49 na majibu ambayo tumepatiwa, nilikuwa naomba mwongozo kuhusu wasanii wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaelewa kwamba Tanzania, hata mimi mwenywe ninaelewa na ninaheshimu kwamba Tanzania ni nchi pekee ambayo inaheshimu maadili na vijana wetu kweli kuna wakati wanazidisha mambo hayo, wanazidisha katika sanaa zao, wanaimba vitu ambavyo pengine kweli wanatoka nje. Lakini naomba mwongozo wako; kwa nini wasanii wafungiwe nyimbo ambayo imeshapigwa mwaka mzima, maudhui yake yameshasambaa kwa watoto mpaka wadogo wanaimba?

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna baraza maalum la kuangalia maudhui ya wimbo kabla haujakwenda hewani, je, baraza hilo linachukuliwa hatua gani kama linaruhusu nyimbo ipigwe, inapigwa mwaka mzima, msanii wa watu ambaye ametengeneza nyimbo yake kwa gharama kubwa bila kusaidiwa chochote anakuja anafungiwa nyimbo kwamba hii nyimbo haina maadili?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema na ninasisitiza tena kwamba ninaheshimu sana maadili na kwa wakati mwingine kweli vijana wetu wanazidisha nyimbo hizo, wanaimba nyingine ambazo zineakwenda nje ya maadili ya nchi yetu lakini je, hii ni njia sahihi ya kufungia nyimbo?

Mheshimiwa Waziri amezungmza hapa kwamba nchi nyingine na ametoa mifano ya nchi mbalimbali ambazo

zimefungiwa, mimi nataka kukataa kidogo kwa sababu nchi nyingine hawafungii nyimbo, isipokuwa wana-*classify* kwamba nyimbo hii ni kwa soko la ndani ikapigwa nyimbo na msanii akanufaika na Serikali ikapata mapato yake lakini nyimbo hii inafaa soko la nje, kwa mfano, Diamond ametutangaza duniani. Akiimba nyimbo ikafungiwa kabisa badala ya kuambiwa kwamba kwa soko la hapa kijana wetu hapana, lakini hii nyimbo itapigwa huko kwingine, kukawa na utaratibu unaoeleweka nadhani ingekuwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba mwongozo wako kwanini tunawanyanyasa wasanii wetu? Tuwaelimishe, tuwasaidie; na hili baraza limechukuliwa hatua gani kwa kuruhusu hizo nyimbo zikapigwa mwaka mzima wakati kazi yao ni kuiangalia, kuisikiliza nyimbo maudhui yake na kuizuia au kuirekebisha kabla haijakwenda kwenye *media?* Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi swali langu Waziri hakunijibu. Swali langu nilikuwa namaanisha Mheshimiwa Vicky alivyouliza.

Je, hii BASATA na Kamati ya Maudhui zinachukuliwa hatua gani, kwa sababu wanaziachia nyimbo za wasanii baadae wanakuja kuzifungia. Mfano, wimbo wa Gigy Money umekaa mwaka mzima wanakuja sasa hivi ndiyo wanauona mpaka watoto wadogo wanatuimbia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba ikiwezekana suala hili tungelijadili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Mbarouk.

**MHE. BAKARI M. MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi nimesimama kwa Kanuni ya 68(7) kwa kuheshimu muda sitaisoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nizungumzie wakati Mheshimiwa Waziri Mwakyembe akimjibu swali namba 49 lililoulizwa na Mheshimiwa Prosper Joseph Mbena, alimnukuu Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere alisema kwamba mwaka 1962, Mwalimu Nyerere alisema; "Taifa ambalo halina utamaduni wake hilo ni Taifa mfu".

Sasa mimi kwa ufahamu wangu ninavyojua wenzetu wa Zanzibar wanalo Vazi la Taifa ambalo ni kanzu nyeupe na koti, lakini sisi huku Tanzania bara mpaka leo bado kuna kizungumkuti cha Vazi la Taifa. Sasa namuuliza Mheshimiwa Mwakyembe, kwa kukosa Vazi la Taifa sisi huku Tanzania siyo Taifa mfu? Naomba anijibu kwa ufasaha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako; wakati Waheshimiwa Wabunge wanazungumzia masuala ambayo yanahusu Idara ya Maji, na walisimama wengi sana kila mtu akitaka kujua hali ya maji na mipango ya Serikali katika Jimbo lake, lakini nafasi hiyo hawakuipata kwa ujumla.

Nilikuwa naomba Mwongozo wako ni kwa nini Bunge lisimuagize Waziri mwenye dhamana atafute taarifa au afanye utafiti wa miradi mbalimbali katika majimbo katika nchi nzima na baadae taarifa hiyo ije hapa Bungeni ili tujue miradi iliyoanzishwa na imekwama ni mingapi, miradi iliyokamilika ni mingapi na wahusika ambao wamesababisha miradi hiyo ikwame na kusababisha shida kubwa ya maji katika Taifa hili wamechukuliwa hatua gani ili tutoe mwongozo rasmi wa Taifa ili Taifa liondokane na kero kubwa ya maji katika majimbo yetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pauline Gekul

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naomba Mwongozo kwa Kanuni ya 68(7) juu ya jambo

ambalo limetokea Bungeni wakati Mheshimiwa Grace Victor Tendega alivyouliza adha ambazo walimu wamekuwa wakizipata Wabunge wengi walisimama, lakini kwa sababu ya wingi wetu na muda hatukuweza kupata nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba Mwongozo wako juu ya matatizo ya walimu katika nchi hii ikiachilia mbali nyumba zao ambazo Serikali imekiri kwamba zaidi ya nyumba laki na elfu arobaini na kitu hazipo. Vilevile walimu hawa wamekuwa wakipata adha hata pale watoto wanapokuwa wamefeli wanashushwa vyeo vyao. Walimu hawa zaidi ya miaka saba hawajapandishwa madaraja lakini hawalipwi *arreas* zao, ni waathirika wa zoezi la uhakiki wa vyeti *fake.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini isikupendeze au isilipendeze Bunge kumtaka Waziri wa Elimu alete maelezo ya kina juu ya lini zoezi hili la uhakiki wa vyeti *fake* litakwisha na walimu wanalipwa lini na wanapandishwa lini madaraja yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ruth Mollel.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuomba Mwongozo wako kwa jambo lilitokea jana na taarifa ambayo umetupa asubuhi hii kuhusu lile tukio la jana la moshi kutokea huku ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sielewi ni kwa nini moshi ulitokea humu ndani na hakuna *smoke detector.* Ningetegemea kwamba kungekuwa na *alarm* za kutushitua sisi huku ndani. Mimi nimeona ni jambo *very serious* jana moshi umetokea hakuna *smoke detectors* na tangu nimekuja kwenye hili Bunge sijawahi kuona tumepewa *fire drill* kama ikitokea moto, tutokeje, twende wapi, kuona kaa mahali ambapo tunakweza kwenda ku-*assemble.* Kwa kweli lile jambo la jana nafikiri ni jambo ambalo tunaomba mwongozo wao liweze kutafakariwa, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, haukuniona huku.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona na mimi nimesimama kwa hisani ya Kanuni ya 68(7) na naomba nisiisome kwa ajili ya muda..

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Mwongozo wako, kwenye ratiba yetu ya leo tunaendelea kuhitimisha mjadala wa Makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 11 *paragraph* ya mwisho na *paragraph* ya kwanza ya ukurasa wa 12 inazungumzia mambo ya Muungano. Kwa hiyo, mambo ya Muungano ni sehemu ya mjadala ambao uko mezani kwako. *(Makofi)*

Mheshimia Naibu Spika, sasa kiti chako jana kilitoa Mwongozo kwamba mamabo ya muungano yasijadiliwe, kwamba kiti kiliahirisha, wewe hukuwa kwenye kiti lakini Mheshimiwa Zungu alikuwa kwenye kiti, aliahirisha kwamba Bunge hili sasa lisijadili mambo ambayo yanahusu muungano kwa muda.

Sasa nilitaka nipate Mwongozo wako, muda ambao mjadala wa Muungano umeahirishwa umekwisha? Kwa sababu kwenye mjadala ambao tutaendelea nao leo Muungano ni sehemu ya mjadala wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pli nilitaka kupata Mwongozo wako kama huu sasa ndiyo utaratibu mpya wa kiti kuchangua eneo gani katika hotuba lijadiliwe na eneo gani lisijadiliwe maana tumezoea katika utaratibu wa kawaida kiti kikiona kama kwenye hotuba kuna eneo ambalo halitakiwi kujadiliwa kiti huwa kinafuta eneo hilo, lakini kwenye hotuba hii kiti hakijawahi kufuta *paragraph* hii ya 11 na ya 12 kwamba ziendelee kujadiliwa lakini kiti kinatukataza tusijadili. *(Makofi)*

Sasa nilikuwa nataka kujua kama huu sasa ndiyo utaratibu mpa wa kuendesha Bunge letu au kitu gani kimejiri lakini tunafidiaje sasa muda ambao watu jana walijiandaa wachangie, hawakupewa hiyo fursa na leo tunakwenda kwenye kuhitimisha, Je, mnawafidiaje Waheshimiwa Wabunge ambao walijipanga kujadili katika eneo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikishukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wangu ni katika swali la 50; Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi katika majibu ambayo ameyatoa kuhusiana na jinsi ambavyo polisi wanachelewesha upelelezi na kusababisha msongamano nimeona swali amelijibu kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule magereza kuna mahabusu wengine ambao wamekaa mahabusu miaka tano mpaka tisa ambao kila siku wanakwenda, wanarudi kwa kisingizio cha kwamba kesi upelelezi bado haujakamilika. Mfano, mwingine ni mimi mwenyewe nimechukuliwa simu yangu sasa hivi ni mwezi wa tatu *cyber crime* wanasema upelelezi haujakamilika, wanashindwa kufungua *IPhone* wanasema ina *passwords* nyingi. Sasa huu ni udhalilishaji na ni suala ambalo linakiuka haki za binadamu kwa sababu simu siyo kwa ajili ya mambo ya kusikiliza tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilitaka Mwongozo wako; kama sisi wawakilishi ambapo muuliza swali anataka ajue hatma ya hawa watu ambao wananyanyaswa, wanakaa mahabusu muda mrefu na polisi kwa kisingizio kwamba upelelezi haujakamilika ni lini sasa Serikali itatoa agizo kwamba upelelezi uwe unakamilika baada ya muda fulani kwa sababu kwa kweli watu wananyanyaswa na haki zao zinanyanyaswa kwa kukaa muda mrefu mahabusu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bungara.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 68(7), na kwa kuwa wewe ni Mwanasheria mbobezi na kwa kuwa muda uliopita Mheshimiwa mbobezi Mheshimiwa Mwakyembe alisema Bunge letu lina wajibu wa kulinda na kuzitetea sheria zilizotungwa katika Bunge hili, kwa hiyo mimi nataka Mwongozo wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, iiwa kweli Bunge lina kazi hiyo aliyosema mwanasheria mbobezi Mheshimiwa Mwakyembe, na Katiba ya Jamhuri ya Muungano na sheria za nchi hii zimeruhusu mikutano ya hadhara na maandamano, lakini Serikali imezuia mikutano ya hadhara na maandamano katika vyama vya siasa. Kwa kuwa wewe ni mwanasheria mbobezi na mwanasheria Mwakyembe ni mbobezi na Bunge kazi yake kuisimamia Serikali.

Naomba mwongozo wako kwa kauli hii ya Serikali ya kusema mikutano ya hadhara isifanyike na maandamano naomba mwongozo Bunge linasema nini kuhusu jambo hili. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Umenisahau.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Naibu Spika, umenisahau huku.

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae Mheshimiwa Jaku.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa miongozo kadhaa hapa na Waheshimiwa Wabunge kwenye mambo mbalimbali, yako mambo ambayo ni kweli yanahitaji mwongozo wa kiti na yako mambo ambayo kimsingi ni maswali na kwa hivyo yanatakiwa kuja kama maswali ili Serikali ipate fursa ya kujibu.

Waheshimiwa Wabunge hii Kanuni kwa sababu tumeshaisoma mara nyingi lakini kwa namna miongozo

ilivyoletwa hapa inanilazimu kuisoma tena ili Waheshimiwa Wabunge tujue ni wakati gani wa kuomba mwongozo, ni wakati gani wa kuleta hoja yako na ni wakati gani wa kuleta maelezo binafsi.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 68(7) inasema hivi; "Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambao hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba "Mwongozo wa Spika" kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye, kadri atakavyoona inafaa."

Waheshimiwa Wabunge, maswali mengi mnayouliza wakati wa mwongozo hayaulizi kama jambo fulani linaruhisiwa ama haliruhusiwi. Ili Mheshimiwa Mbunge ujue Mwongozo unaoomba uko kikanuni lazima wewe mwenyewe ujiulize ama mwishoni mwa huo mwongozo wako useme hivi unataka kujua kiti kinipe Mwongozo je, jambo hili linaruhusiwa ama haliruhusiwi. Ikiwa swali lako ama suala lako haliwezi kumalizwa na linaruhusiwa ama haliruhusiwi ujue huo si Mwongozo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusoma Kanuni hii naanza na mwongozo wa kwanza nilioombwa na Mhesimiwa Vicky Kamata Likwelile ambaye ameomba kwa maelezo marefu ambayo wote tulimsikia akieleza kuhusu majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri kuhusu wasanii wetu na kwamba kama nchi ni lazima kuheshimu maadili na kwamba na yeye anakubaliana na hilo. Lakini akauliza kwamba, kwa nini wafungiwe baada ya mwaka mzima, lakini pia akasema ni hatua gani Baraza linachukuliwa. Katika hatua hii nitajibu miongozo yote miwili, wa Mheshimiwa Catherine Magige na pia Mheshimiwa Vicky Kamata.

Waheshimiwa Wabunge, miongozo hii ya kuhusu hatua gani zinachukuliwa dhidi ya Baraza kwa kuruhusu muziki upigwe mwaka mmoja ama hata zaidi halafu uje ufungiwe baadae haya ni maswali ambayo Serikali inapaswa kujibu

kama imechukua hatua yoyote ama haijachukua hatua yoyote. Kwa hivyo kiti hakiwezi kutoa Mwongozo kwenye jambo kama hili ama kwenye maelezo kama haya kwa sababu hayalengi kusema jambo hili je, linaruhusiwa ama aliruhusiwi kikanuni. Kwa hiyo jambo lolote ambalo liko nje ya utaratibu wa maamuzi yetu ya kikanuni haliwezi kutolewa mwongozo na kiti. *(Makofi)*

Kwa hivyo Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Vick Kamata na Mheshimiwa Catherine Maige mimi niwashauri kupeleka maswali kwenye kitengo chetu cha Bunge ili Serikali iapate fursa ya kujibu wamechukua hatua gani dhidi ya baraza ama kama kuna hatua zozote ambazo zimewekwa kisheria kwamba baraza lisipofanya kazi yake linapwaswa kuchukuliwa hatua gani.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa pia Mwongozo na Mheshimiwa Musa Mbaruku ambaye ameeleza kwamba katika majibu ya Mheshimiwa Waziri Mwakyembe, akiwa anamnukuu Baba wa Taifa kwamba Taifa lisilokuwa na utamaduni ni mfu. Yeye ameuliza kwamba upande wa Zanzibar wana Vazi la Taifa na upande wa Bara hakuna Vazi la Taifa sasa anauliza je, kwa upande wa Tanzania Bara kwamba ni mfuu ama si mfu.

Majibu ya Mwongozo huu Waheshimiwa Wabunge yanalingana na miongozo iliyopita niliyoisema, hiyo miwili. Hili ni swali ambalo Mheshmiwa Mbaruku unapaswa kuiliza Serikali ikujibu na si kiti, kwa sababu sisi kwenye Kanuni zetu za Bunge hatushughuliki na haya mambo ya mavazi ya Taifa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Waabunge nimeombwa Mwongozo pia na Mheshimiwa Waitara kuhusu swali ambalo limejibiwa na Wizara ya Maji, kwa maana ya kwamba Wabunge wengi walisimama wakitaka kuuliza mambo ama matatizo ama adha wanazozipata wananchi katika majimbo yao kuhusu miradi mbalimbali ya maji; ambayo mingine haifanyi kazi mingine inafanya kazi.

Mheshimiwa Waitara naye ameuliza swali akisema kwa nini Bunge limuagize Waziri wa maji alete taarifa na taarifa yake iwe na miradi ambayo inafanya kazi vizuri lakini pia miradi ambayo imekwama na hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa katika maeneo yote mawili. Kwa maana ya kwamba miradi iliyokwama watu wale ambao wamekwamisha wanachukuliwa hatua gani ama viongozi kama ndio wanaohusika hapo.

Kwa hiyo, hili nalo Mheshimiwa Waitara kwa sababu si suala la kama jambo linaruhusiwa ama haliruhusiwi na lenyewe ulipeleke kama swali ili Serikali ipate fursa ya kujibu, kwa sababu hakuna jambo ambalo hapa haliruhusiwi wala ambalo linaruhusiwa katika Mwongozo wako.

Nimeombwa pia Mwongozo na Mheshimiwa Pauline Gekul ambaye ameelekeza Mwongozo wake kwenye swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, kwamba swali lake lililenga hasa kuelezea matatizo ambayo walimu wanakumbana nayo, na ametoa maelezo hapa kwamba wakati mwingine hata walimu wameshushwa vyeo wanafunzi wanapofeli. Akaeleza kuna walimu ambao wamekaa miaka mingi wengine hata kufikia saba bila kupandishwa vyeo na akasema wengine ni waathirika wa vyeti *fake.*

Mheshimiwa Gekul ametoa mawazo yake kwamba kwa nini bune lisiitake Wizara ya Elimu kuleta taarifa juu ya mambo haya ili walimu waondokane na adha zinazowapata. Mheshimiwa Gekul hili nalo kwa kuwa si suala la kuruhusiwa ama kutoruhusiwa humu Bungeni ushauri ni kama huo aliopewa Mheshimiwa Mollel upeleke swali la msingi ili Serikali ipate nafasi ya kuzungumza kwenye mambo hayo.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa pia Mwongozo na Mheshimiwa Ruth Molle ambaye amezungumzia jambo ambalo limetokea jana lakini ni kutokana na taarifa amabyo imesomwa hapa ya Mheshimiwa Spika. Akauliza kwa nini moshi ulivyotokea jana

humu ndani hatukusikia mlio wowote wa kuashiria kwamba jengo letu hili ama humu ndani kuna namna ya kujua kwamba kuna moshi ama kiashiria cha moto mahali.

Pia amesema humu ndani hatujawahi kupewa fursa ya kuelekezwa ama kuelekezwa kwa vitendo yeye ametumia kiingereza *fire drill* kwamba kama moto ukitokea ama janga lolote likitokea humu ndani watu tutafanya nini tutajiokoa vipi. Pia ameeleza ni wapi mahali pa kukutana kama ukitokea moto humu ndani ama likitokea jambo ambalo linatutaka tutoke kwa dharura ni mahali gani pa kutokea.

Waheshimiwa Wabunge, jambo hili la Mheshimiwa Ruth halitatolewa Mwongozo lakini maelezo yake ni kwamba ni jambo la msingi na sisi tumelichukua, ila si jambo linalopaswa kuombewa Mwongozo. *(Makofi)*

Kwa hiyo Mheshimiwa Ruth maelezo uliyoyatoa na hivi vitu vyote ni jambo la kuangalia, nadhani *fire detectors* zipo lakini sasa kama hazifanyi kazi maana yake kuna tatizo kwa hiyo, ofisi inalichukua na kama zimeisha wakati ni suala la kubadilisha. *(Makofi)*

Hili jambo lingine la kusema humu ndani tufaniwe hayo maarifa ya kujua wapi pa kukimbilia na namna gani tutatoka pia ni jambo la msingi sana kwa sababu jana watu wengi walielekea mlango ule lakini pembeni huku kuna milango ambayo wangeweza kutokea. Kwa hiyo tutajikuta wote tuko kwenye mlango mmoja wakati Wabunge wengine wangeweza kupita milango mingine ya dharura. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hili nalo Mheshimiwa Ruth Mollel litafanyiwa kazi na ofisi itakapokuwa tayari itafanya jambo hili, na mimi naamini kwamba itafanywa mapema ikiwa ni pamoja na kuwaelekeza Waheshimiwa Wabunge wapi mahali pa kwenda kusimama kwa sababu inapotokea jambo kama hili watu huwa inabidi wahesabiwe. Kwa hiyo, hilo nalo litafanya Mheshimiwa Ruth Mollel tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nimeombwa pia Mwongozo na Mheshimiwa Mtolea akieleza kuhusu utaratibu wetu ambao tunao leo kwenye *Order Paper* kwamba mjadala unaendelea na kwamba jana Mheshimiwa Zungu alielekeza kwamba mjadala kuhusu Muungano alikuwa anauahirisha kwa muda ili aweze kutoa mwongozo aliokuwa ameombwa na Mheshimiwa Jenista.

Mheshimiwa Mtolea anasema anataka kujua kama huu ndio utaratibu wa Kiti kuchagua eneo fulani la kujadiliwa na kukataza pengine eneo fulani kujadiliwa wakati halijaondolewa kwenye mjadala ama kwenye hiyo taarifa mahsusi inayojadiliwa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa wale ambao walikuwepo jana nadhani walimsikia Mheshimiwa Zungu vizuri, na kwa namna ambavyo mjadala ulikuwa ukienda humu ndani na Mwongozo uliombwa na Mheshimiwa Jenista, nadhani wote hii kanuni sina haja ya kuirudia tena, Mheshimiwa Zungu alisema mpaka atakapotoa Mwongozo. Kwa kuwa alisema mpaka atakapotoa Mwongozo, na kanuni zetu zinaruhusu Mwongozo kutolewa kutolewa papo hapo ama Mwongozo kutolewa baadaye basi utartibu ambao Mheshimiwa Zungu aliuchukua huko kikanuni kabisa na hakuna haja ya kutolea maelezo tofauti na hayo ambayo alikuwa ameyatoa yeye alipokuwa hapa.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa Mwongozo pia na Mheshimiwa Msigwa kuhusu majibu yaliyotolewa kwenye swali namba 50 kuhusu kuchelewesha upelelezi. Mheshimiwa Msigwa anasema jambo hili limejibiwa kisiasa, na kwa sababu yeye alipokuwa mahabusu alijifunza kwamba wako watu wamekaa miaka wengine zaidi ya sita wengine amesema mpaka tisa wakiwa wanapelekwa mahakamani na kurejeshwa mahabusu kwamba kesi zinasubiri upelelezi.

Mheshimiwa Msigwa amemalizia maombi yake ya Mwongozo kwamba Wabunge kama wawakilishi wa watu ni hatua gani zinaweza kuchukuliwa ili watu wasiendelee kunyanyaswa ama watuhumiwa wasiendelee kunyanyaswa

na kukaa muda mrefu kama alivyotoa maelezo yake marefu. Waheshimiwa Wabunge jambo hili halina tofauti na miongozo niliyotoa hapo mwanzo. Kiti kinaulizwa ikiwa jambo linaruhusiwa ama haliruhusiwi chini ya Mwongozo, kwa hiyo hana maelezo tofauti na hayo nilitoa mwanzo. Hivyo Mheshimiwa Msigwa kwenye huu Mwongozo wako Serikali ili ipatae nafasi ya kueleza jambo hili wewe ulipeleke kama swali Serikali itapaswa kujibu kwenye mambo haya ambayo umeeleza kwa kirefu kwamba wananchi wananyanyaswa kwa kukaa muda mrefu mahabusu.

Mwongozo mwingine niliyoombwa na ni wa mwisho nimeombwa na Mheshimiwa Bungara, na yeye anaeleza kuhusu maelezo aliyokuwa ameyatoa Mheshimiwa Waziri Mwakyembe kwamba Mheshimiwa amesema hatuwezi Bungeni tukawa tunajiuliza kuhusu sheria zetu wenyewe, lakini tunapaswa kuzitetea kwa sababu sisi ndio tuliotunga.

Mheshimiwa Bungara ameeleza kwamba mambo mengi yapo kwenye sheria lakini hayafuatwi na mifano yake ni kukataza kwa mikutano ya hadhara ambayo imeruhusiwa kisheria, lakini pia maandamano ambayo yameruhusiwa kisheria.

Mheshimiwa Bungara amemalizia maombi yake ya Mwongozo kwa kusema Bunge linasemaje.

Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo unatolewa kikanuni kwa maana ya kwamba unataka kujua ikiwa jambo liliotokea linaruhusiwa ama haliruhusiwi. Mheshimiwa Bungara naye anaruhusiwa kupeleka swali la msingi ili Serikali ipate nafasi ya kutoa majibu. Waheshimiwa Wabunge baada ya kuyasema hayo tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jaku naomba ukae kwa sababu wewe huwezi kunipa mimi taarifa, kwa hiyo, naomba ukae kwa sababu mimi ndiye niliyekuwa nazungumza.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilisimama mimi kiti chako hakinifanyii haki. Tangu jana nasimama na leo nasimama, kama nanyimwa haki yangu ya msingi hewala.

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae Mheshimiwa Jaku. Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na uchangiaji katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Tizeba alikuwa ameitwa jana wakati lilipotokea lile tatizo, kwa hiyo tutaanza na Mheshimiwa Tizeba dakika 10 atafuatiwa na Mheshimiwa Kange Alphaxard Lugola dakika tano na Mheshimiwa Mwijage ajiandae.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa kuanza kabisa niseme naunga mkono haja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuunga mkono hoja naomba kwa haraka nitoe ufafanuzi wa baadhi ya michango ya Waheshimiwa Wabunge ambayo inagusa sekta ya kilimo na kwa muktadha huo nitazungumzia korosho, kahawa, pamba, ufuta, mfumo wa uingizaji wa mbolea kwa pamoja na soko la nafaka kama muda utakuwa unatosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kwanza jambo la korosho katika namna mbili, moja ni kwa namna gani tumejipanga kuhakikisha kwamba kiatilifu aina ya *surphur* kinapatikana kwa wakulima wa korosho nchini. Mpaka hivi

sasa ninapozungumza Serikali imekwishatoa shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kulipia *advance* ya *suppliers* wa *sulphur* kwa maeneo yanayozalisha korosho. Fedha hizi imelipwa Kampuni ya Mbolea ya Taifa *(TFC)* ambao wao wataingiza tani 8,000; na sasa hivi wanayo *order* ya tani 5,000 ambayo itafika mapema mwishoni mwa mwezi huu au mwanzoni mwa mwezi ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambasamba na *TFC* Kampuni ya Bajuta pia imeshapewa zabuni ya kuingiza hiyo sulpha tani 10,000 na wataingiza tani 5,000 mwishoni mwa mwezi huu, tani 5,000 zingine zitaingizwa na kampuni ya dunia mwanzoni mwa mwezi wa tano au katikati ya mwezi wa tano. Kwa hivyo mpaka kufiia tarehe 15 Mei tuna uhakika tutakuwa na tani zisizopungua 15,000 ambazo hizi tutazitumia kwa maeneo ya Lindi ambako ndiko mwanzo kabisa wa upuliziaji unatakiwa kuwapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nitoe taarifa tu kwamba ziko tani 4,000 sasa hivi nchini zilizomilikiwa na kampuni ya *Expo Trading* na tunafanya mazungumzo nao kuhusu bei ili tukikubaliana bei nayo ianze kugaiwa kwa wakulima hasa katika yale maeneo ambayo yanahitaji dawa hiyo haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Serikali kupitia vyama vya ushirika itaagiza jumla ya tani 35,000 ya *sulphur* mwaka huu, na tuna hakika kiasi hicho cha *sulphur* kitawatosha wakulima kwa nini tunajiingiza kuagiza hizi *sulphur* sasa hivi, hii yote ni kutaka kudhibiti bei ya *sulphur* ili wakulima waweze kupata nafuu wanapokuwa wananunua dawa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la muhimu hapa nitoe tu taarifa kwamba *sulphur* mwaka huu kwa wakulima itauzwa na itauzwa kwa bei itakayokuwa *controlled* na Serikali, na ndio maana tunashiriki katika uagizaji wake ili tuje tuhakikishe kwamba bei itakayouzwa hii *sulphur* itakuwa inahimilika kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kwa wananchi waliouza korosho zao msimu uliopita na sasa hivi hawajalipwa. Moja ya sababu ya wananchi hawa kutolipwa ni mkanganyiko uliotokea baada ya kuwashawishi wafungue akaunti ili malipo yafanyike moja kwa moja benki. Wengine badala ya kufungua wao akaunti waliwabebesha ndugu na marafiki zao na hivyo wale walioingiziwa pesa kwenye akaunti zao kugoma kuwalipa wakulima hawa. Lakini lilitokea tatizo la Benki ya *Covenant* kufungwa ambayo vyama 14 vya msingi vilikuwa vinapitishia pesa katika benki ile. Sasa jambo hili ni la kisheria kwa hivyo suala la Benki Kuu na ile benki linaendelea kufanyiwa kazi na litakapokuwa limetatuliwa wakulima hawa watapewa fedha zao na wala hazitapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kwa haraka suala la masoko na namna ya kuuza kahawa na pamba kwa msimu wa mwaka huu. Serikali imeamua kusimamia ushirika wa nchi hii ili wakulima waweze kunufaika. Utaratibu uliokuwepo wa kuuza kahawa umekuwa hauna manufaa kwa wakulima walio wengi, lakini umewanufaisha zaidi watu wa katikati yaani watu wanaonunua na kuuza na si wakulima wenyewe. Neno linaitwa butura kwa watu wa Ziwa Magharibi wanafahamu maana yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwananchi analima kahawa, anapatwa na tatizo kidogo la shilingi 200,000; mtu mwenye pesa anakuja anampa shilingi 200,000 halafu anamuandikisha mkataba wa shilingi milioni tano na kusema hizo milioni tano wasipozilipa mpaka mwezi wa sita nyumba yake inauzwa; na kwa vile mwananchi huyu anakuwa na shida analazimika kuchukua hizo pesa kwa masharti ya kihalifu namna ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Serikali imeona namna bora ya kuwasimamia wananchi hawa maskini kuwa ni kusababisha wauze kahawa yao kupitia mfumo rasmi mfumo wa ushirika. Kwa namna hii na nimesikiliza sana maoni ya Waheshimiwa Wabunge kwamba tutengeneze utaratibu ambao watau wenye shida kama hao katikati ya ushirika huo waweze kupata msaada. Ni kweli, Mbinga utaratibu huu

unafanyika vizuri, vyama vya wakulima vya Mbinga vinao utaratibu ambao mwananchi akiwa na shida wanao mfumo wa kumsaidia na kwa hivyo tunapeleka huo uzoefu wa Mbinga katika maeneo mengine ili wananchi wa kule wasilazimike kuingia kwenye utaratibu ule usiokuwa na manufaa kwao isipokuwa wapitie ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko jambo la wauzaji wa kahawa moja kwa moja nchi za nje yaani *direct export.* Wauzaji wa namna hii sio wengi, kimsingi ni wale wenye mashamba makubwa ambayo ni kama asilimia 10 au tisa ya uzalishaji mzima hapa nchini. Sasa watu wa namna hii wamekuwa wanauza moja kwa moja na katika kuuza moja kwa moja hatupati takwimu sahihi za mauzo yao. Hawa pia ndio wamekuwa wanafanya hiyo kitu inaitwa butura, wananunua kwa wakulima, wana-*aggregate* halafu wanauza nje moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema kahawa hata kama imethibitishwa *(satisfied)* kwa ubora fulani ipeleke mnadani ili wanunuzi wengine pia wakaijue. Tunapofanya hivi tunazuia *price transfer* kwa sababu uuzaji wa moja kwa moja ambao hauwezi kudhibitiwa na bodi unakuwa unatoa mwanya mtu kutengeneza bei ya chini kwa *sister company* ili alipe kodi isiyostahili halafu fedha inayobaki anakwenda kukutana nayo huko nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko jambo la utayari wa ushirika kusimamia mfumo huu, tunalifanyia kazi, vyama vya ushirika vyenye matatizo tumesha vibaini na tunazungumza na mabenki kuona namna ambavyo navyo vinaweza vikapata fedha kwa ajili ya kulipa *advance* ambayo wamekuwa wanawalipa wakulima wao miaka yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kule *KCU* juzi ilisemekana *KCU* wametangaza bei ya shilingi 1,000 kwa kilo moja ya kahawa. Naomba nitoe taarifa rasmi kwamba jambo hilo sio kweli, wao walikuwa wanafanya bajeti ya chama chao cha msingi kwamba wachukue kiasi gani benki kwa ajili ya kuwa-*advance* wakulima kabla ya kupeleka

kahawa ile mnadani na kamwe ile si bei ya kahawa ambayo wanatakuwa wananunua kutoka kwa wakulima wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamba pia tutauza kwa utaratibu huu huu, na tutapita na tunaendelea kupita maeneo yote ya pamba kujiridhisha kwamba vyama vya msingi vya wakulima wa pamba vipo *in place* na kama havipo basi uchaguzi ufanyike. Angalizo letu ni kwmaba wananchi wachague viongozi waadilifu wasije wakatumia kuchaguliwa kwao kwenda kuwaibia wananchi kama walivyozoea miaka ya nyuma. Nitahadharishe wale wanaogombea uongozi wa vyama hivi vya wakulima kwa lengo la kwenda kuuza wako mwili wao nusu uko jela, nusu uko bado mtaani kwa sababu hatutakuwa na huruma na mtu yeyote atakayejaribu kuiba mali ya wananchi kwa kisingizio chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la mfumo wa uingizaji wa pembejeo nchini. Katika hili tutafanya seminar ya Bunge zima kuelezea mfumo huu unafanyaje kazi.

Naomba Waheshimiwa Wabunge muwe na subira tutawapitisha katika mfumo huu ili uelewa uwe wa pamoja na tuko tayari kusikiliza maoni yenu pale mnapoona kwamba jambo hili haliendi salama.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Mwijage.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye hoja muhimu na mahsusi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kwanza kabisa naunga mkono hoja hii. Ni hoja ambayo imesheheni mambo ya msingi kwa Watanzania na

hivyo ninashangaa sana watu ambao wanabeza juhudi ambazo Mheshimiwa waziri Mkuu anazifanya. Hilo ni kusema tu kwamba washindwe na walegee.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mambo mawili yanayohusu masuala ya mazingira. Kuna mambo mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyazungumzia yanayohusu uharibifu wa vyanzo vya maji, uchafuzi wa mazingira kwenye vyanzo vya maji likiwemo suala la ukataji miti hovyo na suala la mkaa. Nataka niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge jambo moja ambalo wanadamu huwa tunajisahau. Mwanadamu anapomuona mwenzake anakufa hakumbuki kwamba na yeye ni marehemu mtarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanadamu anapomuona mwenzake ni mlemavu hakumbuki kwamba na yeye ni mlemavu mtarajiwa. Vivyo hivyo, wako Waheshimiwa Wabunge ambao wanadhani kwamba mazingira yanahusu tu wanyama watatoweka, miti itatoweka, ndege watatoweka, wanasahau kwamba hata sisi wanadamu vilevile tutatoweka endapo hatutalinda na kuhifadhi mazingira ya nchi yetu. Kwa hiyo, na sisi wanadamu ni watoweka watarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria yetu ya mazingira inazungumzia namna ambavyo tunatakiwa kutoa miongozo kwa Halmashauri zote nchini pamoja na wadau wengine wa mazingira kuhakikisha wanaorodhesha vyanzo vyote vya maji pamoja na milima na vilima wakionesha changamoto za vyanzo vya maji kwenye maeneo yao pamoja na milima na vilima.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongozo hii inatuhitaji sisi baada ya kupata orodha hizo tuweze kuona changamoto za kila vyanzo vya maji ili vyanzo hivi tuweze kuvitengenezea miongozo ya kuvilinda ikiwa ni pamoja na kuvitangaza kwenye Gazeti la Serikali. Sasa kuna baadhi ya Wakurugenzi katiaka nchi hii ambao tangu Ofisi ya Makamu wa Rais imetoa agizo hili la kuwasilisha orodha hizi, muda ulishapita

na juzi nikiwa Morogoro nimetoa muda mwingine wa mwisho kwamba tarehe 20 Aprili, 2018 Wakurugenzi wote nchi nzima wawe wamewasilisha Ofisi ya Makamu wa Rais orodha za vyanzo vya maji kwenye maeneo yao, vilima pamoja na milima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakurugenzi ambao wataendelea kukaidi agizo hili na kutolitekeleza, Mheshimiwa Waziri Mkuu najua mamlaka ya uteuzi Mheshimiwa Rais, kazi yetu sisi Ofisi ya Makamu wa Rais tutaorodhesha Wakurugenzi wote katika nchi nzima ambao wamekataa kutekeleza agizo hili ili mamlaka ya uteuzi itafakari na kuona kama vitumbua vya Wakurugenzi hawa vinastahili kutiwa mchanga ama laa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vya maji vina uhusiano mkubwa sana na ndoto yetu ya Tanzania ya viwanda. Vyanzo vya maji vina uhusiano mkubwa na suala la uzalishaji wa umeme. Niwape mfano mdogo Waheshimiwa Wabunge, Mtera inazalisha megawati 80, Kihansi inazalisha megawati 180, Kidatu inazalisha megawati 204 na vyote hivyo vinahitaji sisi tulinde na kuhifadhi vyanzo vya maji na hasa maeneo ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawataka Watanzania ambao wanalima kwenye bonde hilo wazingatie masharti ya kulima kilimo cha uhifadhi *(conservation agriculture)* na wasijihusishe na uharibifu wa Bonde la Mto Ruaha Mkuu. Hata wake rafiki zangu akina Mheshimiwa Mwamoto, akina Mheshimiwa Chumi, Mheshimiwa Ritta Kabati ambao wana kilimo maarufu kinaitwa vinyungu, kilimo hiki cha vinyungu lazima kiende sambamba na kuhifadhi mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala lililojitokeza la shule ama vyuo ama taasisi ambazo zinatoa mafunzo kutokuwa na matundu ya vyoo na hivyo kusababisha ama wanafunzi, ama wafanyakazi kujisaidia porini na hivyo kuchafua mazingira; pamoja na kwamba kuna baadhi ya shule ambazo hazina matundu ya vyoo lakini hata shule ambazo zina matundu ya vyoo vikiwemo na vyuo vya kati na vyuo vikuu wana tabia ya kutapisha vyoo na kupeleka

kwenye mifumo ya mito ambayo wananchi wanatumia kwa kumwagilia mbogamboga pamoja na matunda. Nimeenda Dar es Salaam pale, kuna vyuo pale ambavyo vinatiririsha maji kwenda Makuburi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Malizia sekunde 30 Mheshimiwa Kangi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo natoa tahadhari, shule zote ambazo nimefanya ukaguzi na kuwaambia watoe mabomba yanayotiririsha kwenye vyanzo vya maji wayaelekeze *DAWASCO,* na tutafanya ukaguzi nchi nzima. Yale mabasi ambayo bado hawataki kutekeleza agizo la Mheshimiwa Mwakyembe la kuchimba dawa, tutaanza kuorodhesha kutumia maafisa mazingira wa wilaya mabasi ambayo wanachimba dawa porini na kuchafua mazingira ili na wao tuwapige faini kama wale wengine. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kangi Lugola. Mheshimiwa Mwijage dakika kumi atafuatiwa na Mheshimiwa Mpina, dakika saba.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nitachangia kwa kujaribu kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wenzangu walio katika Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii ambayo kimsingi ni Wizara ya uratibu. Sisi ili tuweze kufanya kazi zetu tunawategemea sana, ahsanteni kwa msaada mnaotupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengi yaliyozungumzwa, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge, yananijengea uwezo wa kuwaletea hotuba nzuri ambayo italenga kujibu matakwa yenu. Hata hivyo kuna mambo ambayo ningeomba niyajibu leo kusudi niweze kuchangia vizuri Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la msingi la kwanza ni suala la viwanda. Kuna kutoelewa au tuna kuelewa tofauti juu ya suala la viwanda. Ukisoma Mpango wa Pili wa Miaka Mitano tumeamua kujenga uchumi wa viwanda na dhima yetu ni ujenzi wa uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu. Mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu ndiyo *center.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalenga ifikapo mwaka 2025 hii iwe nchi ya uchumi wa kati kwa kupitia uchumi wa viwanda. Sasa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote ili tujenge uchumi wa viwanda kwa mtu ambaye alikuwa hajui viwanda lazima kulingana na matabaka yetu na uwezo wetu twende kwenye makundi manne ya viwanda. Mimi kiwanda ninachokiita kidogo mwenzangu atakiita kikubwa ndiyo maana tunahimiza falsafa ya viwanda vidogo sana, viwanda vidogo, viwanda vya kati na viwanda vikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwatie shime Watanzania na tuwaangalie waliotutangulia. Nchi ya India ambayo yenyewe ina *population* ya bilioni 1.256 lakini ina *income per capita* ya dola 1,800 unaweza kuzidisha ukapata *GDP* yake. Asilimia 38 yake inatokana na viwanda vidogo. Bidhaa unazozikuta madukani India asilimia 40 inatokana na viwanda vidogo, lakini mauzo ya India nje asilimia 45 inatokana na viwanda vidogo. Sasa ukisoma andiko la Mchungaji Profesa Adam Persia anakueleza kwa nini viwanda vidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vidogo hasa kwetu Watanzania ni shule, kama hujawahi kumiliki kiwanda, usianze na kiwanda cha bilioni mia tano, anza na kiwanda kidogo. Kiwanda kidogo kinakufaa wewe muanzishaji, lakini

ni shule una-*train family,* ndiyo maana; napenda niliseme hili; ndiyo maana unakuta *family* za wenzetu kama Madhvani mimi nimezaliwa nasikia Madhvani mikaa 65 iliyopita Madhvani alikuwepo Uganda, lakini Madhvani mpaka leo yupo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana mkagundua sisi Wabunge, Watanzania wote kwa nini tunasoma na watoto wa Wahindi mashuleni lakini hatuombi kazi pamoja na wao? Ni kwa sababu wanakuwa *trained* kwenye *family business* na wanaweza kuendelea miaka mingi na mingi. Kwa hiyo nawasihi muwe mashuhuda, *campaigner,* mhimize Watanzania wakubali suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapozungumza suala hilo tunakwenda kwenye jibu la viwanda, tuna viwanda vingapi? Nina rafiki yangu mmoja Mbunge wa Monduli anasema viko wapi? Hivyo viwanda 3,306 vipo na viko Tanzania. Nimekwenda kutafuta takwimu za viwanda vile, viwanda tulivyonavyo Tanzania ni zaidi ya viwanda 53,000, vimechapwa kwenye karatasi za A4 karatasi 900. Kwa hiyo vipo, vipo Tanzania na ukiviangalia kila kijiji kina kiwanda kimeorodheshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivyo viwanda vinafanya kazi gani? Tumeelekezwa kwamba tuanzishe viwanda ambavyo vitachakata mazao ya shamba, mazao tunayoyalima sisi. Faida ya viwanda hivi hata kama ni vidogo vinaongeza *life span* ya *product* na vinapunguza *post-harvest loss,* ndiyo maana ya kuhimiza hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwape mfano mmoja tulionao sasa hivi wa watu wa Dodoma. Dodoma wana zabibu, sasa hivi zabibu inapata tatizo la soko kwa sababu ya mambo fulani ambayo tunayarekebisha, lakini mtu mwenye kiwanda kidogo cha shilingi 500,000 au 600,000 unaweza kuchukua zabibu ukasaga, unapata mchuzi unauweka kwenye gudulia ambapo unasubiri wakati soko likipatikana unaweza kuuza. Mheshimiwa rafiki yangu ambaye ni mkulima wa zabibu anaelewa kitu hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasihi toka hapa kabla ya andiko langu halijaja muweze kuhubiri viwanda vidogo. Niwaahidi, nimeandika kitabu kuhusu viwanda vidogo nitakitoa kabla ya bajeti yangu, lakini na bajeti inayokuja ni kitabu cha rejea. Kama hujui viwanda ukisoma bajeti yangu nitakayoiandika utaweza kuelewa suala la viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie mazingira ya biashara. Wengi wamezungumzia mazingira ya biashara. Mimi narudia kauli ya viongozi wangu; Mheshimiwa Rais amelizungumzia, Mheshimiwa Makamu wa Rais amelizungumzia, Mheshimiwa Waziri Mkuu amelizungumzia suala la mazingira ya biashara. Zaidi tumeandika andiko *(regulatory reform)* ambayo inaitwa almaarufu *blue print;* tunataka hivi vikwazo viondoke. Hata hivyo ukisoma maandiko hii kazi haikuanza leo. Mpango wa kwanza wa miaka mitano ilikuwa kuondoa vikazo, haikumalizika, tumekwenda nayo na hivi vikwazo vitaondoka na nyingine tusilaumiane ni *mind-set.* Kuna mtu ukiingia ofisini amezoea kuwanunia watu sasa hilo sio tatizo la Waziri wake au Katibu Mkuu wake ndivyo alivyo na tutawabadilisha hao watu waweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la viwanda limezungumziwa suala la matrekta ya URSUS au matrekta yaliyoko *TAMCO* almaarufu kama alivyokuwa akiyaita ndugu yangu Dkt. Mwigulu Nchemba kwamba ni matrekta ambayo yana lengo la kuondoa jembe shambani kulibakiza kwenye ile bendera ya chama anachokipenda na makaburini kusawazisha makaburi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge kwa nini matrekta ya URSUS hayajauzwa, yana maelekezo maalum, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameelekeza yale matrekta yaende kijijini sasa huyo mtu wa kijijini unampaje? Tunatengeneza utaratibu tukishirikiana na Hazina kwamba Wabunge mpewe, wafanyakazi mpewe na ma-*DC* wapewe yaende vijijini si matrektra ya kuvuta mizigo. Watu walileta matrekta unayakuta *airport,* au unayakuta bandarini, haya yanakwenda vijijini. Tuna matrekta 2,400 kwa hiyo

Waheshimiwa Wabunge, yakija myagombanie kama mpira wa kona myapeleke vijijini, halafu mtaona mwaka 2020 mambo yatakavyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie miradi ya kimkakati. Miradi ya kimkakati inatekelezwa, mnaweza mkawa mnaona ucheleweshо, wengine mnasema twende haraka, lakini sheria tuliyoitunga sisi Wabunge mwaka jana ya kuangalia maslahi ya Taifa imetufanya ile mikataba kwa mfano ya Mchuchuma na Liganga iangaliwe mara tatu au nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaeleze, mimi nilikuwepo; nilimsikia Rais wa Zambia na wengi mmeona *clip* za Zambia na kuna nchi nyingine wanalia, waliingia mikataba unakuta kila kitu kimechukuliwa. Naogopa na namkumbuka kaka yangu ambaye alikuwa Waziri hapa. Aliwahi kusema mtafanya maamuzi, maamuzi hayo hata kama mmekufa makaburi yenu yatafungwa minyororo ndivyo alivyosema Sebastian Rweikiza Kinyondo. Nisingependa mimi kaburi langu lifungwe mnyororo.

Kwa hiyo, hii miradi ya kimkakati tusingependa kufanya maamuzi, kwa hiyo tunaipitia na tunapoipitia tunazungumza na ninyi mje mtuhoji mtuelekeze.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuwapongeza Wabunge ambao wametupa *information where we are getting wrong,* lakini kama nilivyowaahidi nitazungumza nanyi zaidi katika bajeti yangu ambayo nimeahidi kitakuwa kitabu cha rejea. Ahsanteni sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mpina, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Isaack Kamwelwe. Mheshimiwa Profesa Mbarawa ajiandae.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi uliyonipa na wa kweli ni dakika saba muda mfupi. Niseme tu kwamba maelezo zaidi

ya kina yatapatikana wakati wa hotuba yangu nitakayowasilisha hapa Bungeni. Sasa kwa muda huo mfupi niongelee mambo machache ambayo yanawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lililozungumzwa kubwa hasa lilihusu migogoro ya watumiaji ardhi ikiwemo mifugo pamoja na upatikanaji wa malisho kwa ajili ya wafugaji. Ilifikia hatua Waheshimiwa Wabunge wakamshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba aweze kuliingilia kati suala hili kwa sababu ni suala kubwa, wafugaji wanahangaika huku na kule kutafuta malisho, wafugaji wameingia kwenye migogoro mikubwa na watumiaji wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narejea kusema kwamba kumekuwa na tatizo kubwa la wafugaji mahali pote ambapo wamekuwa wakilalamikiwa suala la kuingilia kwa wafugaji katika maeneo mbalimbali ya watumiaji wengine wa ardhi na kuleta adha kubwa sana kwa wafugaji katika kitendo hicho cha kukosa malisho na kutafuta maji huku na kule. Ikafika mahali Waheshimiwa Wabunge wakamuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kuingilia kati suala hili ili kuweza kutafuta suluhisho lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu tayari ameshalishughulikia suala hili kwa kiwango kikubwa. Wizara tano zilipewa jukumu la kuhakikisha kwamba zinapitia maeneo mbalimbali kuona kwamba suluhisho la migogoro, kukomesha migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi kama kilimo, hifadhi na maeneo mengine na tayari Kamati hiyo imeshamaliza kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba mambo yaliyopendekezwa kwenye hii Kamati yatakuwa ni suluhisho kubwa la migogoro kwa wafugaji wetu; litakuwa suluhisho kubwa la migogoro ya wafugaji pamoja na watumiaji wengine wa ardhi. Upande wangu mimi yale yaliyoshauriwa kwenye Wizara yangu kuyatekeleza niseme tu hapa kwamba haitafika mwezi Desemba, 2018, nitakuwa nimemaliza mapendekezo yote ya Kamati yaliyowasilishwa kwangu

kuyatekeleza, ili wafugaji hawa waweze kupata ahueni katika nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine ambalo linazungumzia sana suala la Ranchi zetu za Taifa ambazo zinamilikiwa na Shirika letu la *NARCO.* Ugawaji wake, jinsi ulivyogawiwa na wafugaji wengi kuendelea kukosa maeneo ya malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika niombe tu kutoa taarifa kwamba nililiambia Bunge lako kwamba, tunafanya tathmini; tayari tathmini tumeshamaliza ya mashamba yote ya kwetu tuliyonayo, Ranchi za Taifa zote, *holding grounds* zote na hata *LMUs* zote. Tumemaliza kufanya tathmini na sasa tunaingia kwenye kupanga matumizi sahihi ya mashamba haya. Nikuhakikishie kwamba, baadhi ya wafugaji wetu wanaotangatanga huku na kule watapata maeneo ya kulishia mifugo yao katika maeneo haya katika mashamba haya ya taifa ambapo tutawaondoa wale wawekezaji ambao wamekuwa matapeli katika mashamba haya na kuweka wafugaji ambao wanahangaika huku na kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika tathmini hiyo bado tuna mashamba mengine ambayo yapo yanamilikiwa na Serikali ambayo nayo tunafikiria kwamba baadhi ya wafugaji wengi tutawaondoa katika maeneo mbalimbali na kuwaweka kwenye mashamba haya. Hivyo tatizo la malisho kwa kiwango kikubwa, tukitekeleza haya tuliyoshauriwa na Kamati, lakini na taasisi nyingine zinazohusika, kama mwenzangu wa maliasili na utalii akitekeleza na yeye yale aliyoshauriwa na Kamati tatizo la malisho kwa wafugaji wetu litapungua kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hili tatizo ambalo linani-*face* hapa, la muda labda nizungumzie suala lingine lilizungumzwa suala la upigaji chapa, kwamba je, katika hotuba ya Waziri Mkuu limeoekana tu suala la upigaji chapa. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge wasubiri kwa

sababu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi itakuja na hotuba yake hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na labda nimalizie hili suala lililozungumzwa, linalohusu, naona kengele ya kwanza, suala la uvuvi haramu. Suala la uvuvi haramu niombe jambo moja kwa Bunge hili, jambo hili ni kubwa, tunaendesha *operation* zaidi ya tatu za uvuvi haramu. Kuna *Operation Sangara 2018,* kuna *Operation MAT* na una *Operation Jodari.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mambo makubwa ambayo yamefanyika katika hatua za utekelezaji wa mambo haya. Kwa sababu Wabunge wengi wameonesha nia ya kutaka kuelewa jambo hili na kwa sababu Wabunge wengi wameuliza maswali mengi sana katika eneo hili, ilinilazimisha/ nililazimika; na Kamati yangu ya Maji, Kilimo na Mifugo iliniagiza kwamba nifanye semina kwa Wabunge wote ili tuweze kuelezana kwa kina nini kinachotokea katika suala la uvuvi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu maelekezo yao waliponipa tayari nimeshaomba kibali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimeomba kibali kwa Mheshimiwa Spika, ili akubali tarehe ya 21 Aprili 2018 tuweze kutoa semina ili tuwaambie Waheshimiwa Wabunge ili tuwaambie Watanzania jinsi gani rasilimali za taifa ambavyo zimekuwa zikifujwa na watu mbalimbali wasiolitakia mema taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme yapo mambo ambayo yameshauriwa na Wabunge ambayo ni madogo ya uboreshaji. Mimi yale sina tatizo katika uboreshaji na ndiyo maana hata katika lile Bunge nilisema kwamba Mbunge yeyote mwenye hoja yoyote, mwenye ushahidi wowote atuletee sisi ili tuweze kuchukua hatua.

Naomba kutoa taarifa kwamba tayari tumeshasimamisha kazi watumishi tisa ambao walihusika kwa namna ile au nyingine katika kuhujumu zoezi hili, katika kujinufaisha binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile kuna mambo yalijitokeza ikafikia wananchi kwamba, hata wanapotaka kubeba samaki wao tu wa kula nyumbani, ka-*box* kake ka samaki 10, samaki watano wanazuiliwa kwamba hairuhusiwi kisheria, hapana. Nimekataa na nimetoa maelekezo kwa watendaji wote wa Serikali lazima wajue kwamba samaki hawa lazima watasafirishwa kwa njia ya usafiri kuwafikia walaji. Na hili haliwezi kuendelea kutokea...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma naomba ukae. Mheshimiwa Mpina.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kamba, tayari tumeshatoa maelekezo mambo haya yanafanyika, sasa hakuna tena kuzuiliwa wananchi kusafirisha samaki kwa ajili ya kitoweo. Hata hivyo hii isigeuzwe tena ikawa *loop hole* ya watu kutumia mabasi ya abiria kwa ajili ya kufanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Mheshimiwa *Engineer* Isack Kamwelwe atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ajiandae.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kushukuru kwa kupata nafasi hii ili na mimi niweze kujibu baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezichangia wakati wa kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme kwamba, naunga mkono hoja ya hotuba yote ya Mheshimiwa Waziri

Mkuu kwa sababu, imeelekeza, imeeleza utekelezaji wa miradi ya maji katika bajeti ya mwaka huu wa fedha 2017/2018. Hotuba imeeleza kwamba kwa upande wa vijijini tayari huduma ya maji safi na salama imefikia asilimia 60 na kwa upande wa mijini huduma ya maji safi na salama imefikia asilimia 78. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunaendelea na utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ambayo tuliianza mwaka 2006/2007. Programu ya kwanza iliisha mwaka 2017, Juni. Katika awamu hii ya kwanza tulilenga kutekeleza miradi 1,810; lakini hadi leo tayari tumeshatekeleza miradi 1,468. Miradi hiyo tumejenga vituo vya kuchotea maji 123,888 lakini katika vituo hivyo ni asilimia 60 tu ya vituo ndio vinavyotoa maji kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo kwamba miradi mingi tuliweka *pump* za kutumia dizeli, jenerata za kutumia dizeli ambazo Jumuiya za Watumiaji Maji wameshindwa kuziendesha. Hata hivyo yapo maeneo ambayo hizi jumuiya tulizoziunda kwa ajili ya kuendesha miradi ambayo imekamilika wao wenyewe wameshindwa kuziendesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo yaliyolengwa kwamba maji yatapatikana kutoka maeneo hayo lakini kutokana na mabadiliko ya tabianchi maeneo hayo yamekauka maji. Hivyo, Katiba bajeti inayokuja tunataka tuhakikishe kwamba vile vituo vyote ambavyo tayari vimeshajengwa na havitoi maji tutaweka fedha, tutatenga bajeti ili kuhakikisha kwamba tunapeleka yale maji na tunaondoa changamoto zote ambazo zimejitokeza zinazofanya vituo vyote hivi visitoe maji kwa sababu kama vituo hivi vyote vingetoa maji sasa hivi tungekuwa tunazungumzia upatikanaji wa maji safi na salama katika maeneo ya vijijini tungekuwa tumefikia asilimia 85 kama ilivyoelekezwa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mijini tayari tuko asilimia 78. Miradi mingi imeshatekelezwa katika maeneo ya mijini na maji yapo, kwa mfano katika Jiji la Dar es Salaam. Sasa hivi bajeti inayokuja tutatenga bajeti ili kuendelea

kupanua mtandao, ili wananchi wengi waweze kupata maji tuweze kufikia asilimia iliyoelekezwa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwamba maeneo ya miji tufike asilimia 95. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako tukufu katika bajeti ya mwaka 2016/2017 Waheshimiwa Wabunge waliielekeza Wizara ya Maji na Umwagiliaji kuunda Wakala wa Maji Vijijini. Naomba kutoa taarifa kwamba Wizara inaendelea na taratibu za uanzishwaji wa Wakala wa Maji Vijijini wenye majukumu ya kujenga miradi, kusaidia usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji vijijini. Kwa sasa Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imekamilisha kazi ya kuandaa nyaraka muhimu ambazo ni *strategic plan, business plan* na *framework document* kwa kutumia Sheria ya Uanzishwaji wa Wakala nchini ili kusaidia uanzishwaji wa wakala hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nyaraka hizo zitaenda sambamba na maoni ya wadau na baadae itapelekwa kwenye mamlaka husika kwa idhini ya uanzishaji wa taasisi hiyo. Mategemeo ya Wizara ni kuwa Wakala wa Maji Vijijini, utaanza kufanya kazi kuanzia mwezi Julai kwenye bajeti ya 2018/2019. Kwa hiyo, tupo mahali pazuri katika kuhakikisha kwamba tunaanzisha Wakala wa Maji Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wameligusa sana ni kuhusiana na mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India ambao utatuwezesha kutekeleza miradi 17, kati yake 16 ikiwemo Tanzania Bara na mradi mmoja Tanzania Visiwani. Upatikanaji wa fedha hizi umechelewa kutokana na majadiliano kati ya Serikali ya India na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo imechukua muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, majadiliano haya yamechukua muda mrefu kutokana na sababu kwanza Bunge letu tukufu mwezi Septemba lilibadilisha Sheria ya *VAT,* kwa hiyo, ili kukamilisha taratibu Sheria ya *VAT* ianze kufanya kazi imecheleweshа kuweza kusaini *Financial Agreement,* lakini kwa sasa tumefikia hatua nzuri na niwahakikishie tu

Waheshimiwa Wabunge kwamba, fedha hizi dola milioni mia tano tunatarajia kuzitumia kwenye bajeti ijayo kwa mwaka wa fedha 2018/2019…*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla ajiandae.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia kukutana hapa leo tukiwa na afya njema. Pili, na mimi nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, ambayo ni hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitachangia kupitia hoja mbalimbali ambazo zimewasilishwa na Waheshimiwa Wabunge kwa muda wa kipindi chote cha hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utagawanyika katika sehemu tatu muhimu; kwanza nitajikita zaidi kwenye usafiri wa anga, halafu nitakwenda kwenye usafiri wa majini, halafu nitazungumzia mwisho usafiri wa nchi kavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa usafiri wa anga kama unavyojua nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba, anga letu linakuwa salama ili Watanzania na wageni wetu mbalimbali waweze kusafiri kwa njia salama. Katika kutekeleza jambo hili kama mnavyojua, wiki moja iliyopita tulizindua mradi wa ujenzi wa rada nne za kisasa ambapo rada ya kwanza itajengwa pale Dar es Salaam, ya pili

itajengwa Mwanza, ya tatu itajengwa huko Songwe na ya nne itajengwa huko KIA. Mradi ule utakuwa na gharama ya takribani dola za Kimarekani bilioni 67.3 na kazi inaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mnavyojua mwaka jana peke yake katika viwanja vyetu vya ndege takribani wasafiri milioni 4.13 waliweza kusafiri, hiyo ikiwa ni Watanzania pia na watu wengine kutoka nje ambao wanakuja nchini kwetu kwa ajili ya utalii. Ili kuhakikisha kwamba tunajenga miundombinu ya kisasa kuvutia watu watumie kwa kiwango kikubwa usafiri wa anga pamoja na wageni wetu, tumeanzisha miradi takribani 11 sasa nchini ambayo tunafanya ukarabati wa viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukianzia pale Dar es Salaam tunajenga jengo la kisasa ambalo litakuwa na uwezo wa kuchukua abiria milioni 6.5 kwa mwaka na gharama yake ni shilingi bilioni 560 ukilinganisha na jengo lililoko sasa hivi ambalo lina uwezo wa kuchukua abiria milioni 2.5 kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa huko Mtwara tunakarabati uwanja wa Mtwara ambao tunaujenga sasa uwe na urefu wa kilometa 2.8 ambao ndege kubwa sasa kwa mfano *Airbus A320, Airbus A330* ziweze kutua bila matatizo. Tayari mkandarasi tumeshampata ambaye ni *Engineering Construction Engineering Company* ambaye atafanya kazi hiyo kwa gharama ya takribani shilingi bilioni 53. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mwanza tunaendele na ukarabati wa uwanja wa Mwanza ambao tayari sasa hivi tumeongeza eneo la kutua ndege ambalo sasa hivi limekuwa na urefu wa kilometa 3.5 na gharama ya kazi hiyo yote ni takribani bilioni 85. Kazi inayoendelea sasa hivi ni ujenzi wa jengo la *control tower* pamoja na maegesho ya ndege za abiria na ndege za mizigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi mradi huo umefikia asilimia 68. Kazi tunayojipanga sasa ni kuhakikisha tunatafuta fedha kwa ajili ya kujenga jengo la abiria za kisasa lenye uwezo wa kuchukua takribani abiria milioni 2.5 kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mambo ya viwanja vya ndege tumeenda huko Sumbawanga ambako tayari tunataka kujenga uwanja wa ndege ambao una urefu wa kilometa 1.75 na utajengwa kwa gharama ya takribani shilingi bilioni 55.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hiyo vilevile inafanyika huko Shinyanga ambako sasa tutatanua uwanja wetu kufikia kilometa mbili ambayo itagharimu takribani bilioni 49.5 na kazi hiyo tayari mkandarasi tumeshampata. Pia huko Shinyanga tutajenga jengo la abiria.

Aidha, kazi kama hiyo itafanyika Kigoma na Tabora ambako kwa maeneo hayo mawili tutajenga mjengo ya abiria na pesa zipo. Sasa hivi tunatafuta mkandarasi kwa upande wa Kigoma, lakini kwa upande wa Tabora tayari mkandarasi wa kazi hiyo ameshapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kiwanja cha Ndege cha Musoma tayari mkandarasi tumempata na sasa hivi tuko katika mazungumzo ya kuweza kufikia mapatano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kiwanja cha ndege cha huko Songwe kazi ya ujenzi wa jengo la abiria unaendelea na vilevile tunajaribu kutafuta au tayari tumeshampata mkandarasi kwa ajili ya kuweka taa sasa za kuongozea ndege ambapo ndege sasa zitaweza kutua saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama ya kazi hiyo ni takribani shilingi bilioni 4.8. Tayari mkandarasi yupo na tunaendelea na mazungumzo yake kuona lini tutasaini mkataba ili kazi hiyo ianze mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna kazi ambayo inaendelea vile vile huko Songea pamoja na kiwanja cha ndege cha Iringa. Tunaamini hivi karibuni na huko tutaweza kupata mkandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyoelewa kwamba, unaweza kuwa na viwanja vya ndege vizuri, lakini kama huna ndege zako inakuwa si jambo zuri sana. Kwa kulijua hilo Serikali imenunua ndege sita kama wote mnavyojua, ndege tatu sasa hivi ziko mjini hapa Tanzania na zinafanya safari zake za kwenda Dar es Salaam, Dodoma, Tabora, Kigoma, Mwanza, Bukoba, Kilimanjaro, Zanzibar na Songea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni tutaanza safari za Mpanda pamoja na Tanga. Vilevile tutaanza safari za kwenda Entebe huko Uganda, Bujumbura, Burundi na Nairobi, Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo kwa ufupi ndiyo kuhusu usafiri wa anga. Sasa naomba kwa ufupi niende kwenye usafiri wa majini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mbarawa, muda wako umekwisha, lakini naona Wabunge wote wanataka kuendelea kukusikiliza hapa, kwa hiyo, ngoja nikuongezee dakika chache umalizie hayo maeneo mawili yaliyobaki. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa muda huo na fursa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa eneo la usafiri wa majini tuna maziwa makubwa, Ziwa Tanganyika na vilevile tuna Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Ziwa Tanganyika tayari tuna utaratibu tumeshaanzisha wa kununua meli ya abiria ambayo itachukua abiria 600 na mizigo tani 400 ambapo tunaendelea kumtafuta Mkandarasi. Vilevile tunafanya ukarabati wa *MV* Liemba ambapo tayari tumeshapata kampuni ya kutoka Denmark na tumetenga takribani bilioni 3.4 kwa kuanzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *Lake Vicktoria,* kama mnavyojua tunataka kujenga meli ya kisasa. Bado tunaendelea na mazungumzo kutoka Korea. Meli hii itakuwa na uwezo wa kuchukua abiria 1,200 na mizigo tani 200 na magari 25 kwa vile itakuwa ni meli ya kisasa. Tunaamini hivi karibuni tutafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikigusia kidogo kuhusu usafiri wa Kisiwa cha Mafia, najua muda mrefu wananchi kule wamelalamika. Sasa hivi tunataka kujenga *land craft* ambayo ni boti ya kisasa yenye uwezo wa kupeleka abiria kutoka Dar es Salaam kwenda Mafia. Bajeti inayokuja tutatenga takriban shilingi bilioni tatu kwa kuanzia tunaamini baadaye huko mbele tunaweza kumalizia ili wananchi wale sasa na wao tuweze kuendelea au kuwatatulia changamoto inayowakabili kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho kama nilivyosema ni kuhusu usafiri wa nchi kavu. Hapa kuna Wabunge wengi walitoa hoja zao, nikianzia kwa Mheshimiwa Mbunge hapa ambaye yeye alikuwa anazungumzia barabara yake kutoka Kidahwe - Kasulu yenye urefu wa kilomita 63. Kazi inaendelea na tunatafuta hela ili mkandarasi sasa asiweze kusimama kuhakikisha kazi ile inamalizika kwa muda unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuna mradi ambao unaendelea sasa hivi wa ujenzi wa barabara ya kutoka Mafinga - Igawa yenye urefu wa kilomita 137.9, kazi inaendelea vizuri. Pia huko Njombe tunaenda mpaka Makete kwa ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 107.4 na kazi inaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna miradi mingi lakini kwa vile bajeti yetu inakuja, naomba niishie hapa na wakati wa bajeti tutazungumza mengi, Mungu akitujalia. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla na Mheshimiwa Dkt. Kalemani ajiandae. Jamani hawa ni Madaktari wa kisomo, kwa hiyo lazima wapewe heshima yao. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuturuhusu na sisi tuweze kuanza kutoa mchango kwenye baadhi ya maeneo yanayogusa sekta zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwanza naunga mkono hoja yake aliyoiweka mezani na maelezo ya kina kuhusu baadhi ya hoja zilizotolewa na Wabunge tutayatoa wakati wa bajeti yetu ya Wizara. Hapa niseme tu yale yaliyo ya jumla na nianze kwa haya ambayo yamesemewa kwenye michango na yamejitokeza kwenye baadhi ya maswali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na hili ambalo lilikuwa linaongelea kusuhu masuala ya upelelezi kuchukua muda, haki za watuhumiwa na watu kubambikwa kesi. Niseme kwenye jambo hili ambalo ni la msingi na linahusu haki za watu wala sisi Serikali hatuwezi tukatofautiana na ninyi Waheshimiwa Wabunge. Hata juzi Arusha kule Mheshimiwa Rais alituelekeza kati ya mambo ambayo tunatakiwa tuyafanyie marekebisho kwenye utendaji wetu wa kazi ni kuhusu masuala ya ubambikaji wa kesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme hili ni jambo ambalo tumelichukua na tumeshaanza kulifanyia kazi. Kama kuna baadhi ya maeneo ambako bado mambo hayo yanaendelea kujitokeza yatakuwepo makosa ya kibinadamu ambayo yanaweza kujitokeza katika utekelezaji wa kazi, lakini Serikali kama Serikali kusudi lake ni kuhakikisha inalinda haki

za raia wake kwa sababu ni sehemu ya haki muhimu sana ambazo Watanzania wanatakiwa kuzipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upelelezi kuendelea kufanyika wakati mtu ameshafikishwa Mahakamani, hili nalo lipo kwenye utaratibu wa kisheria na si wote wanapokwenda Mahakamani wanakosa dhamana. Kwa hiyo, huwa tunaona ni vema mtu akapelekwa Mahakamani kwa sababu dhamana inakuwa wazi ili mtu aweze kupata dhamana hata kama upelelezi unaendelea. Kwa wale wanaokwama kupata dhamana yenyewe inakuwa inatokana kwa kiwango kikubwa na aina ya makosa pamoja masuala ya kiusalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge walilisemea kwa sauti kubwa suala hili linalohusiana na watu kulundikana magerezani huku wakiwa hawajapata ufafanuzi kuhusu makosa yao ama hatma ya makosa yao. Hata sisi kama Wizara ni jambo ambalo tunaliangalia kwa jicho la tofauti. Kwanza ni gharama kwa Serikali kuwa na watu ambao labda makosa yao yangeweza kumalizika haraka, lakini la pili ni jambo hatarishi kuwachukua watu ambao wana makosa madogo wakakaa pamoja na watu walio na makosa makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewaambiwa hata wasaidizi wangu Jeshi la Polisi pamoja na wengine kwamba kama kuna watu ambao tunaweza tukatathmini tukajua yale waliyofanya na tukaangalia kama hayana matatizo ya kiusalama kwa wao kuwa nje, basi ni vema sana hao watu kutokuwachanganya na watu ambao wana makosa makubwa ambao wako magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu taarifa za kiuchunguzi tulizozipata kuna baadhi ya watu wanapokaa na wahalifu wazoefu ama na wahalifu wenye makosa makubwa ilhali wao wakiwa na makosa madogo, wengine wanapata mafunzo ya kufanya makosa makubwa na wengine watengeneza ushirika na wale ambao wanafanya makosa makubwa. Kwa maana hiyo,

tunazipokea zile hoja na tutaendelea na kuzifanyika kazi. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu sekta hizi zote zinapofanya kazi kwa pamoja zinaharakisha utoaji wa haki za watu ameziangalia kuanzia Mahakama hadi Magereza pamoja na Jeshi la polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo ilizungumziwa ni kuhusu matumizi ya askari kwenye masuala ya chaguzi. Sisi kama Jeshi la Polisi na kama Wizara ya Mambo ya Ndani hatupendi kuona wananchi wetu wanaumizana kwenye masuala ya uchaguzi. Kwenye chaguzi nyingi tumeshuhudia na mara zote ninapopata fursa ya kuongea na wananchi naendelea kuwaambia ni aibu sana kwa nchi ambayo ina siasa za vyama vingi kwa zaidi ya miaka 20 lakini wananchi wake wanafanyiana fujo pale panapotokea pana uchaguzi katika eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba kama pana uchaguzi katika Kata A na vyama vyote vinashiriki maana yake vyama vyote vitakuwepo katika eneo hilo. Kwa hiyo, tulitarajia watu waheshimu taratibu na wanapoheshimu taratibu maana yake hapatakuwa na ugomvi katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara ya Mambo ya Ndani hatutavumilia kuona watu wanakatana mapanga halafu tukasema kwa sababu ni chaguzi ama ni siasa tukaacha kwa sababu tunawajibika kulinda usalama wa raia mara zote na kuwahakikishia usalama mara zote wanapotokea wana mikusanyiko ama wako katika maisha yao ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kwa sababu nimeisikia kengele, liliongelewa suala la kijana kule Mtwara pamoja na lile la Msikitini. Nimewaelekeza wafanye uchunguzi wa ndani ili tuweze kupata taarifa kamili na tutaendelea kuzitoa taarifa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge pale panapokuwepo

na jambo limempata mmoja wa Watanzania tuepuke sana kuliunganisha jambo hilo na dini yake kwa sababu yanapotokea masuala ya uhalifu mtu hakamatwi kutokana na dini yake, kabila au chama chake cha siasa alichonacho bali anakamatwa kutokana na kosa alilolifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tusije tukatumia utaratibu wa kuunganisha kosa mtu alilofanya pamoja na kabila lake, dini yake au chama chake cha siasa. Ingekuwa vitu hivi havifanywi na watu wa makabila haya haya, wa vyama hivi hivi, wa dini hizi hizi basi katika maeneo mengine ambapo tunapaamini kwamba ni mahali patakatifu tusingekuwa tunapata makosa ya aina hiyo. Kwa hiyo, watu wanakamatwa kutokana na makosa waliyofanya na wala kosa alilofanya mtu lisiunganishwe na imani yake, chama chake cha siasa ama kabila lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kufafanua hivi vitu kwenye bajeti zetu za Wizara husika. Kwa muda huu, naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu iliyowekwa mezani. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kalemani na Mheshimiwa Ikupa Stella ajiandae.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pia namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutupa fursa na sisi tutoe michango yetu kwenye hoja aliyoiweka mezani. Nampongeza zaidi yeye na Mawaziri waliopo kwenye Wizara yake kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kufanya na kwa miongozo mbalimbali ambayo wamekuwa wakitupa katika utekelezaji wa majukumu haya mazito tuliyopewa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitambue michango mingi ya Waheshimiwa Wabunge iliyotolewa kwenye sekta ya maliasili na utalii. Niseme tu kwamba

michango yote tumeipokea, tunaifanyia kazi na zaidi maelezo ya kina tutayatoa wakati wa hotuba yetu ya bajeti ili kuwekana vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, naomba nitoe ufafanuzi kwenye mambo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa lililojitokeza katika michango mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge ambalo napenda kulitolea ufafanuzi ni hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Chegeni, Mheshimiwa Njalu, Mheshimiwa Gimbi na Waheshimiwa Wabunge wengine kuhusiana na migogoro ya wafugaji na Hifadhi za Taifa. Naomba hapa nizungumzie pia jambo zima linalohusiana na zoezi la mipaka na utatuzi wa migogoro hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia maelekezo ya Serikali yaliyopitia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye mipaka yote ya maeneo yaliyohifadhiwa tumeweka vigingi *(beacons)* ambazo zinayatambua maeneo ya hifadhi na kuonesha maeneo ya vijiji yanaishia wapi. Mpaka sasa tumefanikiwa kuweka takribani vigingi 27,942 sawa na asilimia 79 ya malengo tuliyojiwekea ya kuweka vigingi katika maeneo yote yaliyohifadhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi hii kubwa ambayo imefanyika, bado kuna changamoto zinajitokeza. Changamoto ya kwanza kubwa ambayo tunaipata ni kwamba kuna wananchi walikuwa wakiishi katika maeneo ya hifadhi ama wakifanya shughuli mbalimbali katika maeneo ya hifadhi wakiamini ni maeneo ya vijiji. Pamoja na mwongozo aliotupa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba *beacon* ziwekwe tu kwanza halafu baadaye tutazungumza na wananchi nini litakuwa suluhisho kwa yale maeneo ambayo tayari wamekuwa wakiyatumia na sisi tumekuwa tukifanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa naomba nitumie fursa hii kuwaondoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na wananchi kwa sababu tunafanya kazi sasa

baada ya zoezi la kuweka vigingi kukamilika ya kupita kwenye maeneo hayo ambayo yanaonekana aidha vigingi vimeingia kwenye maeneo ambayo wananchi wamekuwa wakiyatumia ama kwenye yale maeneo ambapo hifadhi imeingia ndani zaidi kuliko ambavyo ilikuwa kabla hatujafanya zoezi la uhakiki wa mipaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hiyo tumeanza kuifanya na tunaifanya sisi wenyewe, mimi na mwenzangu Mheshimiwa Naibu Waziri hatua kwa hatua tunakwenda kwenye eneo moja baada ya lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro mingine unakuta eneo ambalo limehifadhiwa na linatumika kwa matumizi ya shughuli mbalimbali za kibinadamu ni dogo sana. Kibinadamu tumeanza kufikiria kufanya *variation* ya mipaka yetu na kuyaacha nje maeneo haya ili wananchi waweze kuyatumia kama tunaona kiikolojia hakuna madhara yoyote yale yatakayojitokeza ili tupunguze migogoro ambayo tumekuwa tukiipata baina ya wahifadhi na wananchi ambao ni majirani zetu kwenye maeneo yaliyohifadhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, kuna maeneo mengi ambayo yalitangazwa kama maeneo ya hifadhi ambayo yamekuwa yakitumika kwa muda mrefu sasa kwa shughuli mbalimbali za kibinadamu. Maeneo haya tumeshaamua kuyaachia, baadhi ya maeneo hayo yana Ranchi za Taifa, viwanja vya ndege na vijiji ambavyo vimetangazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, katika ile ripoti tuliyopewa na wataalam wa tume iliyoundwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, tayari kuna maeneo takribani 14 tumeyaachia lakini pia kuna maeneo mbalimbali kama alivyozungumza ndugu yangu Mheshimiwa Vuma tumepewa miongozo na viongozi wetu wakuu kwa mfano Mheshimiwa Rais alisema tuachie eneo la msitu wa kule Kagera Nkanda na tumeshaamua kuachia eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kinachofanyika sasa ni kufanya *variation* ya mipaka ili tuweze kutangaza rasmi lakini hatuna taarifa za wananchi kunyanyaswa katika maeneo ambayo tayari tumekwishatoa mwongozo wa kuyaachia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hivyo kuna maeneo ya Mkungunero, kuna baadhi ya maeneo ambayo tumeona kwamba tunapaswa kufanya *variation* ya mipaka na kuyaachia ili wananchi ambao waliokuwa wanayatumia kwa muda mrefu waendelee kuyatumia kwa sababu hata kama kwa mujibu wa sheria siyo eneo lao, lakini wao wanaamini ni eneo lao. Kwa hivyo, mgogoro hautakwisha kwa sababu wahifadhi wataendelea kuamini kwamba wananchi wamevamia eneo lao, wakati na wananchi wanaendelea kuamini kwamba ni eneo lao hata ukiwaambia nini hawakuelewi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, katika jitihada za usuluhishi ambazo tunazifanya ni pamoja na kukubali kuachia baadhi ya maeneo au kubadilisha baadhi ya maeneo. Kwa mfano, kule Utete tumeachia eneo la Msitu wa Kale na tunafanya sasa taratibu za kurekebisha ili lirudi kwa wananchi lakini tumewaomba Halmashauri watupe eneo lingine lililopo mbali zaidi na mipaka ya mji ili tuweze kulihifadhi ku-*compensate* kwa eneo ambalo tumeliachia, kwa hivyo jitihada hizo zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu migogoro baina ya wanyamapori ambao wanatoka katika maeneo ya hifadhi na kwenda kwenye maeneo ya wananchi. Kwanza hapa changamoto kubwa ambayo inajitokeza ni kwamba wananchi wengi katika miaka ya hivi karibuni wamekuwa wakifanya shughuli zao za kibinadamu aidha kwenye shoroba ambazo ni mapito ya wanyamapori ama kwenye maeneo ya karibu sana na *buffer zone*, eneo kinga la maeneo yaliyohifadhiwa ambazo ni mita 500 tu. Wanyama hawajui mipaka ambayo tuliojiwekea sisi binadamu wamekuwa wakitoka kwenda kwenye maeneo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, tunatoa elimu ya wananchi kuzungusha mizinga ya nyuki kwenye maeneo ya mashamba yao kwa sababu wanyama kama tembo huwa wanaogopa uwepo wa mizinga ile na kurudi kwenye maeneo yaliyohifadhiwa ili wananchi waweze kuepukana na migogoro ambayo inayosababishwa na wanyama hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunazidi kujenga madungu ama *observation towers* kwenye maeneo ya jirani na maeneo wanayoishi wananchi hususani maeneo korofi kwa mfano kule Itilima ambako juzi kumetokea maafa na kule Bunda kwenye Vijijji vya Kihumbu, Hunyali na Maliwanda ili askari wetu waweze kuwa-*track* wanyamapori aina ya tembo ambao wamekuwa wakizoea kwenda maeneo ya vijiji na kuweza kuwarudisha kwa kutumia teknolojia za kisasa kama teknolojia ya kutumia *drones* kwenye maeneo ya mipaka...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Merdad Kalemani atafuatiwa na Mheshimiwa Ikupa Stella Alex, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde ajiandae.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangie katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa heshima ya pekee ningeomba sana kwa idhini yako Wabunge wote tugonge meza zetu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo imesheheni mambo mengi ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hivyo ndivyo basi, naanza kabisa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja ili hata kama nikisahau niwe nishamemaliza kabisa katika suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ya msingi ambayo yamezunguzwa sana katika hotuba hii kwa upande wa nishati ni mambo matatu. Pamoja na mambo mengine napenda sana nijielekeze zaidi katika hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vyazo vya kuzalisha umeme kwa upande wa gesi na suala la maji limetajwa kwa kiasi kikubwa. Napenda kuliondoa wasiwasi Bunge lako Tukufu kwamba vyanzo vya kuzalisha umeme kwa njia ya maji havijatajwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi si kweli, Ilani imetaja vyanzo haijabainisha mradi kwa mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ilani yetu aya ya 43.A imeeleza vyanzo vya msingi ambavyo Serikali itajielekeza katika kuzalisha umeme wa uhakika, unaotabirika na wa gharama nafuu na vyanzo vya maji vikiwemo. Kwa hiyo, napenda sana niondoe wasiwasi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ukurasa wa 81 umetaja bayana vyanzo halali, vyanzo vitakavyotupunguzia bugudha na tofauti ndogo ndogo na migogoro ya upungufu ya umeme ikiwemo vyanzo vya gesi asilia, maji, *geothermal*, makaa ya mawe pamoja na upepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kuwaondoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwamba tunapotaja vyanzo vya kuzalisha umeme kimsingi hatutaji mradi kwa mradi. Mradi kwa mradi utakuja katika mipango yetu ya maendeleo kisekta ambayo tutakuja kuiwasilisha itakapofika wakati wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nieleze kwa nini nasema hivyo. Kwanza kabisa Serikali haijatelekeza kutumia

gesi asilia. Hivi sasa Wabunge wote tunatambua tunayo trilioni 57.5 ya gesi asilia na umeme tunaotumia kwa sasa hivi zaidi ya *megawatt* 787 zinatokana na gesi asilia. Kwa hiyo, si kweli kwamba tumetelekeza kutumia gesi asilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais tarehe 3 Aprili, 2018 alizindua mradi mkubwa wa kuzalisha *megawatt* 198 ambao unakwenda kutupatia *megawatt* 240 mwishoni mwa Juni, 2018. Kama hiyo haitoshi Desemba, 2018 tutaanza tena kutumia nishati nyingine ya gesi asilia ya *megawatt* 185 kutoka kwenye mradi mwingine wa Kinyerezi II nao unatokana na gesi asilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwakani tunaanza kujenga mradi mwingine wa gesi asilia kutoka Somanga Fungu wa *megawatt* 330, nao unatokana na gesi asilia. Mwaka huo huo Julai tutaanza kujenga mradi mwingine wa *megawatt* 300 unaotokana na gesi asilia huko Mtwara. Kinyerezi peke yake kuja kufika mwaka 2020 tutakuwa na *megawatt* 1,560 za gesi asilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusisitiza kwamba matumizi ya gesi asilia bado ni mengi sana. Mbali na kuzalisha umeme, gesi asilia itatumika katika masuala mengine yafuatayo:-

Kwanza, jumla ya trilioni 8.8 itatumika kuzalisha umeme; trilioni 4.3 itatumika kwenye viwanda vya mbolea na *petrochemicals;* trilioni 1.2 itatumika kusambaza gesi majumbani na kwenye magari yetu na trilioni 1.1 itatumika pia kwa ajili ya viwanda vya vyuma. Kwa hiyo, niendelee kusema bado matumizi ya gesi asilia ni makubwa na Serikali inaendelea kuyazingatia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kusema kwenye mradi wetu wa *LNG* tutatumia tani milioni 10 kila mwaka za gesi asilia. Kwa hiyo, nipende kusema tu kwamba pamoja

na vyanzo hivyo tuna maana kwamba bado tunaendelea kutumia kile kinachoitwa *energy mix* kwa maana ya kutumia vyanzo vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini sasa tunataka kuendeleza Mradi wa *Stiegler's Gorge?* Nitumie nafasi hii kusahihisha kidogo, naomba Waheshimiwa Wabunge mradi huu tuuite Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Rufiji badala ya *Stiegler's Gorge*. *Stiegler's Gorge* ilikuwa ni jina la Mzungu aliyefika maeneo yale na alishaondoka na hayupo. Kwa hiyo, si vema sana kuendelea kumuenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema hapa, Mradi huu wa Maporomoko ya Mto Rufiji utakaoweza kuzalisha *megawatt* 2,100 ni mkubwa sana. Waheshimiwa Wabunge, tutambue kwamba tumekuwa tukitumia miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia maji tangu enzi za ukoloni na miradi hiyo tunaitambua; tuna Mradi wa Kidatu, Mradi wa Kihansi, Mradi wa Mtera na *New Pangani Fall*. Miradi hii ina uhai wa zaidi ya miaka 40 na imeshaanza kuchoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitumie nafasi kueleza kwamba ni vema sana tukaanza sasa kutumia miradi mikubwa ambayo itatutoa kwenye changamoto za upatikanaji wa umeme. Kuanza kwa mradi huu kutakuwa na manufaa makubwa yafuatayo:-

Tukiingiza *megawatt* 2,100 kutoka kwenye zile tulizonazo na zingine tukaingiza kwenye vyanzo mbalimbali tuna uwezo sasa wa kujitosheleza hapa ndani na kuwauzia majirani zetu. Kwa hiyo, niombe Bunge lako Tukufu kwa pamoja tumuunge mkono Mheshimiwa Rais wetu kwa kuanzisha mradi huu. Kwa kweli tukifanya hivyo tutajenga sasa uchumi wa viwanda utakaotuondoa kwenye changamoto za umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ukijengwa pamoja na kupeleka umeme katika gridi ya Taifa lakini utaleta maendeleo makubwa sana. Moja ya maendeleo ni ujenzi

wa barabara za viwango vya lami kuelekea kwenye mradi wenyewe. Maendeleo mengine kwa sababu bwawa hili litakalojengwa litakuwa na urefu wa kwenda juu takribani ghorofa zaidi ya 78, itakuwa ni chanzo kikubwa cha kuvutia utalii ambapo utaleta fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile bwawa hili litahifadhi maji ya kutosha hata kwenye kilimo cha umwagiliaji. Niwashawishi Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono juhudi za Serikali ili mradi huu uendelee kutekelezeka sambamba na miradi mingine ya kuzalisha umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye mradi....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha, nakupa dakika moja.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye mradi wa *LNG,* unaendelea vizuri. Utekelezaji wa miradi unaenda hatua kwa hatua, tulishakamilisha hatua tatu za mradi huu ambapo tulishapata eneo la ukubwa wa hekta 2,071. Tulishafanya tathmini ya fidia ambayo ni takribani bilioni 3.3 na tumeshakamilisha tathmini kwa ajili ya kuanza ujenzi. Kazi zinazoendelea sasa hivi kwenye *LNG* ni kukamilisha majadiliano ambayo yatakamilika Septemba 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii nimwombe sana Mheshimiwa Mbunge mwenzangu, Mheshimiwa Nape tuwahamasishe wananchi wa maeneo yote ya Mtwara na Lindi uwekezaji wa *LNG* bado uko pale pale na mwaka huu wa fedha tumeomba bilioni 6.5 Waheshimiwa Wabunge mkiidhinisha mradi utatekelezeka vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaombe wananchi wa Mtwara na wananchi wengine waendelee kwenda kuwekeza Lindi na Mtwara kwa sababu mradi huu bado uko pale pale na utakamilika ndani ya wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nichukue nafasi hii kusema kwamba mradi huu utaanza kujengwa ndani ya miaka mitano na ukikamilika manufaa yake yataanza ...

**NAIBU SPIKA:** Shukrani sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Ikupa Stella Alex atafuatiwa na Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Mheshimiwa Jenista Mhagama ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote, napenda nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipatia kibali cha kuweza tena kuzungumza ndani ya Bunge lako Tukufu na ikiwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia hoja ya bajeti ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ambavyo imewasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye ndiye Waziri wangu na dada yangu mpendwa kwa miongozo ambayo wameendelea kunipatia ambayo inaniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kila siku nikiwa kama Naibu Waziri ninayeshughulikia masuala ya watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo naomba pia nimshukuru sana Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Naibu Waziri mwenzangu. Kiukweli ushirikiano anaonipatia unaniwezesha kutekeleza majukumu yangu kila iitwapo leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niende moja kwa moja kuchangia hotuba hii na sana sana nitajikita katika kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge lakini ufafanuzi mwingine utatolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri mwenzangu pamoja na Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna hoja ya uanzishwaji wa Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu. Uanzishwaji wa mfuko huu ni hitaji la kisheria, Sheria Na.9 ya mwaka 2010 inaeleza wazi kwamba ni lazima kuwe na Mfuko ambao unashughulikia maendeleo ya watu wenye ulemavu. Mfuko huu una faida nyingi ikiwa ni pamoja na kusaidia kufanya tafiti za watu wenye ulemavu, lakini pia elimu ya watu wenye ulemavu pamoja na mafunzo yaani *vocational training* kwa watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vya fedha vya Mfuko huu ni pamoja na fedha ambayo inatengwa na Bunge lako Tukufu, lakini pia fedha ambayo inatokana na wadau mbalimbali. Serikali yetu sikivu inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli mwaka huu wa fedha tayari imekwishatenga fedha ambazo zitasaidia sana katika uanzishwaji wa huu Mfuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara taratibu zitakapokamilika za kuanzishwa kwa huu Mfuko utazinduliwa rasmi. Nitoe rai kwa wadau mbalimbali wa masuala ya watu wenye ulemavu kwamba Mfuko huu utakapokamilika kuanzishwa basi wajitokeze kuuchangia kwa sababu chanzo kimojawapo cha fedha za huu Mfuko ni wadau mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ilijitokeza pia hoja kwamba tunapoelekea kwenye uchumi wa viwanda basi Serikali ihakikishe inajali kundi la watu wenye ulemavu kuona kwamba wanapatiwa ajira. Pia hili ni takwa la kisheria. Sheria Na.9 ya mwaka 2010 kifungu cha 31 kinaeleza wazi kwamba

waajiri wanatakiwa kuajiri watu wenye ulemavu yaani mwajiri ambaye anakuwa na waajiriwa kuanzia 20 na kuendelea basi ahakikishe kwamba asilimia tatu inakuwa ni watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi niseme tu kama Serikali imepokea ushauri huu na itaendelea kusimamia sheria hii kuona kwamba waajiri wanaajiri watu wenye ulemavu kwenye viwanda vyao ili na wao waweze kufaidi keki yetu ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, nitoe rai sana kwa waanzishaji wa viwanda kwamba wazingatie miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu. Tunaposema miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu hatumaanishi tu kwamba zile *ramp* maana yake tukisema miundombinu watu wanafikiria kwamba inakuwa tu ni *ramp*. Unapokuwa umeanzisha kiwanda chako na uka-*install* zile mashine zako kwa jinsi ambavyo mtu mwenye ulemavu hawezi kuzitumia tayari umeshamwekea kikwazo. Kwa hiyo, niombe sana waanzishaji wa hivi viwanda wazingatie miundombinu ambayo itakuwa ni rafiki ili watu wenye ulemavu waweze kuajiriwa katika viwanda vyao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ambavyo tumesikia kwenye hotuba yake imeanzisha kanzidata ambayo itakuwa inajumuisha wale wahitimu wote wenye ulemavu ambao wamehitimu kutoka kwenye vyuo mbalimbali. Kanzidata hii itasaidia sana kuweka mfumo rahisi kwa watu wenye ulemavu kuweza kuajiriwa na kupata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inaendesha Programu ya Kukuza na Kurasimisha Ujuzi na katika programu hii na watu wenye ulemavu pia ni miongoni mwa watu ambao ni wanufaika na wataendelea kunufaika. Kupitia programu hii watu wenye ulemavu wataweza kukuziwa ujuzi wao na kurasimishiwa ujuzi ambao utawawezesha kujiajiri na kuajiriwa maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa kuna hoja ya uboreshaji wa vyuo vya watu wenye ulemavu. Hivi vyuo ni vile vyuo ambavyo vinatoa mafunzo kwa watu wenye ulemavu, Serikali imeendelea kuviboresha vyuo hivi. Kama tunavyofahamu kwamba vyuo vilikuwa vingi na kama vinne hivi bado havifanyi kazi, lakini Serikali imejikita kuhakikisha kwamba Chuo cha Yombo na Singida kinapewa miundombinu ambayo inakuwa ni rafiki kwa kukarabatiwa kupitia Serikali yenyewe kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukarabati unaendelea kufanyika lakini pia Serikali inahakikisha kwamba vyuo hivi vinakuwa na vifaa ambavyo vinatakiwa, vifaa saidizi, vifaa vya kujifunzia na kufundishia ili sasa iwe rahisi kwa watu wenye ulemavu kuweza kupata mafunzo stahiki sambamba na mahitaji yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niongelee hoja ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge ya upungufu wa Walimu, walezi, wapishi pamoja na walinzi kwenye shule zetu za watoto wenye ulemavu. Nikiri wazi kama Serikali kwamba ni kweli tatizo hili lipo ama upungufu huu upo. Hata hivyo, Serikali yetu sikivu tayari Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Ofisi ya Mheshimiwa Rais – TAMISEMI ilishafanya kikao Januari, 2018 ambapo tulijadili changamoto nyingi ambazo zinawakabili watu wenye ulemavu ikiwemo changamoto hii ambayo imezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba changamoto hii imechukuliwa na inafanyiwa kazi na Serikali yetu sikivu. Kutokana na ukubwa wa tatizo si kama hili tatizo litakuwa *solved* kwa muda mfupi, lakini Serikali yetu tayari imeshaanza kulifanyia kazi kuona kwamba hawa walimu, wapishi pamoja na walezi na walinzi basi wanaweza kupatikana katika haya maeneo ambayo yameainishwa kwa maana ya shule za watoto wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa pia kuna hoja kwamba Serikali sasa ilete sheria kwa sababu matamko yamekuwa ni mengi kwa ile asilimia 10. Niseme kwamba ushauri huu Serikali imeupokea na itaufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa kuna hoja kwamba vifaa saidizi kwa watu wenye ulemavu viendelee kutolewa maeneo mbalimbali ikiwemo maeneo ya vijijini kwa sababu maeneo ya vijijini yameonesha kwamba yana uhitaji mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba Serikali yetu sikivu imelichukua hili na itaendelea kusambaza vifaa hivi kama ambavyo tumeona katika shule mbalimbali ikiwemo shule za vijijini vifaa hivi vimeendelea kusambazwa kwa wanafunzi. Pia nafasi inapopatikana tumeona kwamba vifaa hivi vimekuwa vikitolewa hata kwa watu wenye ulemavu ambao pia siyo wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee pia pendekezo kwamba *VETA* itoe kipaumbele kwa watu wenye ulemavu kwa ajili ya kupata zile stadi za mafunzo. Niseme kwamba kama Serikali tumelichukua pendekezo hili na tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na hoja kwamba kuna idadi kubwa ya watu wenye ulemavu ambao wanakaa vijijini, hivyo Serikali iangalie jinsi gani ya kuwawezesha kwa kuwatengea fedha. Hilo kama Serikali pia tumelichukua kama ushauri na tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kwa hoja ambazo nilikuwa nazo nimeweza kuzikamilisha na niseme kwamba naunga mkono hoja iliyopo mbele yetu ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ambavyo imewasilishwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ikupa. Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, tutamalizia na Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kukushukuru kwa nafasi. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima na afya Waheshimiwa Wabunge wote. Pia nichukue fursa hii kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu ili kuchangia hoja ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa Naibu Waziri ninayeshughulikia masuala ya kazi, vijana na ajira, naomba nitumie fursa hii kwanza kabisa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli; Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan; Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa; Waziri wangu Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa ushirikiano na miongozo ambayo wamekuwa wakinipa kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu lakini pia nisimsahau Mheshimiwa Naibu Stella Ikupa kwa ushirikiano anaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Dodoma Mjini nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa azma yake ya kutekeleza kwa vitendo Serikali kuhamia Dodoma ambako hivi sasa tumeshuhudia maendeleo mengi sana katika Jimbo la Dodoma Mjini ambayo yanatokana na uamuzi huo mkubwa wa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kutokana na uamuzi huo wa Mheshimiwa Rais, kwa sababu asilimia kubwa hapa ya Waheshimiwa Wabunge mnaishi Dodoma na mimi ni Mbunge wenu kwa namna moja ama nyingine, nataka tu nitoe ufafanuzi katika baadhi ya mambo ambayo mmekuwa mkikutana nayo huko mtaani mojawapo ikiwa ni katika zile barabara ambazo zinawaletea tabu kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ujio huu wa makao makuu hapa Dodoma tayari hata wahisani wenyewe

wameanza kuona namna ya kuboresha mji wetu. Tumepata fedha za ziada na hivi sasa kuanzia Julai barabara nyingi sana za kwetu zitakuwa na lami. Pia tuna mradi mkubwa wa *Storm Water Drainage* katika eneo la Ilazo ambalo limekuwa kikwazo kikubwa sana kwa watu kufika kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kutokana na azma hii ya Serikali Dodoma sasa inakwenda kujengwa soko kubwa la kisasa ambalo litakuwa ni kubwa na lenye ubora kuliko mengi sana Afrika Mashariki na Kati. Vilevile tunakwenda kujenga stendi kubwa ya kisasa ambayo itakuwa ina maegesho ya zaidi magari 600 kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia utakwenda kujengwa uwanja mkubwa wa kimataifa wa mpira wa miguu ambao utatoa fursa nyingi katika Jimbo letu la Dodoma Mjini. Haya yote yanatokana na kazi kubwa ambayo imefanywa na Mheshimiwa Rais ya kuhamishia Dodoma kama sehemu ya makao makuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo kama maneno ya utangulizi, kwa heshima na taadhima naomba sasa nijibu hoja ambazo zimewasilishwa na Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wakichangia katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza kubwa lililojitokeza hapa ni kuhusiana na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ambapo Waheshimiwa Wabunge wamechangia kwa kuiomba Serikali kuhakikisha kwamba elimu ya kutosha inatolewa kwa wafanyakazi na waajiri na kuhakikisha kwamba sheria hii inazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi umeanzishwa kwa mujibu wa sheria ya mwaka 2008 ambayo lengo lake ni kuhakikisha kwamba wale wafanyakazi wote wanaopata matatizo yanayotokana na kazi zao waweze kufidiwa na mfuko huo. Sheria hii ilipita

hapa Bungeni na ndani ya sheria imetaka waajiri wote nchini wajisajili katika Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ili mfanyakazi yeyote anayepata matatizo akiwa kazini, mwajiri tumuachie kazi yake ya kimsingi ya shughuli anayoifanya na kazi ya kumhudumia mfanyakazi aliyeumia ifanywe na Mfuko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii ilitungwa hapa na kuwataka waajiri wote wajisajili na kabla ya kuanza kufuatilia waajiri wangapi wamejisajili, Mfuko ulifanya kazi ya kutoa elimu ya kutosha kwa kwenda katika kanda mbalimbali kuwaelimisha waajiri juu ya umuhimu wa huu Mfuko. Baadaye Mheshimiwa Waziri wa Nchi alitoa maelekezo kwamba sasa ufanyike utaratibu kuhakikisha kwamba waajiri wote wanasajiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hiyo imefanyika na hata baada ya kikao cha juzi cha Baraza la Biashara la Taifa ambalo lilikuwa chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Rais, maelekezo yalitoka kwamba zile kero ndogo ndogo ambazo zinawakabili waajiri Serikali tukae nao na tuweze kutafuta namna nzuri ya kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba tayari sisi katika Ofisi ya Waziri Mkuu maelekezo hayo tumeshayafanyia kazi na elimu inaendelea katika baadhi ya kanda tunakutana na waajiri ili kuwaambia umuhimu wa Mfuko huu wa Fidia kwa Wafanyakazi ambao ni mkombozi kwa wafanyakazi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojitokeza katika michango ya Wabunge ni kwamba tuhakikishe wafanyakazi wetu wengi wanaofanya kazi katika maeneo mbalimbali ya viwanda na maeneo mengine wanapatiwa vifaa kinga kwa mujibu wa sheria. Sisi kama Wizara kupitia Wakala wa Afya na Usalama Pahala pa Kazi *(OSHA),* tumekuwa tukifanya kaguzi mbalimbali kuhakikisha kwamba wafanyakazi wote wanapatiwa vifaa kinga ili itusaidie pia kuwakinga na madhara mbalimbali ambayo yanatokana

na kazi na mwisho wa siku kumfanya mfanyakazi wa Kitanzania afanye kazi katika mazingira ambayo ni rafiki na kulinda na afya yake pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii inafanyika na niwashukuru sana na kuwapongeza *OSHA* kwa kufanya kazi hii kwa weledi mkubwa. Naamini kabisa kwamba tutaendelea kufanya kazi hii ya ukaguzi ili kulinda nguvu kazi ya Taifa hili isipate madhara au maonjwa kutokana na kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ilizungumzwa hoja na Waheshimiwa Wabunge hapa ya kuitaka Serikali kuboresha kilimo ili kuongeza ajira kwa vijana na vilevile kuwapatia mikopo washiriki katika shughuli za kilimo. Sisi kama Wizara tuliona kwamba ni kweli, ukisoma katika tafiti ya *Integrated Labour Force Survey* ya mwaka 2014 inazungumza kuhusu idadi kubwa ya vijana wanaoshiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu sana shughuli ya kilimo haikuwa inapewa kipaumbele sana kwa miaka ya nyuma. Sisi kama Serikali tukaona kwamba moja kati ya eneo ambalo linaweza likaajiri vijana wengi kwa wakati mmoja ni katika kilimo hasa kilimo biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulianza kwanza kwa kujaribu kubadilisha mitizamo *(mindset)* ya vijana juu ya suala zima la kilimo. Asilimia kubwa ya vijana walikuwa wanachukulia kilimo kama ni shughuli ya kufanya baada ya kukosa shughuli ya kufanya ni kama ni *last resort.* Kwa hiyo, sisi kama Wizara tukaitafsiri tukasema kwamba kwa mujibu wa Sera yetu ya Ajira inasema ajira ni shughuli yoyote halali inayompatia mtu kipato ikiwemo kilimo. Kwa hiyo, tukaanza kuhamasisha vijana kushiriki katika kilimo. Hii tunaifanya pamoja na Wizara ya Kilimo tukiwa tuna mpango mkakati wa kitaifa wa kuwahusisha vijana katika kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao vijana wa kwanza wa mfano ambao tumekuwa tukiwatumia ambao ni vijana waliotoka Chuo Kikuu cha Sokoine wanaoitwa *SUGECO.* Vijana hawa wali-*graduate* Chuo Kikuu cha Sokoine wakaziweka *degree* zao pembeni kwa kile walichokisomea, wakakaa sawasawa katika kilimo, leo hivi navyozungumza wale vijana wanatoa mafunzo kwa vijana wenzao lakini vilevile kilimo hiki sasa kimewafanya wasifikirie ajira nyingine. Hivi ninavyozungumza wameingia kwenye mipango mikubwa ya kidunia ikiwemo mpango wa Bill and Melinda Gates ambao kwa nchi za Afrika ni Tanzania na Nigeria tu ndiyo tumepata nafasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia sisi kama Ofisi ya Waziri Mkuu, katika mpango wa kukuza ujuzi wa miaka mitano wenye lengo la kuwafikia vijana takribani milioni 4.4, moja ya programu tuliyonayo ni Programu ya Kitalu Shamba. Katika mwaka ujao wa fedha tumeshaagiza mamlaka za mikoa waombe kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu maombi ya vitalu shamba, tutawafundisha vijana wa Kitanzania kutengeneza vitalu shamba na tutatoa vitalu shamba ili wafanye kilimo biashara cha kisasa. Lengo ni kuhakikisha kwamba vijana wengi zaidi wanafanya shughuli ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia kupitia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, pale Morogoro tuna shamba la miwa la Mkulazi kwenye kiwanda cha sukari, asilimia kubwa ya tuliowachukua kushiriki katika uchumi ule ni vijana ambao ndiyo *out growers* na pale kuna hekari 63,000. Vijana wa Morogoro na maeneo ya karibu watapata fursa kushiriki katika uchumi huu wa viwanda*. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ilijitokeza hoja nyingine hapa kwamba Serikali ihakikishe ajira hizi katika miradi hii mikubwa kama ya bomba la mafuta, mradi wa reli huu mkubwa inawagusa na kuwanufaisha Watanzania. Sisi kama Ofisi ya Waziri Mkuu tuliliona jambo hili, tulichokifanya awali ni kuhakikisha kwamba wataalam wetu wanakaa na kuona ni nafasi na ujuzi gani unaohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshafanya *coordination* ndani na hivi sasa ninavyozungumza Wakala wetu wa Huduma za Ajira anafanya kazi hiyo kuhakikisha kwamba Watanzania wengi zaidi hasa vijana wanapata fursa ya kushiriki katika uchumi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano katika hili bomba la mafuta, mpaka hivi sasa maombi ya vijana yaliyokuja ni takribani 23,650 ambapo uhakiki unaendelea ili kuwa-*link* na zile fursa. Lengo letu vijana wengi zaidi wapate nafasi za ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ilijitokeza hoja moja hapa ya kwamba Mfuko wa Maendeleo ya Vijana unatoa mikopo kwa ubaguzi wa itikadi ya vyama vya siasa. Naomba niliweke hili sawasawa, Mfuko wa Maendeleo wa Vijana *(YDF)* upo kwa mujibu wa sheria na una mwongozo wa nani anatakiwa kupewa mkopo akikidhi masharti gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mle hakuna sharti linalosema uambatanishe na kadi yako ya chama za siasa, hakuna. Sharti ni kwamba lazima kila Halmashauri iunde *SACCOS* ya vijana ndiyo itakopesha vikundi katika eneo husika. Kwa hiyo, niondoe hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba mikopo hii ni kwa ajili ya vijana wote wa Kitanzania wanaokidhi masharti ya mwongozo ambao umewekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ilijitokeza pia hoja ya Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA)* ambapo Wabunge wali-*raise concern* tu kwamba yale maeneo yao wanayotumia *especially* kule Dar es Salaam hawana vyumba vya kutosha na wanafanya kazi katika mazingira magumu. Nichukue fursa hii kulitangazia Bunge lako Tukufu kwamba tumefanya mawasiliano na zile Wizara ambazo zinatoka kule Dar es Salaam ambazo zimeacha Ofisi wazi, hivi sasa Tume hii ipo katika hatua za mwisho za kupata majengo mengine ambayo yatawafanya wafanye kazi kwa uhuru na ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya mwisho ni kuhusu Nembo ya Taifa na ilisemwa kwamba nembo ile jinsi ilivyo haiakisi mazingira ya Tanzania na kwamba mtu akiiona anaweza akapata picha tofauti kwa sababu kuna mwanamke anaonekana pale ana kama nywele ambazo sio za Kitanzania kwa maana ya *wig.* Naomba niliweke wazi tu kabisa suala hili, Nembo ya Taifa imeanzishwa kwa mujibu wa *National Emblems Act,* Sura ya 10 na ukiangalia siyo kweli kwamba haiakisi mazingira yetu kama inavyoonekana hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nembo hii ni moja kati ya alama za Taifa na ukiangalia hapo, huyo anayeonekana kama kavaa *wig,* kile ni kilemba cha kuonesha kwamba huyu ni mwanamke wa Kitanzania na ndiyo mazingira yetu. Pia kuna Mlima Kilimanjaro ambao upo peke yake Tanzania, hakuna mlima mwingine wowote Afrika na duniani, hicho ni kielelezo kingine pekee. Pia kuna mawimbi pale kuonesha bahari, mito na maziwa yetu lakini pale chini ukiwaangalia wamekanyaga karafuu na pamba kuonyesha kwamba haya ni mazao makuu yaliyopo katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaondolee hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba siyo kweli nembo hii haiakisi mazingira ya Taifa letu la Tanzania. Ukiona yenyewe inasema jinsi ilivyo, wanasheria wana lugha moja wanasema *res ipsa loquitur,* kwamba mambo yanaongea yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema haya sasa, naomba nitamke rasmi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mavunde. Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu

Spika, nadhani nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuweza kutufikisha siku hii ya leo ambapo tunapata nafasi ya kuhitimisha hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya bajeti ya Ofisi yake lakini vilevile na Mfuko wa Bunge kwa bajeti ya mwaka 2018/2019 na baada ya kupitia pia utendaji kazi wa Serikali katika ofisi hii kwa mwaka wa fedha uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nasema hivyo kwa sababu Watanzania wamempambanua Mheshimiwa Rais wetu kama kiongozi mahiri, imara, shupavu na ni mzalendo wa kweli kabisa ambaye amedhamiria kusimamia maendeleo ya nchi yetu na kufanya mageuzi ya kisasa katika kuleta maendeleo ya Taifa la Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja naye nimpongeze sana Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na vilevile nimpongeze sana Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Ally Mohamed Shein. Hawa wote wanafanya kazi nzuri sana katika kujenga Taifa letu, kudumisha Muungano na kuhakikisha kwamba misingi iliyojengwa na Waasisi wa Taifa hili inaendelea kufuatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi ya pekee nimshukuru sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo na maelekezo ambayo amekuwa akinipatia mimi pamoja na watendaji wote wa Ofisi yake ili kuhakikisha kwamba tunachapa kazi na tunatekeleza maagizo ambayo tumekuwa tukiyapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakubaliana nami kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu ni mchapa kazi na kiongozi mahiri na hiyo ameweza kujipambanua kabisa katika shughuli zake za Serikali ndani na nje ya Bunge. Tumwombee kwa Mwenyezi Mungu ili aendelee kumjalia afya njema ya kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwapongeza hao niliowasema lakini kwa dhati nimpongeze sana Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde na Mheshimiwa Stella Alex Ikupa, Naibu Mawaziri katika Ofisi yangu. Hawa wamekuwa ni wasaidizi wangu wa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niwashukuru sana Bi. Maimuna Tarishi, Bw. Erick Shitindi, Profesa Faustine Kamuzora pamoja na Wakuu wa Taasisi zote, Wakurugenzi na wafanyakazi wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa jinsi ambavyo tumepeana ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa sina fadhila kama sitamshukuru Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Naibu Spika, Katibu wa Bunge, wafanyakazi wote wa Bunge na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri ambazo wamekuwa wakizifanya katika Bunge hili na hasa kutusaidia sisi Ofisi ya Waziri Mkuu kama waratibu wa shughuli za Bunge kuweza kutekeleza majukumu ya Serikali ipasavyo ndani ya Bunge lako. Shukrani zangu za dhati pia ziwaendee Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge ndani ya Bunge letu na Wabunge wote kwa ujumla kwa kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee niwashukuru sana Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo ndugu yangu Mheshimiwa Jitu Soni pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, ndugu yangu Mheshimiwa Mchengerwa na dada yangu Mheshimiwa Najma Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya UKIMWI ndugu yangu Mheshimiwa Oscar na Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Dkt. Tisekwa na wajumbe wote kwa jinsi ambavyo wametusaidia sana kutekeleza majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee niwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Peramiho

kwa kuendelea kuniamini, kuniunga mkono na kunipa ushirikiano mkubwa kutekeleza majukumu katika Jimbo letu na tunaona na kushuhudia maendeleo makubwa ya Jimbo la Peramiho. Naendelea kuwaeleza kwamba tupo pamoja na hasa kutekeleza kwa vitendo kaulimbiu ya Hapa Kazi Tu Hakuna Kulala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijielekeze katika hoja ambazo zimebakia, lakini kwa muda muafaka Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuja kujibu hoja nyingine ili kuhitimisha hotuba yake. Hoja nitakazoanza kuzijibu ni hoja zinazomhusu Msajili wa Vyama vya Siasa na Ofisi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza ilikuwa ni Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ifanye jitihada za kutosha kusuluhisha mgogoro katika Chama cha Wananchi *(CUF)* ili kuepusha athari zinazoweza kujitokeza katika Muungano na katika mgogoro huo. Naomba nichukue nafasi hii kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kwamba mgogoro huu wa Chama cha *CUF* kwa sasa upo Mahakamani, kwa hiyo sitachukua nafasi hii kuujibu mgogoro huo ama kumuagiza Msajili wa Vyama kushughulika na mgogoro huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa ninachotaka kusema hapa ni hiki kifuatacho. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Msajili wa Vyama vya Siasa kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya siku zote wakati akiratibu na akitekeleza majukumu yake kama Msajili wa Vyama vya Siasa. Amekuwa akifanya kazi nzuri sana na sisi wote ni mashahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Msajili wa Vyama vya Siasa anafanya kazi hii kwa kuzingatia Sheria Na. 5 ya Vyama Vya Siasa ambayo ndiyo inayosimamia vyama vya siasa katika nchi yetu ya Tanzania. Sisi wote tumekuwa ni mashahidi, Msajili wa Vyama vya Siasa mpaka sasa amefanikiwa kusajili vyama vya siasa 19 ndani ya nchi yetu ya Tanzania ambavyo vimepata usajili wa kudumu lakini Msajili wa Vyama vya Siasa

ameendelea kusimamia utekelezaji wa sheria na kanuni mbalimbali za vyama vya siasa katika nchi yetu ya Tanzania kwa weledi mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo naomba tu niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Msajili wa Vyama vya Siasa pamoja na kutakiwa kusuluhisha migogoro hiyo ambayo nimeisema katika Chama cha Wananchi *CUF,* naomba niwashauri wenzetu wanaohusika na mgogoro ndani ya chama cha siasa cha *CUF,* ili mgogoro huu Mheshimiwa Msajili wa Vyama vya Siasa aweze kuushughulikia vizuri, uko utaratibu wa kisheria na Mwanasheria Mkuu wa Serikali anajua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunamtaka Msajili wa Vyama awe *mediator* katika mgogoro huo basi niwashawishi na kuwaomba waondoe mgogoro huu katika Mahakama ulikopelekwa mgogoro huo na Msajili wa Vyama anaweza akafanya kazi yake. Vinginevyo Msajili wa Vyama hawezi kuingia katika mgogoro huu kwa sababu mgogoro huo tayari umeshasajiliwa na upo katika Mahakama zetu na hivyo tumwache Msajili wa Vyama aendelee na shughuli nyingine ambazo hafungwi nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee na hoja nyingine. Waheshimiwa Wabunge na hasa Wabunge wa Upinzani wamelalamika sana na kusema kwamba suala la maandamano ni suala la Kikatiba na wamesema kwa sababu suala la maandamano ni haki ya Kikatiba wanafikiri upo msingi wa vyama vya siasa kuachiwa waendelee na maandamano bila kuzingatia sheria, hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba suala la maandamano katika nchi yetu ya Tanzania linaratibiwa na sheria za usalama ndani ya nchi yetu chini ya vyombo vya usalama na hasa polisi na Katiba haiwezi kuchukuliwa kwamba ndicho kigezo cha kuviruhusu vyama kufanya maandamano bila kuzingatia taratibu na sheria zilizowekwa. Naomba sana kwa heshima yote niwaombe

Watanzania wote, niviombe vyama vyote vya siasa katika nchi yetu ya Tanzania wahakikishe wanazingatia sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba yetu imeruhusu maandamano lakini maandamano yameratibiwa kisheria na kama yameratibiwa kisheria ni lazima tuhakikishe kwamba tunazingatia sheria katika kuratibu maandamano kwenye nchi yetu. Labda niulize kitu kimoja, tukiamka hapa siku moja asubuhi na kila mtu ameamua kuandamana; wakulima au wafanyakazi au kila mtu aamue tu kuandamana kwa sababu Katiba imesema, nadhani itakuwa siyo sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuviomba vyama vyote katika nchi yetu kuheshimu Katiba na sheria katika kutekeleza wajibu wao na siyo kuvunja sheria za nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo ilikuwa imetolewa na Waheshimiwa Wabunge ni kwamba chaguzi ndogo ambazo zimekuwa zikiendelea kwa sasa, zimekuwa zikigharimu sana fedha za Serikali. Baadhi ya Wabunge wakajaribu kulinganisha pia gharama ambazo zimekuwa zikitumika katika chaguzi hizi ndogo na utekelezaji wa majukumu ya Serikali na miradi mingine ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme demokrasia ni gharama. Hakuna demokrasia yoyote mahali popote ambayo haina gharama yoyote. Nasema hivi kwa sababu kama Jimbo la Uchaguzi kwa mujibu wa sheria na Katiba yetu liko wazi, hakuna jinsi, ni lazima tufanye uchaguzi. Kama ni Jimbo la Uchaguzi la Ubunge ama la Udiwani ni lazima kwa mujibu wa sheria na Katiba apatikane mwakilishi wa kuwawakilisha wale wananchi kwenye jimbo husika. Hatuwezi kufanya uchaguzi bila kutumia gharama, kwa hiyo, hiyo ni demokrasia ndiyo maana nasema ni gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, niseme neno moja, nina mfano tu mdogo. Jimbo la Songea Mjini baada ya kuwa wazi na uchaguzi kufanyika, Mbunge ambaye sasa hivi anawakilisha Jimbo la Songea Mjini, ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, ameniambia kwa muda huu mfupi kwa sababu nafasi iliyokuwa wazi imejazwa ameweza kufanikiwa kupata fedha za Kitanzania zisizopungua bilioni sita kwa ajili ya ujenzi wa barabara na miundombinu ya stendi katika jimbo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, gharama tulizozitumia kwenye uchaguzi ni bilioni nne, lakini zimewawezesha wananchi wa Jimbo la Songea kupata bilioni sita kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Kwa hiyo, naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba ni ukweli usiopingika kwamba demokrasia ni gharama na kama demokrasia ni gharama ni lazima tuendelee kufanya uchaguzi kujaza nafasi wazi kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo hoja nyingine iliyozungumzwa, imesema kwamba kuna kila dalili ya Msajili wa Vyama kukusudia kuua Upinzani katika nchi yetu ya Tanzania. Naomba niseme yafuatayo:-

Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Ali Hassan Mwinyi, mwaka 1991 alimteua Jaji Nyalali kukusanya maoni ya Watanzania kuamua kama nchi yetu iende katika mfumo wa vyama vingi au ibaki katika mfumo wa chama kimoja. Watanzania asilimia 80 walisema hawataki mfumo wa vyama vingi, Watanzania asilimia 20 walisema wanataka mfumo wa vyama vingi, lakini ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi iliyofanya maamuzi magumu tuingie katika mfumo wa vyama vingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu za kuingia katika mfumo wa vyama vingi zilikuwa wazi tu, ni kuwafanya Watanzania waone kwanza Chama cha Mapinduzi hakiogopi mageuzi na hakiogopi mfumo wa vyama vingi.

Vilevile ilikuwa ni kuhakikisha kwamba demokrasia ya wachache waliochagua mfumo wa vyama vingi inaheshimiwa na wengi waliokataa mfumo wa vyama vingi. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya niliyoyasema inajidhihirisha kabisa kwamba Serikali ya chama chetu ilifanya maamuzi ya kuingia katika Mfumo wa Vyama Vingi ili kufuata demokrasia, kwa hiyo hakuna sheria yoyote inayomruhusu Msajili wa Vyama kuvunja demokrasia na kufuta Mfumo wa Vyama Vingi katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Msajili wa Vyama aendelee kuchukua hatua stahiki kama Kamati ya Bunge ilivyotushauri kwa vyama vyote ambavyo havitaki kufanya shughuli zake kwa kufuata sheria na taratibu tulizoweka ili kusaidia Mfumo wa Vyama Vingi katika nchi yetu uweze kuwa ni mfumo halisia ambao unaendana na matakwa ya kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nizungumze machache kuhusu Tume ya Uchaguzi. Kwenye Tume ya Uchaguzi imetokea hoja kwamba Tume hiyo imekuwa haina weledi, haizingatii sheria na taratibu katika kuendesha shughuli za uchaguzi na wakati mwingine imekuwa pia ikisimamia uchaguzi huo bila kuzingatia sheria na taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi Tanzania. Tume ya Uchaguzi imeanza kufanya kazi ya kusimamia uchaguzi mwaka 1995 tulipoingia katika mfumo wa vyama vingi. Mwaka 1995 tumemaliza uchaguzi salama na Serikali imeingia madarakani na tumeendelea kufanya kazi. Vilevile mwaka 2000, 2005, 2010, 2015, Tume hii ya Uchaguzi ndiyo

imesimamia uchaguzi wetu na hata sisi Wabunge ambao tuko ndani ya Bunge lako Tukufu tumesimamiwa uchaguzi wetu na Tume hiyohiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kushangaa sisi tuliposhinda, Tume hii ya Uchaguzi ilikuwa imefanya vizuri, hatukusema lolote na hatukuwa na malalamiko yoyote lakini leo tunasimama na kusema Tume hii haina weledi na haifuati utaratibu wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukuhakikishia sisi kama Serikali tumeendelea kuisimamia na kuiratibu Tume ya Uchaguzi kwa kuzingatia Katiba kwa sababu Katiba inasema wazi Tume ya Uchaguzi ni huru na inafanya kazi zake kwa uhuru ulio kamili.

**MBUNGE FULANI:** Hamna.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa Katiba pale ambapo uchaguzi umekwishafanyika na kama chama chochote kinaona kwamba misingi ya kisheria haijafuatwa, chama hicho kimeruhusiwa kwenda mahakamani na kule mahakamani ndipo kutakapopatikana haki ya kisheria kwa chama chochote kinacholalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niliarifu Bunge lako Tukufu, kwa chaguzi hizi ndogo zote zilizopita kesi zilizofunguliwa kwenye kata hizo takribani kama arobaini na kitu mpaka 50, kesi za uchaguzi zimefunguliwa kwa kata mbili tu. Kwa hiyo, naomba tuone kama kweli Tume hii ilikuwa haisimamii uchaguzi huo kwa haki naamini kabisa kata nyingi kesi za uchaguzi zingekuwa zimefunguliwa. Kwa majimbo yote ambayo Tume ya Uchaguzi imeshaendesha uchaguzi hakuna jimbo hata moja ina kesi ya kupinga uchaguzi katika jimbo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niseme kwamba Tume hii ya Uchaguzi inafuata utaratibu katika

uendeshaji wa shughuli zake na kama mtu yeyote, chama chochote kina malalamiko naomba sana kifuate sheria na kiende Mahakamani. Niviombe vyama vyetu vya siasa visikimbilie kulalamika kwenye vyombo vya habari, ni vyema vyama vya siasa vizingatie sheria za nchi tulizonazo katika kuendesha chaguzi zetu tunazoendelea nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine kwa Tume hii ya Uchaguzi ilikuwa ni kuhakikisha kwamba tunaboresha daftari la wapigakura kwa wakati. Naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba shughuli ya kuboresha daftari la wapigakura tumeshaianza ndani ya Serikali kwa mujibu wa sheria na taratibu tulizonazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshaanza kuhuisha kanzidata ya daftari la wapigakura katika nchi yetu ya Tanzania, tumeshaanza kutoa elimu na tumeshaanza kufanya shughuli zote ambazo zinatakiwa ili daftari la wapigakura katika nchi yetu liwe limeboreshwa na liendane na wakati kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliambiwa pia tuhakikishe kadiri iwezekanavyo watendaji wote wa Tume ya Uchaguzi ambao watakiuka maadili ya kisheria kama watendaji ndani ya Tume basi wachukuliwe hatua na ikiwezekana wapewe adhabu zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikuhakikishie kazi hiyo inafanyika vizuri wa sababu tunazo sheria, tunayo miongozo na tunazo taratibu ambazo zimewekwa bayana. Kwa hiyo, watendaji wote ambao wataonekana wanakiuka taratibu za kisheria katika kufanya kazi ndani ya Tume yetu ya Uchaguzi basi watachukuliwa hatua stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambazo zilikuwa zimejitokeza zilikuwa zinahusu mapambano dhidi ya UKIMWI katika nchi yetu ya Tanzania. Katika eneo hili mambo yafuatayo yaliongelewa kwa kiasi cha kutosha.

La kwanza, ilikuwa ni bajeti kuendelea kutolewa kwa wakati; la pili ilikuwa ni tozo ndani ya Serikali ili kutunisha Mfuko wa *ATF (AIDS Trust Fund);* la tatu ilikuwa ni kuhakikisha kwamba asilimia 10 ambayo iko kwenye *own source* ambayo inatumika kwa akinamama na vijana inatumika pia kwa ajili ya kuwahudumia wanaoishi na VVU lakini ya nne ilikuwa kuhakikisha kwamba upatikanaji wa dawa kwa ajili ya wenzetu wanaoishi na VVU unaendelea kuwa wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilihakikishie Bunge lako kwamba tumefanya kazi ya kutosha na Wizara zinazohusika. Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa mwaka huu wa fedha imeongezeka. Suala la tozo kwa ajili ya Mfuko wa Kudhibiti UKIMWI katika nchi yetu, tumeshapeleka mapendekezo yetu kwenye Ofisi ya Waziri wa Fedha na tunaamini kabisa wenzetu watatushauri njia gani ya kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwamba mfuko wenyewe kupitia bodi umeshaanza kufanya kazi ya kutosha ya kukusanya fedha ili kuhakikisha kwamba unakuwa na fedha na hiyo ni kujihami na upungufu wa fedha za wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la asilimia 10, naomba mtuachie, tunachukua pendekezo hilo, tutalifanyia kazi kwa pamoja na wenzetu wa TAMISEMI. Tutakuja kutoa majibu tuone kama hiyo asilimia kumi tunaweza tukagawana hiyohiyo ama tunaweza kutumia Mifuko kama *TASAF* ama mifuko mingine kuhakikisha hawa wenzetu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI na wao wanaweza kusaidiwa ili kuweza kukidhi mahitaji yao na kuwafanya waweze kutumia dawa vizuri, lakini kuwasaidia waweze kuendelea kuishi wakiwa na afya njema. Naomba niseme hilo nalichukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lilikuwa ni suala la kuwezesha wananchi kiuchumi. Tuliambiwa kwamba kwenye miradi inayoendelea kwa sasa tujitahidi kuhakikisha kwamba Watanzania wazawa na wao wanapata nafasi za kazi ama wanakuwa ni wakandarasi washiriki katika miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikuhakikishie, kupitia mpango wetu wa *local content* ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu, tumeweza kuanzisha mpango mkakati mahsusi wa kuzungumza ndani ya Serikali kuhusu suala la *local content* kuhakikisha kabisa kwamba Watanzania katika miradi mikubwa ya kitaifa, lakini vilevile katika shughuli zinazoendelea katika halmashauri zetu na wao wanapata nafasi ya kushiriki kama washiriki wa uchumi katika nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka pia tulifanya hata marekebisho ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ambayo inatupelekea kuwafanya Watanzania waweze na wao kuwa ni washiriki kwenye suala zima la maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya sekta ya hifadhi ya jamii, Waheshimiwa Wabunge wametushauri kwamba tutoe elimu kwa Watanzania kuhusu sekta hii. Naomba kukuhakikishia kwamba kazi hiyo inafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, walitaka tuhakikishe sheria mpya inaanza kutumika kwa haraka kwa kuwa na kanuni zake, naomba niwahakikishie kanuni ziko tayari na zinakamilishwa kwa hatua ya mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Wabunge walituagiza tupanue wigo wa hifadhi ya jamii ifike mpaka kwenye sekta isiyo rasmi. Naomba niwahakikishie kwa mabadiliko ya sheria tuliyoyafanya Bunge lililopita sasa sekta isiyo rasmi inatambulika rasmi katika suala zima la hifadhi ya jamii katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la BAKWATA, kwa nini wamefanya mkutano wao hapa Bungeni. Naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge, Serikali yetu haina dini, Serikali yetu inafanya kazi na taasisi zote za dini bila kujali ni aina gani ya taasisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, wala isiwe tabu kwa BAKWATA kufanya mkutano wao hapa, kama kuna taasisi nyingine inataka kufanya mkutano hapa Bungeni na wao walete maombi ili mradi tu wafuate taratibu na sheria. Vilevile mkutano wanaotaka kuja kuufanya hapa uwe ni mkutano ambao tutakuwa tumejiridhisha kwamba mkutano huo hauna madhara ndani ya Bunge na nje ya Bunge letu la Tanzania. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hakuna haja ya kuhangaika ni kwa sababu gani BAKWATA wamefanya mkutano hapa, ninachosisitiza ni suala la misingi ya kisheria na aina ya mkutano unaotakiwa kufanyika hapa, kama ni vitu ambavyo vinaelezeka na havina madhara kila mtu anaweza akafanya mkutano mahali popote ambapo pana ukumbi. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, suala ambalo pia nataka nilizungumze kwa ufupi ni suala la dawa za kulevya. Nianze kwa kuipongeza Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya katika nchi yetu ya Tanzania kwa kazi nzuri. Imefanya kazi nzuri sana katika maeneo matatu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la *supply* (kudhibiti upatikanaji wa dawa); kwenye suala la *demand* (kudhibiti uhitaji) na katika kupunguza madhara (kwenye masuala ya *harm reduction*). Kwa hiyo, Tume imefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge, tukubaliane hapa kwamba suala la uhalifu katika nchi yetu ya Tanzania si la Muungano na wala suala la Mahakama si suala la Muungano, lakini suala la ulinzi wa Taifa ndilo suala la Muungano katika nchi yetu. Kwa hiyo, mamlaka hii kwa sheria tuliyonayo inafanya kazi upande wetu huku Bara lakini kwa sababu uhalifu hauna mipaka ndiyo maana tunasema ni lazima mamlaka hii ifanye kazi ya kutosha na mamlaka katika upande wa pili wa Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ni hali ya kawaida tu, kama upande mmoja ukifanya kazi, upande mwingine usipofanya kazi ni shida ama pande zote mbili tusipofanya kazi kwa pamoja itakuwa shida. Naomba niwahakikishie sisi wenyewe ndani ya Serikali jambo hili tunalifanyia kazi kwa pamoja pande zote mbili za Muungano kuhakikisha dawa za kulevya katika nchi yetu ya Tanzania zinakoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa nafasi uliyonipa, hoja bado ziko nyingi kiasi, tutazijibu kwa maandishi. Nichukue nafasi hii kuwaomba sana Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla kuendelea kuheshimu sheria na hasa katika kushughulika na shughuli ya vyama vya siasa katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja na nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kujibu hoja ambazo zimewekwa mbele yetu katika siku hii ya leo. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha asubuhi, sasa nachukua fursa hii kusitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11:00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) alikalia kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae, Katibu!

**NDG.STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA**: Hoja za Serikali sasa nichukue fursa hii kumkaribisha mtoa hoja, Mheshimwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu ili uhitimishe hoja yako, karibu sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu na una saa moja. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema hadi leo ninaposimama katika kikao hiki cha sita cha Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge lako hili Tukufu kwa ajili ya kuhitimisha hoja ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Naungana na wenzangu walionitangulia kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameendelea kukupa afya njema na kurudi hapa kuendelea na kazi yako ya kuongoza Bunge hili Tukufu Mungu ni mkubwa na aendelee kukupa afya njema zaidi. *(Makofi)*

Aidha, nikushukuru sana wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kuendelea kusimamia Bunge hili kwa michango iliyotolewa Waheshimiwa Wabunge, majadiliano na hasa hoja ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii pia kuwashukuru Wenyeviti na Wajumbe wote wa Kamati ya

Kudumu ya Katiba na Sheria, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya masuala ya UKIMWI kwa taarifa nzuri walizoziwasilisha maoni na ushauri waliotoa kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa majikumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge.

Vilevile nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa pongezi maoni, ushauri na hoja mbalimbali mlizozitoa wakati wa kuchangia hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwa Serikali hii ya Awamu ya Tano imepokea kwa mikono miwili pongezi zenu na michango yenu ambayo naamini itakuwa chachu ya kuongeza kasi ya utekelezaji wa mipango ya bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa naomba niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wa kisekta kwa maelezo ya ufafanuzi waliyoyatoa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Jenista Johakimu Mhagama (Mbunge) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde (Mbunge) Naibu Waziri wa Kazi Ajira na Vijana na Mheshimiwa Stella Alex Ikupa, (Mbunge) Naibu Waziri watu wenye Ulemavu kwa maelezo mazuri wakati wa kufafanua hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge zilizoelekezwa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie pia fursa hii kuwapongeza sana Makatibu Wakuu wangu Mama Maimuna Tarishi, Profesa Kamuzora na Bwana Eric Shitindi kwa pamoja na Wenyeviti wa Tume wa Uchaguzi, Tume ya *TACAIDS,* Kamishina Jenerali, Madawa ya Kulevya, Msajili wa Vyama vya Siasa, Wakurugenzi wote na watendaji wote walio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi nzuri ya uratibu wa hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge ambazo sasa tumeanza kuzijibu.

Mheshimiwa Spika, katika mjadala huu uliotumia siku tano Waheshimiwa Wabunge 124 walichangia kwa kuzungumza moja kwa moja hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge 50 walichangia kwa njia ya maandishi.

Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote mliochangia hoja yangu, hata hivyo kutokana na muda kutokuwa rafiki sana naomba nisiwataje kwa majina, lakini naomba majina yote ya Waheshimiwa Wabunge yaingizwe katika *Hansard* na ninayo hapa.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchangia hoja Waheshimiwa Wabunge wengi wanakiri na kupongeza mafanikio yaliyopatikana kutokana nautendaji wa Serikali ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo napenda nitumie nafasi hii ya awali kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wa Serikali za Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar kwa kusimamia ipasavyo utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015.

Naendelea kutoa rai kwa viongozi na watendaji kuendelea kuifanyia kazi na kutekeleza kwa dhati falsafa ya Serikali ya Awamu ya Tano inayosema hapa kazi tu. Kwa mantiki hiyo viongozi, watendaji na wawakilishi tunaowajibu mkubwa sana wa kuwatumikia wananchi kwa kuwapokea, kuwasikiliza na kuwahudumia kama namna bora kabisa ya kutekeleza falsafa hiyo ya Mheshimwia Rais na Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pongezi mlizozitoa Waheshimiwa Wabunge kwa hakika si tu zimetutia moyo na kutupa nguvu zaidi ya kusonga mbele, bali pia zinatoa mwelekeo mzuri hususani pale zinapoainisha mafanikio muhimu ya kitaifa na kimataifa ambayo yamepatikana ndani ya kipindi cha takribani miaka miwili na nusu ya utendaji wa Serikali hii ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na michango maoni ushauri napongezi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge naomba uridhie nitoe maelezo ya jumla kwa maeneo

yafuatayo ambayo baadhi yetu walihitaji kujua faida za kwa nini tumetumia fedha kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kwanza ni ule mradi wa usimikaji wa mfumo wa rada. Mnamo tarehe 2 Aprili, 2018 Mheshimiwa Rais alizindua mradi wa usimikaji mfumo wa rada nne kwa ajili ya kuongoza ndege kwenye viwanja vyetu hapa nchini ambavyo ni vinne; uwanja wa Julius Kambarage Nyerere - Dar es Salaam, uwanja wa KIA kule Kilimanjaro, uwanja wa Mwanza na uwanja wa Songwe kule Mkoani Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi hii yote imegharimu jumla ya shilingi bilioni 67.3. Hivi sasa nchi yetu rada moja tu ya kiraia iliyoko kwenye Uwanja wa Ndege wa Dar es Saalam ambayo uwezo wake wa kuona ndege ni asilimia 25 tu ya eneo ambalo linatakiwa kuona ndege. Aidha, uwezo wa rada hiyo ambayo ilinunuliwa mwaka 2002 ili itumike kwa miaka 12 kwa sasa imepungua uwezo wake kutokana na uchakavu ulionayo. Hali hiyo imesababisha baadhi ya mashirika ya ndege nchini kuhairisha kuja Tanzania kwa sababu hayaonwi, hakuna mawasiliano moja kwa moja na mahali petu Dar es Salaam, kwa maana Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mradi huu wa rada ni sehemu ya mipango ya Serikali ya kuimarisha usafiri wa anga nchini na ambao utakuwa na manufaa mwengi kwa Taifa letu. Miongoni mwa manufaa hayo sasa ni kuimarisha usalama wa nchi yetu kwa kuongeza uwezo wa kuhudumia anga yetu kutoka asilimia 25 ya sasa mpaka asilimia100 pindi zitakapokamilika na kuanza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nataka tuanze kurejesha imani na mashirika ya ndege ambayo yaliahirisha kuingia nchini hiyo pia ni jambo muhimu. Lakini nataka turahisishe pia shughuli za kuongoza ndege zinazoingia hapa nchini kwa kuongeza pia mapato ya nchi yetu kutokana na tozo ambazo tutakuwa tunatoza kwa ndege zile kuingia na kuhudumiwa na rada zetu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge hiyo ilikuwa ni faida za kwa nini mradi ule tumeutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi wa pili ni kufufua Shirika la Ndege la Tanzania, ununuzi wa ndege hizi ni mipango ya Serikali ya kufufua shirika letu la ndege ambalo lilishakufa kabisa. Kama tulivyoshuhudia tarehe 2 Aprili, 2018 Mheshimiwa Rais akiongoza wana Dar es Salaam kwa niaba ya Watanzania kupokea ndege yetu ya tatu aina ya Bombardier Dash 8 Q400. Ni mwelekeo wa kulifufua shirika letu ambako sasa Serikali tumenunua ndege sita, ndege tatu zimeshaingia ndege tatu zingine zitaingia ambazo tunataka zitoe huduma ndani na nje ya nchi kwa lengo la kukuza na kama kichocheo cha ujenzi wa uchumi wa viwanda hususani viwanda vya usindikaji wa mazao kama vile matunda, usafirishaji wa maua, mbogamboga, samaki, na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, usafiri imara wa anga na wenye uhakikia utasaidia sana kukuza sekta ya maliasili na utalii. Kama ambavyo mnafahamu Watanzania wote kwamba watalii wengi zaidi ya asilimia 70 wanatumia usafiri wa ndege kuingia nchini na nchi yetu ni miongoni mwa nchi zinazoongoza kuwa na vivutio vingi ambavyo watalii wanavipenda sana. Kwa hiyo, tunataka moja kati ya malengo ni kuongeza idadi ya watalii nchini kutoka watalii milioni 1.3 ya sasa na ikiwezekana kuifikia milioni tano ifikapo mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nataka tuimarishe usafiri wa anga ndani ya nchi na ndiyo sababu sasa tunajenga viwanja vingi vya ndege katika kila mkoa ili kuwezesha ndege zetu kutua kila mkoa na kuweza kusafirisha vile ambao watakuwa wanaweza kusafiri. Lakini pia tunataka tufungue fursa za utalii kwenye mikoa hiyo ili watalii wetu waweze kusafiri kwa ndege wafike kwenye maeneo yetu, tuna vivutio vingi; Kigoma tuna eneo la sokwe ambako sasa wanaanza kufika kwa sababu ndege inakwenda sasa mpaka Kigoma na maeneo mengine mengi ambayo yana vivutio vya aina hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili tunataka tukuze sekta nyingine ambazo zinahitaji usafiri wa ndege sekta ya

kilimo lakini sekta ya mifugo, uvuvi. Lakini pia nataka tuongeze ajira nyingi ili wengine wafanye kazi kwenye shirika letu la ndege kwa kupitia maeneno yote ambayo tuliyonayo. Kwa hiyo, mradi wa ufufuaji wa shirika la ndege ulikuwa na malengo hayo kwa kifupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uko mradi mwingine wa kuanzisha uzalishaji wa umeme kwa wingi hii imetolewa maelezo mazuri sana na Waziri wa Nishati kwa nini tunaanzisha vyanzo vingi vya kuzalisha umeme na vyanzo hivi ni vingi tunataka kwenye maji, kwenye gesi asilia lakini kwenye upepo kwa kutumia hata pia takataka, uko uwekezaji unakuja muda mfupi wa kutumia takataka zetu kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, malengo yetu ni kupata umeme wa kutosha ili sasa uende sambamba na matakwa yetu ya kuboresha viwanda nchini ambavyo vitakuwa vinaendeshwa na umeme. Lakini pamoja na hiyo tunataka pia tuhakikishe kwamba tunasambaza umeme tunapata umeme wa kutosha ili miradi yetu ya usambazaji wa umeme kwenda vijijini tupeleke umeme wa kutosha, umeme wa uhakika na umeme ambao tutakuwa tunajiridhisha kwamba tunao tunaweza pia kutumia umeme huo kwa wajasiliamali kutengeneza ajira nyingi hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia utatupatia mapato ya Serikali kupitia tozo hizo kidogo ambazo tutakuwa tunazipata kutokana na matumizi ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze kwa kifupi sana kuhusu ujenzi wa mradi wa uzalishaji umeme ambao toka mwaka 1970 ndiyo ulikuwa umebuniwa na hakukua na mafanikio lakini azima yetu ya kuboresha eneo hili ndiyo kwa sababu tumeamua tutumie bonde lile la Mto Rufiji au maporomoko ya Mto Rufiji kuwa ndiyo maeneo ya kuzalishia umeme mwingi wa kutosha. Eneo hili tukishalianzisha kama alivyosema Mheshimiwa Waziri tutaongeza kiwango cha maji ambacho wanyama wetu kule msituni wataweza kutumia vizuri, lakini pia itasaidia kwenye umwagiliaji kwenye miji ambako watu wanaishi uko Ikwiriri na maeneo mengine ya

Wilayani Rufiji na eneo lote linalopita mto huo pamoja na kuongeza mazalia ya samaki ambayo pia tunayo, na kuongeza sasa ubora wa hifadhi yetu ya Selous ambayo pia itakuwa inaembelewa na watalii wengi na maeneo haya yatakuwa ni kivutio. Kwa hiyo, miradi hii ikiwemo na huu wa maporomoko ya Mto Rufiji malengo yetu hasa ni hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna mradi mwingine ambao Waheshimiwa Wabunge walitaka kujua unafaida gani, ujenzi wa reli ya kisasa. Hatuna ubishi kwenye ujenzi wa reli ya kisasa kwamba reli hii kwa miaka mingi ilikuwa inapoteza uwezo wake lakini sasa kwa kuanzisha mradi huu wa reli ya kimataifa *(standard gauge)* utaweza kusafirisha mizigo na abiria kwa haraka zaidi na kwa sababu tunatumia umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia kupitia mradi huu ambao tulitaka tujenge kwa kilometa 1219 utaweza kurahisisha pia kufanya biashara ya uhakika na nchi jirani kama Rwanda, Congo, Burundi na nchi yoyote ile ambayo itahitaji kutumia reli yetu kusafirisha mizigo yake. Kwa hiyo, tunauhakika kwamba kupitia reli hii tutaweza kupata fedha kupitia tozo mbalimbali za watumiaji wa reli hiyo kutoka nje ya nchi na ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia mnafahamu kwamba tunayo reli ambayo sasa inatumika tunaendelea kuiboresha ili iendelee kutoa huduma kwa sasa mpaka hapo tukapofanya mabadiliko na tunaendelea kupanua wigo kwa kuipeleka Tanga, tunaboresha kutoka Segera mpaka Arusha na kupitia Moshi na tunaendelea pia kuijenga/kuidumisha reli hiyo kutoka Tabora kuelekea Mpanda; na sasa nataka tuende mpaka Ziwa Tanganyika kule mpakani kabisa ili iendelee kutoa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapoanza sasa reli hii mpya itakuwa na uwezo wa kubeba mizigo zaidi ya tani 10,000 sawa na malori 250 ya tani 40/40 ambayo tutaondoa kwenye barabara. Kwa hiyo, faida nyingine kwamba tunataka tuimarishe barabara yetu iweze kutumika muda

mrefu ili pia iweze kutumika na wengi. Lakini pia kupitia mradi huu sasa tunazalisha ajira za kutiosha ambazo tumeanza kuona Watanzania wengi wakienda kupata ajira na utakapokamilika tunatarajia takribani ajira 30,000 za moja kwa moja na nyingine 600 kwa ajili ya wajenzi, walinzi na sekta zote ambazo zinahitaji kuhudumia njia hiyo ya reli.

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine ambao Waheshimiwa Wabunge walihitaji kujua kwa nini tumeutekeleza, ni ukuta kuzunguka Mradi wa Mererani.

Mheshimiwa Spika, wote mnajua kwamba Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kuhakikisha kuwa inalinda raslimali zetu, maliasili na madini. Ujenzi huu ambao umeshakamilika na umezinduliwa utasaidia sana kuhifadhi kulinda na maliasili ambazo ziko pale na Mheshimiwa Rais amefanya hili ilikuwa ni azma na hasa alidhamiria kufanya hivyo pale alipofanya ziara Mkoani Manyara na alikuwa anazindua barabara kutoka KIA kwenda Mererani na alipopata malamiko akaona ni muhimu sasa hayatekeleze.

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie ukuta huo wa kilometa 24.5 ambao umekamilika sasa utawezesha sasa mali zote kuzitambua pale ndani. Na ikumbukwe kwamba kabla ya ujenzi inakadiliwa kuwa kwa mujibu wa taarifa za Wataalam wetu inakadiliwa kuwa zaidi ya asilimia 40 ya uzalishaji ilikuwa inapotea tulikuwa hatuna manufaa nayo. Kwa hiyo, madini yetu ya Tanzanite sasa tunauhakika kwamba tunaweza kuyadhibiti na tukapata mapato yanayokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushahidi katika kipindi hiki kifupi ambacho tumeweka utaratibu wa ulinzi na huku ukuta unajengwa kuanzia Januari mpaka mwezi Machi, 2018 tumeingiza pato la milioni 714 kwa miezi mitatu tu ukilinganisha na pato ambalo tumelipata kuanzia Januari mapaka Disemba ya mwaka 2017 la milioni 147.1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo muone namna ambavyo tulikuwa tunapoteza fedha nyingi na sasa ambavyo

tunatarajia kupata pia fedha. Kwa hiyo, ukuta huu unafaida sana na tutaendelea kuimarsha na katika kuboresha tmeridhia ukuta ule na Mheshimiwa Rais ameridhia tumekaribisha Watanzania na wale wachimbaji na yoyote ambaye yuko kule jirani kuweka uwekezaji kule ndani, tutakuwa na maduka na nyumba ambazo za kupumuzika ili eneo lile kulifanya kuwa eneo la kivutio tutakuwa na nyumba za kufanyia mauzo ya hiyo Tanzanite kwenye eneo ambalo litakuwa kidogo linapandisha uchumi hata wenyeji wetu wa pale Mererani nao wataweza kunufaika na ujenzi wa ukuta huu wa pale Mererani.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na *issue* ya utambuzi wa mifugo, wengi walipoona kwenye risala yetu hawakuelewa tulikuwa tunalenga nini.

Waheshimiwa Wabunge, wote mnajua kwamba nchi yetu iliingia kwenye migogoro mingi sana ya wakulima na wafugaji na kukawa na ongezeko kubwa sana la mifugo nchini na mifugo mingine ilikuwa inatoka nje kuja kulisha ndani na kurudi nje ambayo sisi ilikuwa haitupi tija. Kwa hiyo, ili kudhibiti pia hata maliasili zetu zitumike na watanzania wenyewe kwanza, zoezi la kutambua mifugo maana yake linatuwezesha kutambua tuna mifugo mingapi, wapi na inamilikiwa na nani ili pia tuweze kuipangia utaratibu mzuri wa malisho wa namna nzuri ya huduma ya madawa lakini na huduma nyingine ikiwemo na jitihada tunazozifanya sasa za ujenzi wa viwanda ambavyo vitataka Watanzania wanufaike kupeleka ng'ombe, wauze, wapate fedha za kutosha ili waweze kujiendesha maisha yao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, zoezi hili tumeendelea, lina faida nyingi na nawasihi tu Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuendelee kushirikiana ili tukomeshe mauaji ya wakulima na wafugaji ambayo kwa sasa kumetulia kidogo na tungependa utulivu huu uendelee kwa kutokana na zoezi hili ambalo tunaendelea nalo.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge niseme tumepata faraja sana kuona utulivu huu, mauaji tena ya wakulima na

wafugaji yamepungua na tutaendelea kuyadhibiti kadri ambavyo tutaweza kulisimamia zoezi hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kujibu hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge nao pia waliweza kuzieleza na sisi tulizichukua sasa ni muhimu kuzitolea majibu na baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kwa Serikali zimejibiwa na Waheshimiwa Mawaziri wa kisekta, lakini Naibu Mawaziri nao wamejibu na zile hoja zilizosalia zitajibiwa kama ambavyo tumeendelea, ziko nyingine ambazo tutazijibu kwa maandishi na hoja ambazo pia zina mwelekeo wa kisekta zitatolewa ufafanuzi na baadhi ya Wizara ambazo zitakuja hapa kuja kuwasilisha bajeti zake na tayari tumewaagiza maswali yote na hoja zenu zote waziweke ili waje wazitolee majibu wakati wa hoja zao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(13) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la mwaka 2016 naomba sasa nitumie fursa hii ili kujibu sambamba na kutolea ufafanuzi kuhusu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ambavyo zimetolewa.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria walitaka Serikali kudhibiti zabuni za ujenzi wa miradi ya maendeleo kwamba zabuni hizi za ujenzi wa miradi ya maendeleo zitolewe kwa uwazi. Lakini kipaumbele kitolewe kwa makampuni ya ndani ya nchi ya wakandarasi yanayokidhi vigezo na uwezo wa kutekeleza, kukamilisha miradi kwa wakati na kwa mujibu wa mikataba ya miradi husika.

Mhesghimiwa Spika, nataka nieleze kwa Watanzania kwamba tumeimarisha utoaji wa zabuni. Zabuni zetu zinatolewa kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura ya 410 ambayo wote wanapata zabuni zile ni wale wenye makampuni yaliyosajiliwa, yana sifa zote na yana uwezo wa kutekeleza miradi na zabuni hizi ni za wazi na mara nyingi tunashindanisha kwa makampuni ambayo yanahitaji kuomba nafasi hizo. Lakini pia tumeanza kutoa mwongozo wa ushirikishwaji wa Watanzania ili kupata zabuni zile *(local*

*content).* Kwa hiyo, tuna uhakika sasa kwa utaratibu tuliojiwekea Watanzania wenye makampuni wataendelea kunufaika na zabuni za ndani ili pia waweze kufanya kazi za ndani tuweze kuwajengea uwezo wa kufanya kazi hizo na kuongeza kazi nyingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, na tumeanza kushuhudia makampuni mengi ya Kitanzania yakifanya kazi hizo, lakini pia hata Serikali imetoa nafasi ya kuzungumza na *private sectors* (sekta binafsi) ili kusikia changamoto wanazozikabili na sisi kuwaambia yale ambayo wanatakiwa waboreshe ili tuendelee pia kuimarisha kwenye maeneo hayo. Lengo letu la kukutana nao ni kutaka tu kuhakikisha kwamba na wao wananufaika na zabuni za ndani ya nchi ili fedha ambayo inalipwa iendelee kubaki nchini na pale ambapo inabidi kupata makampuni ya nje mara chache ndiyo wanaweza kupata nafasi kwa kadri ya ushindani utakavyojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ambayo Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI iliitoa inayotaka Serikali kuimarisha ukusanyaji wa mapato, udhibiti wa matumizi ya Serikali na ufuatiliaji wa miradi yetu ya maendeleo. Wanataka Serikali ihakikishe kuwa fedha zote za miradi ya maendeleo zinatumika kwa tija na kwa kuzingata thamani ya fedha ya miradi husika *(value for money).*

Mheshimiwa Spika, lakini pia wanataka Serikali iweke mpango mkakati wa kupata vyanzo zaidi vya mapato ili viweze kutekeleza miradi yote ya maendeleo. Kwenye hoja hii nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali imepokea maoni haya na kwamba tutaendelea kuyafanyia kazi kupitia mkakati ambao tumeuweka wa kwanza, kubainisha vyanzo vyote vya mapato kwa kila sekta. *(Makofi)*

Mbili, ukusanyaji wa mapato hayo na kwenye ukusanyaji wa mapato haya tumetaka ukusanyaji wote uwe wa kielektroniki ili kudhibiti mianya ya kupoteza fedha na

tumeanza kuona tija kwa kutumia elektroniki tunapata mabadiliko makubwa sana ya fedha ambayo tunaikusanya. Lakini pia baada ya kuwa tumekusanya fedha hizi, tumeweka mfumo wa kudhibiti matumizi yake na tumesisitiza kwa watumishi wenye dhamana ya matumizi ya fedha hizi za umma ni lazima wawe waadilifu na waaminifu na tumesimamia hili pia kwa kupeleka kaguzi za mara kwa mara kuona kama fedha hizi kweli zinakusanywa, zinatumika vizuri baada ya kuwa tumeetoa maelekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na hii pia tumeelekeza hata kwenye Halmashauri zetu. Halmashauri zote zibainishe vyanzo vya mapato, Halmashauri zijikite katika kukusanya mapato yake, lakini baada ya mipango kupitia Baraza la Madiwani lazima tusimamie matumizi na tumewaasa Baraza la Madiwani lisimamie kikamilifu matumizi ya fedha hizi badala ya kuwaachia Wakuu wa Idara pekee na pale kwenye uovu taarifa itolewe na kupitia kaguzi za ndani na wakaguzi wa nje nao watabaini na pale ambako kuna tatizo tunachukua hatua mara moja kwa wale wote ambao siyo waaminifu katika kuhifadhi fedha hizi na kuzitumia.

Mheshimiwa Spika, na Halmashauri tumezipa malengo. Tunataka kila Halmashauri mwishoni mwa mwaka wawe wamekusanya kwa asilimia 80. Mkakati huu bado unaendelea na kwenye Halmashauri zetu mtakapoingia kwenye Mabaraza ya Madiwani endeleeni kusisitiza na kwa kufanya hilo inawapa fursa Waheshimiwa Wabunge kupanga mipango ya maendeleo kwenye Halmashauri zenu vilevile na Waheshimiwa Madiwani.

Kwa hiyo, tuungane pamoja katika kudhibiti jambo hili la ukusanyaji wa mapato lakini pia namna ya kutumia fedha zile na zote tuhakikishe zinakwenda kweye miradi ya maendeleo ya wananchi ambayo italeta tija kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja inayohusu usimamizi na matumizi ya fedha za umma ambayo nimeieleza vizuri na mimi nasema kwenye eneo hili tumeanza

kupata *report* ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Fedha za Ndani za Serikali ambayo ilikabidhiwa kwa Mheshimiwa Rais hivi karibuni na tutakuja kuileta Bungeni ili pia tuweze kufanya mapitia kwa pamoja. Nataka niwahakikishie hiyo ni njia mojawapo ya kudhibiti matumizi haya ya fedha za umma na tutaendelea kudhibiti matumizi ya umma na tumeendelea kuchukua hatua kwenye maeneo ambayo udhibiti wake una udhaifu.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumepata taarifa na wote mnajua kwenye ukaguzi wa mwaka wa fedha 2016/2017 Kurugenzi tatu tu ndiyo zimepata hati chafu nchini kati ya Halmashauri zote 180 na ngapi na hatua kali zimechukuliwa dhidi yao na hilo ni fundisho kwa Wakurugenzi wengine kwamba lazima wasimamie matumizi sahihi ya fedha za Serikali na Waheshimiwa Madiwani waendelee kutusaidia kubainisha matatizo ya matumizi ya fedha kwenye Halmashauri hizo na Waheshimiwa Wabunge wenzangu na ninyi ni sehemu ya wategemewa wetu kwamba mtatuambia wapi kuna tatizo na ili tuweze kuchukua hatua kwa lengo la kunusuru fedha hizi za umma ziende kwa wananchi kutekeleza miradi wanayoitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine ya miradi ya maji vijijini, hoja imeitaka Serikali ikubali kuanzisha Wakala wa Maji Vijijini pamoja na kuongeza tozo za shilingi 50 kwenye mafuta ya petroli na dizeli ili kutunisha Mfuko wa Maji kwa lengo la kutatua tatizo la maji ambalo linagusa maneo mengi hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nieleze kwamba Serikali yetu ya Awamu ya Tano imedhamiria kwa dhati kuhakikisha kwamba tunatoa huduma za maji kwenye miji yetu na vijijini na Mheshimiwa Rais katika hili amewekea msisitizo na amehakikisha kwamba maeneo yote ya miji na vijijini kunakuwa na miradi ya maji na ameanzisha kampeni ya kumtua ndoo mama kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampeni hii maana yake ni kuhakikisha kila kijiji wanakuwa na eneo la kuchota maji ili

kumwezesha mwanakijiji asizagae hovyo bila kujua wapi mahali pa kupata maji. Kwa hiyo, Wizara ya Maji imeendelea kufanya vizuri sana, Waziri na Naibu Waziri wanafanya kazi yao vizuri, Katibu Mkuu na wote kwenye Ofisi ile kuhakikisha kwamba miradi yote inaratibiwa vizuri na inakwenda vijijini na kwa bahati nzuri na mimi nimefanya ziara kwenye maeneo niliyopita kila Halmashauri ya Wilaya ina miradi ya maji. Mahitaji ya maji ni makubwa, lakini nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba zoezi letu la kuhakikisha tunatoa huduma ya maji linaendelea. Malengo yetu kufikia mwaka 2020 maeneo ya miji yawe yamefikia asilimia 95 na maeneo ya vijijini angalau tuwe tumefikia asilimia 85 ya huduma ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutaenedelea kutafuta vyanzo zaidi vya kuhakikisha kwamba tunaanzisha miradi mingi ya maji kwa ajili ya matumizi ya vijijini. Kwa hiyo, wazo lenu la Serikali iendelee kutafakari kwa makini namna ya kupata fedha hasa kwa kuingiza tozo ya shilingi 50 kwenye mafuta ya petroli na dizeli tunaendelea kutafakari na tutawaambia hatua tuliyoifikia baada ya kuona miradi hii tuliyoiweka, miradi ambayo tumeipanga na tumeipeleka vijijini; tumeshapeleka vijiji vingapi, miji mingapi na miji mingapi na vijiji vingapi bado havijapata huduma ya maji na gharama ya miradi inayotakiwa ni ya kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa kila Halmashauri tumeagiza kila kijiji kifanyiwe upembuzi yakinifu kuona wapi tunaweza kupata chanzo cha maji ili tutoe huduma ya maji kwenye Hamashauri hiyo.

Mheshimiwa Spika, eneo la nne, ni elimu msingi bila malipo. Utekelezaji wa mpango huu bila malipo toka ulipoanzishwa tumeanza kuona mafanikio makubwa. Moja imeongeza idadi ya usajili, imepunguza kero za wazazi za kuchangia ile michango ile holela holela, hapa tunazungumzia ile michango holela na michango ile ingawa pamoja ilikuwa ina tija, Serikali ilichofanya ni kupeleka fedha badala ya kuwachangisha wananchi na tumeshaeleza mara kadhaa na hapa narudia tu kueleza kwamba tunaendelea

kutuma fedha kwenye Halmashauri zetu na zinaenda kwenye shule za msingi na sekondari na jumla ya bilioni 18.5 zinakwenda pamoja na fedha ambazo tumezipeleka sasa fedha majukumu kwa ajili ya Maafisa Elimu, Wakuu wa Shule na Waratibu Elimu Kata nazo pia zinaendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai mwaka 2017 mpaka mwezi Machi 2018, jumla ya shilingi bilioni 187 zimetumika kupeleka kwenye shule zetu ili kuendelea kuwapunguzia wazazi wa kuchangia ile michango midogo midogo. Suala la michango limeratibiwa vizuri, hatujazuia michango kwa wananchi, lakini tumeliondoa kwenye ngazi ya shule kwa sababu ya kuogopa kuwa huru wa kuchangisha michango mingi kwa kisingizio kwamba wamekaa na kamati za shule, wamekaa na bodi za shule na hatimaye kurudisha tena kero kwa wazazi badala yake michango hii sasa itaratibiwa na Mkurugenzi kwenye Halmashauri. Mkurugenzi anayo fursa au kwa kuanzisha Mfuko wa Elimu kwenye Halmashauri na kuwataka wazazi wachangie ili kupeleka huduma kwenye maneo mengine inaweza kuwa miundombinu au vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia sana suala la upatikanaji wa chakula kwenye shule zetu ambazo wanafunzi wetu wanahitaji kupata chakula. Jambo hili linaweza kuratibiwa vilevile lakini lazima lisimamiwe na Mkurugenzi kwa sababu tunapokuwa na shule mbili jirani kwenye kijiji, shule moja imekuwa na ubunifu wamepata chakula, shule nyingine hawana ubunifu, hawana chakula tunaleta mgongano pale kijijini na ndiyo maana tumesema Mkurugenzi aratibu vizuri michango. Suala la chakula shuleni ni muhimu kwa hiyo muhimu zaidi ni kwamba Wakurugenzi wote waendele na ubunifu, watenge fedha kwenye bajeti zao za halmashauri, wajue wana shule ngapi zinahitaji kuhudumiwa kwa chakula na hasa zile ambazo ziko pembeni sana na vijiji ambazo hazimuwezeshi mwanafunzi kurudi nyumbani. Kwa hiyo michango yote sasa itaratibiwa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ili ngazi ya shule waendelee na kazi yao ya utoaji wa taaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kuimarisha kutoa huduma kwa kupeleka fedha kadri tunavyozipata na kwa kadri ya mahitaji kule shuleni ili jambo hili tuweze kuwaondolea kero wazazi walioko kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, eneo la tano, ni uzalishaji wa mazao ya biashara ambayo tumezungumza mara kadhaa na utekelezaji wake tumeuona, manufaa kadhaa tumeyaona, lakini tulianza na mazao matano; kahawa, chai, tumbaku, korosho na pamba. Tumesimamia kutoka kilimo chake mpaka masoko yake, lakini siyo kwamba ndiyo mwisho, tunaendelea kuratibu mazo mengine. Tunatambua tuna alizeti, ufuta, mbaazi, karafuu kule Zanzibar, tuna mazao mengine kama ya jamii ya kunde, mazao haya yote yanaendelea kuratibiwa na Wizara ya Kilimo na mimi nawataka Wizara ya Kilimo sasa muharakishe uratibu wa mazao haya ili nayo pia yaingie kwenye mpango bora wa kilimo na tukashirikisha Maafisa wa Kilimo wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nini tumekifanya Serikali? Kwanza tumeimarisha ugani kwenye ngazi za vijiji na Kata na kupitia ugani pia tumeimarisha vyuo vya utafiti ili viweze kutafiti mazao haya kutoka ardhi inayofaa kupandwa kwenye maeneo haya lakini namna ya kulihudumia zao lenyewe.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho, tunaendelea kuimarisha ushirika kwa maana ya sekta ya masoko ili kuweza kuweka mfumo mzuri wa kumwezesha mkulima kuuza mazao yake na tuna uhakika maeneo haya tutayaimarisha. Lakini tuna zao la mkonge ambalo pia nalo sasa linaanza kutuletea tija na lina bei inapanda juu ambalo linalimwa maeneo machache hasa Mkoa wa Tanga, Kilimanjaro maeneo Same na maeneo machache sana kama mkoani Morogoro. Tumeendelea pia nalo kuratibu vizuri na tumeshaoweka Afisa Zao la Katani ndani ya Wizara ili ashirikiane na wakulima wa mzao haya ambayo kilimo chake kinahitaji zaidi ya ukubwa wa hekari tano, 10 na kuendelea. Kwa hiyo, tumeimarisha mfumo wa kilimo kwa ujumla wake na mimi nina uhakika hatua tunayoifikia sasa itatusaidia sana kuhakikisha kwamba wakulima wetu wanapata tija.

Mheshimiwa Spika, kwa wafanyabiashara kwenye eneo hili nao pia hatujawaacha nyuma, tumeendelea kukaa nao vikao mbalimbali kuwaonesha njia nzuri ya kupata uwezo wa kununua mazao yetu ili mazao haya yapate masoko mazuri. Najua saa hizi tunahangaika na soko la mbaazi ambako ni nchi pekee ambayo inatumia mbaazi kwa wingi ni nchi ya India na India kwa miaka yote hiyo walikuwa wanalima zao hilo na kwa bahati nzuri kwao na mbaya kwetu, ilipofikia mwaka 2017 walikuwa wamezalisha mbaazi zaidi ya asilimia 30 ya uwezo wa kawaida, kwa hiyo, wamezuia kuingiza mbaazi kutoka nchi nyingine kwa sababu wana mbaazi nyingi zinatosha. Hata hivyo tunaendelea kuzungumza nao na tuliwahi kusema hapa mbele yenu bado niendelee kuwahakikishia kwamba mazungumzo yanaendelea ili kuhakikisha kwamba tunapata masoko ya mazao yetu ili yaweze kupata tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wa sita ambao kwangu mimi nahitaji kuueleza ni hii miradi mikubwa; ni namna ambavyo Serikali inatakiwa kuimarisha ajira kwa Watanzania kupitia miradi ambayo tunaitekeleza.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kujihakikishia kwamba fursa hizi za kuanzisha miradi hii mikubwa ni fursa ambazo pia zitatoa nafasi ya ajira kwa Watanzania na tumejiwekea malengo kwenye miradi hii mikubwa, idadi ya wageni ambao wanatakiwa kufanyakazi katika maeneo yale. Tunajua tuna wataalam na tunajua pia na sisi tumekosa utalaam baadhi ya maeneo, kwa hiyo, tumetoa fursa kwa wageni lakini kwa uratibu mzuri sana kuona ni wangapi na utaalamu gani unatakiwa ambao sisi hatuna ndiyo tunawpaa fursa, vinginevyo idadi kubwa ya waajiriwa ni watanzania wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna miradi mikubwa mingi tu ila yote niliyoitaja awali; reli, viwanja vya ndege, ujenzi wa mitambo ya umeme, lakini hata bomba pia la Tanga - Hoima nayo ni sehemu ya ajira na litachukua sehemu kubwa sana, kwa hiyo, tuendelee kuwapa matumaini Watanzania kwamba tunahitaji sasa kupanua wigo wa kupata ajira. Na

kwa taarifa tulizonazo sasa kwenye miradi hii zaidi ya asilimia 80 ya kila mradi uliopo ni Watanzania wenyewe kwahiyo tunaleta faraja, nataka niwahakikishie tutaendelea kuimarisha/kuongeza idadi ya miradi ili watanzania wengi wapate fursa ya kuweza kuajiriwa na kufanyakazi waweze kupata vipato vyao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niendelee kusisitiza tu kwamba miradi hii mikubwa, moja kati ya faida kubwa tunayoipata ni kupunguza kilio cha ajira na uzuri wa miradi hii yote inachukua ajira za watu wa ngazo zote, za elimu zote; asiyesoma kabisa, wa darasa la saba, kidato cha nne mpaka hao waliomaliza ma-*degree* wanapata fursa ya kufanyakazi kwenye sekta hizo. Na Serikali pia imeandaa utaratibu au programu maalum ya kitaifa ya kukuza ujuzi, kuwawezesha Watanzania kufanyakazi kwenye maeneo hayo ili wawe na sifa na programu hizi zinaendelea na Serikali imetenga fedha za kugharamia mafunzo hayo, lakini tumehamasisha wale Watanzania wanaoendesha miradi hii au wanaoendesha sekta za kibiashara kuwapokea Watanzania wetu kwenda kupata ujuzi kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, na mafunzo haya tumeyapa asilimia 60/70 wanatumia mafunzo kazini zaidi halafu asilimia 40/30 wanatumia kwa kupata maelekezo na tumeanza kushuhudia vijana wetu wakimaliza wanapata ujuzi wanapata na ajira pia. Kwa hiyo, tumetengeneza utaratibu ambao Watanzania wanaendelea kupata ajira kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya saba inayotaka Waziri Mkuu kufanya ziara katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wenzangu nitafanya ziara mikoa yote nchini na si tu kwenye mikoa, nataka nifike kwenye Wilaya na majimbo yenu nakuja kuona kazi zinazoendelea, kuja kuona changamoto zilizopo, lakini kutatua changamoto zilizopo na maeneo tuliyopita tumefanya haya.

Kwa hiyo, wale ambao mikoa yao bado sijagusa baada ya Bunge tunakuja kuona miradi yenu na hizi ziara hizi ndio zinaongeza na nani kwenu kwa hiyo tutaendelea kuja kuwatembelea ili muweze kupata fursa ya kuonyesha miradi mliyoitekeleza katika kipindi chote ambacho mpo na tutaendelea kuwaunga mkono kuhakikisha kwamba mnafanya kazi vizuri wakati wote kwenye majimbo yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya nane Waheshimiwa Wabunge walisema Serikali iendelee kusimamia amani, umoja na mshikamano wa kitaifa. Jambo hili ni muhimu sana na ninapolizungumza niseme tu kwamba tutaendelea kusimamia kwamba nchi hii inaendelea kuwa na amani, umoja na mshikamano wa kitaifa na tunapotumia kupata nafasi hizi ni lazima tuendelee kukumbushana Watanzania wote kwamba nchi hii ili tupate maendeleo ambayo tunayalilia ambayo Waheshimiwa Wabunge wanaelezea wanaruhusu fedha zitumike kwanza lazima tuwe na amani ili pia tuweze kufanya hayo maendeleo ambayo tunayahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia maendeleo ya maji lazima tuwe na amani, elimu tuwe na amani, kilimo tuwe na amani nchi zote zenye vita watu hawana nafasi ya kuoga hamna mtu anafuata maji kila mmoja anakimbia huko anakojua alikotizama hajui kama huko kuna huduma au la ilimradi ameokoa maisha yake. Mmeshuhudia nchi mbalimbali tena nchi nyingi zinakimbilia Tanzania, sasa je, Watanzania tukianza kukurupushana hapa ndani tunakimbilia wapi? Kama wao wanakuja hapa sisi tunaenda wapi? Kwa hiyo, ni muhimu sana tukasimamia amani yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kutoa wito kila mmoja kwa nafasi yake aendelee kuimba amani, aendelee kuimba msisitizo na utulivu wa nchi ili tuweze kufanya maendeleo ambayo tunakusudia. Nitoe wito kwa kila mmoja kutekeleza adhima hii ili pia tuweze kusimamia amani yetu hapa nchini ni jambo muhimu sana tupambane na yale yote ambayo

yanaleta uchokozi wa amani wa kuvunja amani nchini ili pia kila mmoja aweze kuwajibika namna ambavyo tunataka tuweze kuimarisha amani ambayo tunayo kila mmoja ajaribu kuepuka matatizo yanayopelekea nchi hii kuwa isitawalike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo limezungumzwa sana jana kwa masikitiko makubwa ni suala la Muungano nieleze sana masikitiko yangu juu ya mjadala ulioendelea jana sikuridhika sijaridhishwa na mjadala wa jana najua ziko hoja, lakini mjadala wa jana kwa namna nilivyojifunza ni migogoro ya mtu na mtu, kundi na kundi jambo ambalo halileti tija wala afya hapa kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba Muungano wetu unaendelea vizuri, lakini natambua pia yako mapungufu na viongozi wetu wote Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Serikali za Mapinduzi Zanzibar wote wameapa kusimamia Muungano huu na sisi jukumu letu pia kuhakikisha kwamba tunaunga mkono ili tuulinde Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba kutokana na kuingia madarakani na sasa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ina miaka miwili, yako maboresho Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yako maboresho. Maboresho haya yanaweza kuathiri mfumo wa kawaida ambao tulianza nao ambao tunaumaliza kupitia vikao ambavyo tulivyonavyo, inawezekana jambo hilo baada ya mabadiliko linahitaji *harmonization* ya kisheria. Kwa hiyo, jukumu hilo ni jukumu la Kamati ambayo inasimamiwa na Makamu wa Rais ambaye pia naye ndio anahitisha kikao cha pamoja ili tuweze kuzungumza. Lakini kwa namna ambavyo mjadala umeendelea jana na watakao na niwasihi sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu hakuna afya kwenye mjadala kama ule wa jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuzuii Mbunge yeyote kuuliza swali lolote juu ya ufafanuzi juu ya mwenendo wa Muungano lakini majibishano ya mtu mmoja na mmoja hayo hayana

afya. Lakini tumeanza kulifanyia kazi na hatutatoa mwanya wa Wabunge kujibishana kupeana maneno makali kwa sababu ya mwenendo wa Muungano Serikali tumejipanga vizuri tutasimamia Muungano wetu, tutatoa kero zetu ili tuende vizuri pande zote mbili tuweze kufurahia Muungano wetu ambao sasa tunao.

Mheshimiwa Spika, mimi niseme tu kwamba Muungano wetu ambao huwa tunakutana mara kadhaa katika kujadili vitu ambavyo vinahitaji kufanyiwa mabadiliko Makamu wa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan ndio Mwenyekiti wetu na sisi watendaji wa chini, mimi ni mjumbe na Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar ni mjumbe na Mawaziri walioko kwenye Wizara zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa tumefanya mabadiliko kadhaa ndani ya Serikali na namna ya kuendesha sekta mbalimbali ni kweli yako maeneo ambayo yanahitaji kubadilisha pia na sheria na vitu vingine, mijadala yetu inaendelea na tarehe 28 hapa tunakutana na tunafanya/ tunaendelea na mjadala huu wa maeneo yote ambayo yanaweza kuleta manung'uniko. Kwa hiyo, nawasihi Waheshimiwa Wabunge wenzangu jambo hili tuliendeshe kwa lugha nzuri za kiistarabu si vyema tukafanya tukarudia tena kama ilivyotokea jana, haifurahishi kundi moja likakasirika lakini kwa sababu mtu mmoja au wawili kuwakasirisha watu wengine jambo hili si jema sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini yote hii imetokana na *issue* ya sukari na mimi nataka nieleze nchi yetu inahitaji sukari kwa sababu hatuna viwanda vinavyotosha kuzalisha sukari. Zanzibar tunahitaji sukari, Bara tunahitaji sukari; na kwa kuwa Zanzibar wana kiwanda kimoja, Bara tuna viwanda vitano, viwanda hivi vitano vyote havitoshi kupeleka sukari hata kule Zanzibar kutoka huku mpaka kule Zanzibar hata kila Kiwanda cha Mahonda kiwe na uwezo wa kuzalisha sukari ikatosha Zanzibar pia na huku kwa hiyo tunachofanya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara ya Biashara ndio inayoratibu uletaji wa sukari Zanzibar na Serikali ile inatoa fursa wafanyabiashara kuleta sukari nchini pale Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, huku Bara tumeunda chombo kinaitwa Bodi ya Sukari ndio inaratibu kuleta sukari iwe kutoka ndani kupitia viwanda vyetu au kutoka nje ya nchi sasa sukari ya Bara kupitia viwanda vyake na huu ni mkakati wa kitaifa wa kulinda viwanda vya ndani, tunapolinda viwanda vya ndani tumebana uingizaji holela wa sukari ndani ya nchi ili tusije tukaathiri uzalishaji wa ndani. Huku tukiwa tunaendelea ku-*harmonize* kodi zake na nini, utakuta sukari ya nje inayoingia nchini ni ya bei rahisi kuliko sukari inayozalishwa ndani ya nchi na kwa maana hiyo kiwango cha sukari inayozalishwa ndani gharama yake inakuwa kubwa viwanda vya Bara hata kila cha Zanzibar gharama yake ni kubwa, kwa hiyo, ukileta sukari kutoka nje maana yake sukari ya ndani haiwezi kuuzika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa jambo ambalo najua Mawaziri tunahitaji pia tuwe tunawapa taarifa Watanzania na Waheshimiwa Wabunge wakiwepo ni kwamba mpango wa sukari kwa Tanzania Bara hata ile *gape sugar* tuwe tunapotoa matangazo kutaka watu na kuwapa vibali walete hatuchagui kama  tumempa kibali ni wa Bara au wa Zanzibar wote wanapata sukari, nataka niwaambie mimi ndio natoa vibali mwaka 2016 tulipoingia madarakani tulikuwa na *gape sugar* ya tani 140000 kwenye tani 140000 kati ya wafanyabiashara ambao tumewapa vibali wa Zanzibar wawili na watanzania Bara watatu lakini kiwanda hicho cha Mahonda nilikipa kibali kikaingiza tani 390. Naeleza hili ili muone kwamba tunafanya kazi kwa pamoja mwaka 2017 sukari ambayo tumeingiza *gape sugar* ni tani 140000 walioleta sukari Tanzania ni Wazanzibar wawili na wa Bara wawili. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, muone namna ambavyo tunashirikiana na wale Wazanzibar mmoja ni *agent* wa hiyo Mahonda. Nataka niwaambie ukweli ili muone kwamba tunapotoa vibali hivi hatuangalii sura, hatuangalii huyu mtu anatoka wapi, ili mradi mfanyabiashara Mtanzania tunatoa vibali. Ni mwaka huu tu sasa tume-*improve* zaidi tumesema sukari mwaka huu ebu tuwape wazalishaji wenyewe na kibali cha *gape sugar* ya tani 135,000 tumewapa viwanda vyenyewe

na tayari wameshaagiza na sasa sukari imeshaanza kuingia tulitaka tuwahi hata Mfungo wa Ramadhani ili nchi nzima iwe na sukari ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hasa mwaka huu peke yake ndio haijafanya Wazanzibari kuingia wala Watanzania kupata vibali wafanyabiashara wengine kwa sababu inaletwa na viwanda vyenyewe. Kwa hiyo, kama kuna malalamiko yaliyopitia hapa Bungeni yakaletwa hapa kwamba hakuna vibali ni kutokana na *nature* hiyo. Na mimi naamini wakati huo tunafanya majaribio, lakini mkakati wetu tunavitaka viwanda hivi vizalishe sukari ya kutosha ili nchi ijitegemee yenyewe na tukiruhusu sukari nyingi kuingia kwa uingzaji holela viwanda hivi sukari yao itabaki viwandani haitanunulika kwa sababu sukari ya ndani ina gharama kubwa kuliko sukari ya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kauli hii Mawaziri wa biashara wote wa Bara na Visiwani kama tutaiangalia vizuri hata kule Zanzibar kiwanda cha Mahonda hicho kiwango cha uzalishaji wake ile *gape sugar* ndio tutoe vibali badala ya kuacha watu wanaingiza holela vitafunika soko la ndani.

Mheshimiwa Spika, mimi nilishafika Zanzibar nimeshazungumza na Waziri wa Biashara, nimeshazungumza na Waziri wa Kilimo wakati ule Mheshimiwa Hamad Rashid, yule mfanyabiashara wa Mahonda amekuwa na matatizo mengi sana, miwa yake mara nyingi imekuwa ikichomwa, haifikii uzalishaji na leo kiwanda kile kimefungwa hakizalishi.

Mheshimiwa Spika, ni jukumu letu sisi kuhakikisha tunamlinda mwekezaji yule na mtaji aliouweka pale ili aweze kupata mtaji hakuna sababu Waheshimiwa Wabunge kulumbana hapa suala la sukari, sukari imeratibiwa vizuri, lakini uratibu huo tunalinda viwanda vya ndani, tunataka viwanda hivi vizalishe, viongeze uwezo, viongeze mtaji ili viweze kutosheleza mahitaji ya ndani tunaweza kusema nchi nzima tuna viwanda sita tu Kilombero, *Kagera Sugar*, Mtibwa, *Manyara Sugar* lakini pia tuna hiyo Mahonda ni viwanda hivyo tu tunaongeza kiwanda kimoja *Bagamoyo Sugar*

wameshaanza kujenga, tunaongeza kiwanda pale Mbigili, Mkulazi malengo yetu tuongeze sukari. Tuna shamba Kigoma kubwa sana tunataka tulime sukari, pale Manyara tunataka tupanue lile shamba nimeshakwenda pale kiwandani kuona wana eneo kubwa tu wanaweza kupanua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi yetu sasa ni kuwezesha viwanda hivi na wawekezaji kupata mtaji wa kupanua viwanda ili sukari iingie hapa ndani yaani tuzalishe ndani, ijitosheleze hapa ndani. Kwa hiyo, nataka niseme Waheshimiwa Wabunge msigombane bure, sukari tumetaka viwanda vya ndani viwe na uwezo wa kuzalisha vifikie malengo, hatuhitaji kuagiza mara kwa mara, kwanza sukari nyingi tukiileta watu wa *TFDA* wanasema rudisha kwa sababu labda inakosa ubora na vitu vya namna hiyo. Lazima tujiridhishe sukari inayoingia nchini ina ubora, kwa hiyo, naamini baada ya kauli hii mgogoro huu wa sukari sitousikia tena hapa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nakaribisha maoni ya namna ya kuboresha sekta hii na bado Wizara ya Kilimo itakuja kwa hiyo, mnaweza mkatoa pia maoni yenu si tutakuwa hapa tunasikiliza tutapokea maoni yenu Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, jambo hili la sukari lisivuruge Muungano wetu, jambo hili la migogoro mingine, mapungufu mengine kwenye Muungano wala lisiwe jambo kubwa kwa sababu Kamati ipo na sisi tuko tayari tutasimamia mapungufu yote, tutayaondoa Bara na Zanzibar ni nchi moja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kila mmoja, ni kila mmoja ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kusema haya nadhani kwenye eneo hili ambalo nimetumia muda mrefu nitakuwa nimeeleweka na naomba niwasihi mnielewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba baada ya kusema haya sasa naomba nihitimishe na nikiri kwamba hoja zote za Waheshimiwa Wabunge zilizowasilishwa na kuzungumzwa moja kwa moja hapa Bungeni na zile za maandishi zote ni za msingi na ni muhimu na hivyo Serikali inazipokea na

tutazifanyia kazi. Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti Serikali imeadhimia kwa dhati kabisa kuhakikisha kwamba utekelezaji wa miradi kuimarisha utendaji, usimamizi makini wa rasilimali na nidhamu ili kukidhi dhumuni rasmi la Serikali katika kuwafikishia wananchi huduma za kuwaletea maendeleo hili tutalisimamia kikamilifu, tunataka watanzania wanufaike na huduma zote za nchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea pia kutenga fedha ili kukabiliana na changamoto mbalimbali zilizopo katika sekta zote na msukumo utawekwa katika kusimamia utekelezaji wa mageuzi yaliyobaki katika sekta mbalimbali ikiwemo ya kilimo, mifugo, uvuvi, maji na miradi mikubwa yote ya kielelezo ili ikikamilika na ikamilike kwa haraka na ianze kuleta mafao ambayo tunayatarajia kuyapata au manufaa tunayotarajia kuyapata ikiwemo na ajira kutoka kwa Watanzania, muhimu pia hapa ni kukumbuka kuwa bajeti ni chombo muhimu cha kutekeleza sera na malengo yaliyowekwa kupitia Serikali iliyopo madarakani na mimi naamini kama ilivyotangulia kuelezwa hapo awali muda hautoshi kujibu kila hoja ningeweza kutoa ufafanuzi yote lakini yote yameelezwa menigne yote yameelezwa na Wabunge na kwa sababu tuko hapa miezi mitatu kadri jambo linapozaliwa mko huru kuja kwa *consultation* halafu tuweze kutoa ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tuendelee kuunga mkono jitihada za viongozi wetu na hasa kiongozi wetu Mkuu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi zake kubwa anazozifanya katika kuimarisha ulinzi wa rasilimali za Taifa ikiwemo madini na tumeongeza ukusanyaji wa mapato ambayo yametuwezesha sasa kutekeleza mafanikio haya ambayo tumeyaeleza kwenye hotuba yetu yote na yale ambayo yatakuja kuzungumzwa na sekta husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusisitiza tena kwamba suala la kuwahudumia Watanzania, kuwaletea maendeleo pamoja na kuhakikisha nchi yetu inafikia uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda mafanikio yake hayo

yatatoka mikononi mwetu sisi sote. Kwa hiyo, ni muhimu sana sasa wote tuunge mkono jitihada za Serikali ili tuweze kuwafikia wananchi wetu huko waliko kwa kuwapelekea miradi ya maendeleo ni muhimu sana pia kwa wadau wote kufanya kazi zaidi kwa kuwa na nidhamu zaidi katika kila jambo umnalolifanya ili uweze kupata matokeo mazuri, na hii sasa tuendelee sasa kuunga mkono falsafa hii ya awamu ya tano ya hapa kazi tu ndio italeta majibu ya haya yote tunayosema.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YANDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono tunakushukuru sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuhitimisha hoja yako, ambayo uhitimishaji wake umeungwa mkono na Wabunge wengi sana humu ndani hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Katibu!

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI- KATIBU WA BUNGE**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Kamati ya Matumizi, Waheshimiwa Wabunge naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza zoezi la kupitia mafungu. Tunakumbushana tu kuhusu utaratibu ambao tumekuwa tukiutumia.

Sasa tuko katikati ya Bunge, kwa hiyo, naamini kanuni zetu mnazifahamu vizuri, sina haja ya kuzirudia sana. Wale mtakaosimama kwenye mishahara ya Mawaziri mtauliza masuala ya kisera tu!

Majina ya watakaofanya hivyo mtayapata kutoka kwenye kambi za vyama, kutoka kwa Makatibu wenu. Tukishamaliza majina yale kwa nafasi ambazo zimekubalika mezani kwa dakika ambazo tumegawana tutaendelea na mafungu mengine kwa Mbunge yeyote kuweza kusimama kwenye fungu lolote maalum ambalo anataka ufafanuzi wa ziada.

Kila Mbunge ataruhusiwa kuuliza kwenye fungu hilo hilo mara moja tu, jambo moja. Haitakuwa mambo kadhaa Mbunge yule yule katika fungu lile lile.

Basi, kama nilivyosema mwanzo nadhani hatuna haja ya kueleza sana, mengi tunayafahamu. Kwa hiyo, sasa nadhani ni vizuri tukaanza. CCM mpaka sasa hivi sina jina hata moja kwa hiyo nasonga mbele au la sivyo kama kuna karatasi ilikuwa inanijia haijanifikia.

Katibu!

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Mwemnyekiti, tunaanza na Kitabu cha Pili, Matumizi ya Kawaida.

**MWENYEKITI:** Naanza na *CUF,* nani, Ahaa, Katibu. Katibu taja.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

Kif. 1001 – *Administration and HRM*...........Sh. 4,507,246,469/=

**MWENYEKITI:** Kama nilivyosema mwanzo, sasa tunaendelea. Mshahara wa Waziri hapo. Kwa hiyo, tunaanza na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo kwenye *Program 10, Administration* mshahara wa Waziri.

Nilipokuwa ninachangia kwa kuongea hapa Bungeni na pia kwa maandishi nilizungumzia suala la Serikali kutokutenga maeneo ya mifugo na wakati Sheria ya Ardhi inasema Waziri watashauriana waweze kutenga maeneo ya mifugo, yatengwe, yalindwe na yatangazwe kwenye Gazeti la Serikali na nikaelezea namna gani ambavyo sekta hii imekuwa haileti tija kutokana na kwamba mifugo inaonekana inazurura maeneo yote wakati sheria inasema wazi kwamba maeneo yatengwe na mpaka sasa hivi nikataka kujua kwamba Serikali itakuwa na mkakati gani kuhakikisha kwamba mikoa yote, wilaya zote ambapo mifugo ipo kunatengwa maeneo ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunategemea kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu angalau kama kiongozi Mkuu watuambie kuna mkakati gani wa kutenga maeneo ya mifugo ili tuone kwamba mifugo ambayo ni rasilimali ya Taifa inakuwa na maeneo na iache kunyanyasika kwa jinsi ambavyo sasa hivi mfugaji ananyanyasika, mifugo yenyewe inanyanyasika. Naomba majibu kwenye hilo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi wa jambo hilo Mheshimiwa Waziri wa Mifugo tafadhali, Mheshimiwa Mpina.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa swali hili zuri na nilijaribu kulieleza pale, lakini muda wangu ulikuwa mfupi sana kwa dakika saba nilizokuwa nimepewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni kwamba tayari kama Serikali tumeshajipanga vizuri sana kutekeleza ile sheria ya mwaka 2010 inayohusu malisho ya mifugo pamoja na chakula cha mifugo ili kuhakikisha kwamba maeneo kwanza yanapatikana, yanatambuliwa na yanasimamiwa kwa mujibu wa sheria hiyo.

Kwa hiyo, katika Halmashauri zote nchini, maeneo ya wafugaji yatatengwa na yatatambuliwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile nitaeleza kwamba hata maeneo ambayo yapo kwa Serikali kwa sasa ambayo mengine yapo upande wa *NARCO* tuna *Holding Grounds, LMU's* hizi zote zitatumika pia kuwaokoa wafugaji ambao mifugo yao inatangatanga huku na kule kwa kukosa malisho. Lakini vilevile nikasema kuna timu ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliiunda, timu ya Wizara tano ambayo tayari mapendekezo yake imekamilisha na imetoa jukumu kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, imetoa jukumu kwa Wizara ya Maliasili na Utalii, imetoa jukumu kwa TAMISEMI. Hawa wote wamepewa maelekezo namna ya kuhakikisha kwamba tunaondoa kero hizi za wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni ile kuhakikisha kwamba palipo na mifugo lazima maji yapatikane na hili Serikali ya Awamu ya Tano ndiyo kazi ambayo tutaifanya kubwa. Sasa kwa sababu hili jambo linahitaji maelezo marefu nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge kwa sababu Wizara ya Mifugo itawasilisha taarifa hii kwa kina, asubiri muda huo tutampa maelezo kwa kina ambapo kuna nafasi ya kutosha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Halima Bulembo, CCM.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana upo TAMISEMI, Wizara ya Vijana inashindwa kuwa na usimamizi wa moja kwa moja na Serikali inashindwa kuhakikisha Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya fedha husika kwamba inatoka. Serikali ina mkakati gani kuhakikisha fedha hizi ziwe zinatoka kuja kwetu vijana? Mfano mwaka 2017/2018 mapato ya halmashauri za ndani zote ilikuwa ni bilioni 680 ambapo asilimia tano ya vijana ukitoa katika

bilioni 680 unapata bilioni 34, zile hazijatoka kuja kwetu sisi vijana. Kwa hiyo, kama Mbunge wa Vijana ningeomba kwanza kabisa Serikali itengeneze *separate audit report* ya fedha za vijana na ziwe zinaletwa kila mwaka katika Bunge la Bajeti tukiwa tunajadili Wizara ya Vijana ili sisi tujue ni halmashauri zipi zimetoa na zipi ambazo hazijatoa ibaki kwetu sisi Wabunge kulia na Wakurugenzi ambao wanashindwa kutoa fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, ningeomba *commitment* kwa Serikali kwamba itahakikisha inaleta hizo ripoti kila mwaka katika Bunge la Bajeti ili kuhakikisha vijana tunaweza kujua ni fedha ngapi tunapata na zinatokaje. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI ufafanuzi tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipata vizuri hoja ya Mheshimiwa Bulembo na jambo hili lazima niseme kwamba hapa siwezi kusema nitatoa *commitment* isipokuwa kesho baada ya *presentation* yetu ya bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuna jambo kubwa sana linafanyika katika eneo hilo. Lengo letu kubwa tumekuja na mtazamo mwingine mpana zaidi wa jinsi gani vijana na wanawake wataweza kunufaika zaidi kupitia mfuko huu hata zaidi ya hivi sasa wanavyonufaika na kwa sababu sitaki ku-*pre empt* hotuba ya bajeti yangu ya kesho namuomba Mheshimiwa Halima Bulembo avute subira, jambo hili atapata fursa nzuri sana ya kulichangia na kupata ufafanuzi wa kutosha katika bajeti itakayowasilishwa kesho. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rashid Shangazi, CCM.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anahitimisha hoja iliyoko mbele ya Bunge lako amezungumzia namna ambavyo Wizara ya Sekta ya Kilimo inavyohusika katika kuboresha

mazao hasa mazao yale ya biashara. Lakini wote ni mashahidi hapa tunaona jinsi ambavyo zao la kahawa linavyozidi kupotea. Ni ushahidi ulio wazi kwamba Kilimanjaro ilikuwa inaongoza kwa kilimo cha kahawa, Mkoa wa Kagera ulikuwa unaongoza, Kigoma, Mbeya na kadhalika. Sasa tumeona hatua mbalimbali zinazofanyika katika baadhi ya mazao ikiwemo pamba, korosho na mengineyo. Lakini katika zao hili la kahawa hatujaona mkakati mahsusi ambao unaweza kwenda kulinyanyua zao hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nione Serikali inazungumzaje katika suala hili la kunyanyua kilimo cha kahawa ambacho kimepotea na kwa kweli kama sitapata majibu ya kuridhisha nina kusudia kushika shilingi katika mshahara wa Waziri. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo ufafanuzi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Naomba nimjibu Mheshimiwa Shangazi katika swali lake juu ya zao la kahawa ambalo ni zao mojawapo katika mazao ya mkakati yale matano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali na Wizara ya Kilimo, tumejipanga kisawasawa katika zao la kahawa na limekuwa lina mtafaruku kutokana na kwamba zamani kulikuwa na ule mpango wa wafanyabiashara kununua kahawa moja kwa moja kutoka kwa wakulima, lakini sasa hivi hilo zoezi kama Serikali tumelisitisha kutokana na kwamba *direct export* ambayo wale wafanyabiashara walikuwa wanaifanya kwa wakulima tumegundua kwamba wakulima wamekuwa hawanufaiki.

Kwa hiyo, tumeona kwamba vyama vya ushirika tuweze kuviimarisha na kwamba wafanyabiashara wote ambao wanataka kununua kahawa basi wanunue kahawa hii kupitia katika ule mnada wetu wa kule Moshi ili mkulima wa Kitanzania aweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge wengine wote tutakapokuwa tunawasilisha bajeti yetu hapa tarehe 15 Mei basi mpango na mkakati mzima wa kuhusu zao la kahawa, lakini vilevile na mazao mengine tuweze kuwaletea hapa na tuweze kuwapa ushauri kama Serikali tumejipanga vipi kuhakikisha kwamba mkulima wa Tanzania ananufaika katika kufurahia kilimo chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara ya Kilimo tumepanga kuzindua hivi karibuni mpango mkakati wa kilimo ambao pia utashirikisha Wizara nyingine zaidi ya sita na haya yote ni katika kuhakikisha tunaboresha kilimo cha Tanzania pamoja na wakulima kwamba wananufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa MWenyekiti, naomba Mheshimiwa Mbunge asitoe shilingi yake ili awe na uhakika na Serikali ya Awamu ya Tano. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kwamba inawezekana Mheshimiwa Naibu Waziri hajanielewa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hoja yangu iko kwenye uzalishaji na yeye amejikita zaidi kwenye soko. Tunachozungumza, sasa hivi kuna mabadiliko ya tabianchi, hiyo kahawa yenyewe haikui, kwa hiyo, tulitaraji kwamba Wizara hii ingekuja na mkakati kupitia vituo vya utafiti, wafanye utafiti kwamba kwa hali ya hewa iliyopo sasa ni aina gani ya kahawa ambazo tupande ili ziweze kuleta tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Bunge lako angalau unipe nafasi Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono tuweze kulijadili jambo hili. Naomba nitoe hoja Waheshimiwa Wabunge tuweze kulijadili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi, sasa mtajadili nini wakati Wizara ya Kilimo inakuja? Si tarehe 15 Mei kesho kutwa tu? *(Kicheko)*

Nakushukuru sana. Mheshimiwa Saed Kubenea.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru...

**MWENYEKITI:** Mliounga mkono mko watatu, yaani hata haiswihi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Kubenea tafadhali.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia hiyo au?

**MWENYEKITI:** Ulijiandikisha katika kuuliza maswali ya kisera au?

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchaguzi huru na haki ni jambo ambalo linasaidia utengemano katika Taifa letu. Katika maoni ya Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria walieleza umuhimu wa Tume ya Uchaguzi kuwa chombo huru ili kiweze kuaminika miongoni mwa jamii. Tume yetu ya Uchaguzi sio chombo huru kwa kuwa baadhi ya wasimamizi wa uchaguzi au karibu wote ni watu ambao wameteuliwa na Rais na Tume yenyewe haina wafanyakazi wake katika ngazi ya majimbo na ngazi ya kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi katika Katiba yetu Ibara ya 74 imeeleza wazi kwamba watu wasiohusika na uchaguzi wasioruhusiwa kuwa wajumbe wa Tume ya Uchaguzi ni pamoja na viongozi wa vyama vya siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini upo ushahidi ulio wazi kwamba baadhi ya makada wa Chama cha Mapinduzi

ndiyo wasimamizi wa uchaguzi katika majimbo yetu ya uchaguzi. Kwa msingi huo naomba kauli ya Serikali, ni lini italeta Bungeni Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili kukifanya chombo hiki kiwe huru na kinachoweza kuaminika miongoni mwa wadau wote wa uchaguzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitapata majibu yakinifu, ninakusudia kutoa shilingi ili jambo hili liweze kujadiliwa. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tafadhali. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili liko Mahakamani na kwa hiyo, haliwezi kujadiliwa katika Bunge hili, ahsante. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kubenea. Kwa taarifa hiyo bado unataka kuendelea. Eehe, unasemaje?

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo! Kilichokuwepo Mahakamani ni juu ya watu walioshiriki katika kupiga kura, kusimamia uchaguzi. Ninachozungumza kimeelezwa vizuri kwenye Tume ya Jaji Francis Nyalali ya mwaka 1991, Tume ya Jaji Robert Kisanga mwaka 2003, Tume ya Mabadiliko ya Katiba iliyoundwa chini ya Jaji Joseph Warioba na Bunge Maalum la Katiba kwamba ni lazima Tume ya Uchaguzi ifanyiwe marekebisho ili iendane na matakwa ya mfumo wa vyama vingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo jambo lolote Mahakamani hakuzuii Serikali kuleta Muswada Bungeni na mifano ipo hai. Kuna kesi ya kupinga sheria ya magazeti ya mwaka 1976 ilikuwa Mahakamani lakini Serikali imeleta Muswada Bungeni wa sheria mpya ya magazeti nayo imepitishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo suala hili naomba lijadiliwe ili Bunge lako litoe tamko/Serikali itoe tamko, lini italeta hapa Bungeni Muswada wa kubadilisha Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kwa msingi huo naomba kutoa hoja na naomba niungwe mkono na Wabunge wenzangu.

**MWENYEKITI:** Jamani, ni jambo la kikanuni, tunalifahamu kwamba tukitaarifiwa kwamba jambo lipo Mahakamani...

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**MBUNGE FULANI:** Sasa si umeongea hiyo?

**MWENYEKITI:** Eeh, lazima mihimili hii isiingiliane jamani. Lazima tuheshimu uhuri wa Mahakama. Kwa jinsi hiyo tunaendelea. Mheshimiwa Oscar Mukasa. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya maeneo ambayo Serikali imefanya kazi nzuri sana mpaka sasa ni eneo la madawa ya kulevya kwa maana ya sheria, lakini na utekelezaji wa sheria hii. Mifano tumeishikia na tumemsikia Mheshimiwa Jenista ametuambia tumetambuliwa hata Kimataifa. Lakini kwa bahati mbaya, moja ya matokeo ya kazi hiyo nzuri ni kuzalishwa kwa warahibu wengi (watu ambao walikuwa wanatumia madawa ya kulevya sasa wanaacha).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa changamoto yake ni kwamba zinahitajika *sober houses* za kutosha. Ukizingatia kwamba kwenye bajeti *vote* ya Kamisheni ya madawa ya kulevya hakuna bajeti ya maendeleo.

Nataka kusikia *commitment* ya Serikali kwenye ujenzi wa *sober house* ili tukabiliane na ongezeko la hawa watu vinginevyo tunakuwa tunachota maji na kuyamwaga badala ya kuyahifadhi unapotaka. Nakusudia kushika shilingi kama sitapata maelezo ya kujitosheleza. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ufafanuzi tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mheshimiwa Oscar na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya UKIMWI kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakitusaidia sana kishauri Serikali kuhusu eneo hili la dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana sana na Mheshimiwa Oscar kwamba toka mamlaka ilipoanza kufanya kazi imeweza kufanya kazi nzuri sana katika maeneo yote matatu ya kimsingi katika mapambano ya dawa za kulevya nchini kwenye eneo la *supply,* kwenye eneo la *demand* na kwenye eneo la *harm reduction,* maeneo haya yote yamefanyiwa kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume hii ndio kwanza imeanza kufanya kazi na sasa hivi ina takribani mwaka mmoja tu toka imeanza kufanya kazi, pamoja na matokeo hayo mazuri ambayo yameweza kutufanya nchi yetu itambulike kwenye medani za kimataifa. Kwa hiyo, tulichokifanya kwa mwaka huu wa fedha, tumeamua kwanza kuongeza bajeti kwenye Tume, ili iweze kukidhi mfumo mpya wa tume ambao umejengwa kwa mujibu wa sheria ya mwaka 2015 na mabadiliko yake ya mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninafurahi kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba ni muda mfupi tu uliopita mimi na timu nzima ya mamlaka tulishiriki mkutano wa kimataifa kule Vienna kuhusiana na mapambano dhidi ya dawa za kulevya na nchi yetu imepata heshima kubwa kama nchi ya mfano katika mapambano haya na moja ya uthibitisho wa kazi hiyo nzuri katika nchi yetu ya Tanzania, mwaka huu mwezi wa tisa tutapokea ujumbe wa mkutano mkubwa wa kimataifa wa viongozi wanaopambana na dawa za kulevya katika Bara zima la Afrika utafanyika Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kazi ambayo ni *specific* tuliifanya kule ni kujaribu sasa kutengeneza mfumo wa miradi ya maendeleo ambayo tutaipa picha ya *alternative development* kwa maana ya kwamba maeneo yale ambayo yameonekana yakikithiri kwa kulima mazao ambayo ni dawa za kulevya kama bangi na mirungi tuweze kutafuta mazao mbadala na kuyapeleka katika maeneo hayo, ili vijana waache kulima dawa za kulevya wajikite katika mazao mengine ya kibiashara ya kuwaongezea uchumi. Ninaomba nilihakikishie Bunge lako tukufu huko tunakokwenda tutaendelea kutenga hiyo bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza hapa kuhusu suala la *sober house;* tumeshakamilisha miongozo ya kuhakikisha kwamba *sober house* ambazo zinamilikiwa na watu binafsi ziendeshwe kwa miongozo maalum ili kutoa tiba inayotakiwa na sio kuiendesha kibiashara kama ilivyokuwa inafanyika nyuma na sisi kama Serikali tumeanzisha *centre* ya kitaifa hapa Dodoma na imekwishakujengwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshaweka jiwe la msingi, tunataka kuitumia kama *centre* ya kufanya *rehabilitation* kwa wale ambao tayari walishakumbwa na tatizo la urahibu, ili waweze kuondokana na matumizi ya dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *centre* hiyo hapa Dodoma tutaanza pia kufundisha shughuli za ufundi stadi kusudi kuwafanya wakishaondoka kwenye urahibu warudi wakafanye shughuli za ufundi stadi na kuweza kufanya miradi yao midogomidogo na kuweza kujiajiri kama wanavyojiajiri Watanzania wengine. Kwa hiyo, naomba kukuhakikishia Ofisi ya Waziri Mkuu inafanya kazi nzuri sana katika eneo hili la dawa za kulevya na ndio maana hata medani za kimataifa zimeona kabisa kazi nzuri ya Serikali yetu katika eneo hilo na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akitujalia tukiendelea hivyo, basi huko tunakokwenda tutakuwa tumepiga hatua kubwa zaidi na tutaweza kuwa na bajeti ambayo ni endelevu inayoweza kusaidia maeneo yote mawili. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Oscar Mukasa wewe ni Mwenyekiti.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhika.

**MWENYEKITI:** Eeh! Kwa kweli. Wewe ni Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI na Dawa za Kulevya kwa hiyo, na Mheshimiwa Waziri muendelee ku-*pursue* kupitia Kamati yetu ya Bunge yatokanayo na baadhi ya mambo ambayo mnaona yanahitaji kurekebishwa na kuwekwa sawa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Venance Mwamoto, hayupo! Eeh, haya, Mheshimiwa Felister Bura.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, nchi yetu hukumbwa na maafa ya mara kwa mara na kwa wakati usiotarajiwa; na wakati mwingine maafa haya hupoteza maisha ya watu na mali zao na kuwarudisha watu katika umasikini uliokithiri na tumeshuhudia maafa ya mafuriko maeneo mbalimbali na wakati mwingine maafa ya moto.

Na kwa kuwa, kwa sasa hakuna *centre* kubwa ambayo inashughulika na maafa yanapotokea na wananchi wanashindwa wakimbilie wapi kutoa taarifa hizi kwa sababu, *centre* kubwa ya kutoa taarifa hakuna; na kwa kuwa, Dodoma ndio Makao Makuu ya nchi yetu kwa sasa, na katika bajeti ya Waziri Mkuu aliyoisoma sikuona mahali ambapo Serikali inatarajia kujenga *centre* kubwa ambayo itasimamia masuala ya maafa yanayowapata wananchi.

Je, Serikali inasema nini katika hili la kujenga kituo kikubwa cha maafa hapa Dodoma? Na nisipopata majibu ya kuridhisha nitatoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ufafanuzi tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninampongeza

Mheshimiwa Felister Bura na hasa anavyoitizama Dodoma kwa jicho kubwa zaidi na jinsi itakavyotakiwa Dodoma ifanane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015 tulifanya mabadiliko makubwa ya sheria ambayo itaratibu suala zima la maafa katika nchi yetu ya Tanzania. Sheria ile ilisababisha tujiandae kutekeleza majukumu kadhaa ya kimsingi ambayo yanajitokeza wazi katika sheria hiyo ya mwaka 2015, pamoja na jambo ambalo nitalitolea majibu lililoulizwa na Mheshimiwa Mbunge, ilikuwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba kwanza tunaziimarisha Kamati za Maafa katika ngazi za wilaya na mikoa kwa kuzipa mafunzo na kuhakikisha kwamba, zinatambua majukumu yake pale inapotokea tatizo hilo la kimsingi la maafa katika maeneo husika na hatimaye katika hatua ambayo inakuwa ni nje ya uwezo wa ngazi ya wilaya na mkoa basi, utaratibu wa kimuundo wa kiutekelezaji unaratibiwa pia, na Kamati ya Maafa ambayo iko kwenye ngazi ya Taifa kwa kutegemea sheria inavyosema na matamko ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati wa utekelezaji wa sheria hiyo, sheria imeagiza pia, ni lazima nchi ijitosheleze kwa kuwa na kituo kikubwa ambacho kitakuwa ni *Centre for Emergency* katika nchi yetu ya Tanzania. Tulichokifanya mpaka sasa ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu na hasa baada ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuratibu zoezi la kuhamia Dodoma, kwa hiyo, tulichokifanya tumeanza kutafuta eneo ambalo tumeshalipata, Miyuji, eneo ambalo litajengwa hicho kituo kikubwa cha maafa, *inshallah* Mwenyezi Mungu akitujalia huo uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu tumeshapitisha tayari malipo ambayo yanatakiwa tuyafanye ili tuweze kutwaa kiwanja hicho na kikamilikiwa kwa ajili ya shughuli hiyo maalum. Lakini vilevile Ofisi ya Waziri Mkuu imeanza kufanya mazungumzo na marafiki wa nje, lakini kuangalia pia uwezo wa ndani ya nchi ambao utatusababishia sasa kuanza kujengwa kwa kituo hicho kwa kazi hiyo maalum kabisa ya kukabiliana na majanga ya

maafa katika nchi yetu ya Tanzania. na kituo hicho tunategemea kama Mungu atajalia tukifika kuweza kukijenga, basi tunataka kiwe ni kituo cha mfano katika Afrika Mashariki, lakini ikiwezekana kwenye Bara zima la Afrika kwa hiyo, tumeanza kazi hiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Bura, bado tena? Haya kwa haraka haraka.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa maelezo yake, lakini hajasema *specific* kwamba ni mwaka gani? Kwenye bajeti yao hawajatenga fedha, hakuna fedha za fidia, hakuna fedha za kuanza kazi, atuambie ni lini wanaanza? Waheshimiwa Wabunge asiposema kipindi, basi naomba mniunge mkono, ili suala hili lijadiliwe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimia Waziri wa Nchi ni lini? Kifupi kabisa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mara tutakapokuwa tumekamilisha kujenga uwezo huo wa ndani wa kibajeti na vilevile tutakapokuwa tumeweza kushirikiana na marafiki wetu katika maendeleo tutatoa taarifa na hivyo shughuli hiyo itaanza kutekelezwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa. Katiba yetu Ibara ya 63(2) inaelezea kuhusu chombo hiki ambacho ni Bunge kwamba, ndio chenye mamlaka au ndio chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano cha kuisimamia Serikali na kushauri. Lakini vilevile kanuni zetu Nyongeza ya Pili inaelezea kuhusu vyombo vya Bunge vya uwakilishi katika Mabunge mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kujenga hoja hii ili niweze kuelezea ni namna gani Bunge letu linakosa hadhi mbalimbali na niseme tu kwamba Bunge hili linawakilishwa

katika Mabunge mbalimbali, likiwemo Bunge la Afrika, Bunge la Dunia kwa maana ya *Inter Parliamentary Union, ACP, EU* na mengine mengineyo. Lakini kwa muda mrefu Wabunge au wawakilishi hawa wameshindwa kwenda kuwakilisha kwenye Mabunge hayo kwa sababu ambazo wawakilishi hawa bado hawajazijua, ama ni tatizo la fedha ama ni tatizo la kibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukisoma pia katika hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ameongea na kusema kwamba wawakilishi hawa wameshiriki, jambo ambalo si kweli. Kwa mfano *ACP* mwaka jana Disemba hawajashiriki na mwaka huu pia, Machi hawajashiriki. *IPU* mwaka huu mwezi wa tatu walipaswa kuwa Geneva, lakini hawakufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua ni sababu zipi zinazosababisha Wabunge/wawakilishi ambao wamechaguliwa na Bunge hili kushindwa kwenda kuwakilisha wakati kuna nchi mbalimbali, ndogo tu kiuchumi, zinaweza kwenda? Na nisipopata majibu ya kuridhisha nitaomba niungwe mkono kwa kushika shilingi ya Waziri Mkuu, jambo ambalo sio jema sana.

**MWENYEKITI:** Ninapata taabu kidogo Mheshimiwa Susan. Swali ambalo *actually* ni la Bunge, sasa unataka Waziri alijibu.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyojua Mheshimiwa Jenista ni Waziri anayeshughulika na Uratibu na Bunge na hata hivyo, kwenye hizi hotuba zote na kasma inaonesha iko chini ya Waziri Mkuu, *unless otherwise,* lakini nilijua hivyo na ndio sababu wamewasilisha katika mjadala uliopita. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri haya, jibu mambo ya Bunge.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa

Mwenyekiti, ninaomba tu nijibu swali hili la kimsingi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utendaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa maana ya Uratibu wa Shughuli za Bunge unachukua taswira tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taswira ya kwanza ni haki na mfumo mzima wa utendaji kazi wa Bunge na Shughuli za Wabunge ambao unasimamiwa na Tume ya Huduma za Bunge ndani ya Bunge letu tukufu. Lakini kazi yangu nyingine kubwa mimi, kama Waziri sasa kwenye Bunge hili, ni kuhakikisha kwamba Serikali inatenga fedha na kutoa fedha kwa Bunge, ili Bunge liweze kuendesha shughuli zake bila kukwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nilihakikishie kwanza Bunge lako tukufu kwamba kwa kipindi hiki na Mheshimiwa Spika, nadhani utakuwa ni shahidi kwa sababu, wewe ni kiongozi wetu wa Bunge, Serikali imekuwa ikitoa fedha zote ambazo amekuwa akihofu Mheshimiwa Mbunge kama zimekuwa zikitolewa na Serikali kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Bunge, zimekuwa zikitolewa bila kukwama na fedha zote zimeingia kwenye Mfuko wa Bunge kama ilivyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu wa fedha ambao sasa ndio tunajadili hapa mbele yako, ukienda kwenye *Vote* ile ya 42, ukienda *sub vote* 3006, kifungu ambacho huko mbele ninawahisha shughuli kama kwa ridhaa yako unaruhusu kipengele ambacho kinazungumzia *International Relations and Protocal* kimetenga tena fedha ya kutosha kwa ajili ya safari za Wabunge nje ya nchi, ikiwemo uwakilishi huo katika taasisi mbalimbali za kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, upande wangu kama Waziri ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kama ni suala la fedha, fedha hizo zimetengwa na kama ni masuala mengine ya kuhudumia Waheshimiwa Wabunge nadhani shughuli hizo

zote kwa kusimamiwa na tume mambo yote yanayohusu Bunge na Wabunge yamekuwa yakiratibiwa sawasawa katika kipindi hiki ambacho tunamaliza. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na kumbe nilikuwa sahihi kwamba anayajua haya mambo. Naomba sasa nipate ufafanuzi wa kina, kama Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba fedha zipo, lakini Wabunge toka Disemba nilivyosema hawajaenda na hata mwaka huu hawajaenda. Sasa kama tatizo sio fedha, naamini tatizo litakuwa ni kibali. Sasa nilikuwa naomba kujua kwa nini kama ni kibali, na ninatambua kwamba kibali kinatolewa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha kuona kwamba, muhimili mkubwa kama huu unaombewa kibali kwa Rais, wakati hata ma-*VC* wa vyuo mbalimbali sasahivi, *according to* kwenye Kamati tuliambiwa kwamba, ma-*VC* baada ya kuona kwamba watu wanaoenda kufanya *research* wanapata shida ya kuondoka nchini, ma-*VC* wamepewa kibali kwamba wanaweza wakatoa ruhusa kwa wafanyakazi kwa maana ya Wahadhiri kwenye vyuo vyao.

Ni kwa nini basi Bunge ambalo ni muhimili ambao unatakiwa kuisimamia Serikali, wenyewe nao upate kibali, uombe kibali kutoka kwa Rais, jambo ambalo mimi nadhani labda hii ndio sababu tunaonekana kwamba, Bunge linakuwa linakosa hadhi. Nilikuwa naomba pia nipate ufafanuzi kama sio fedha, tatizo hasa ni nini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hiyo ni hofu ya Mheshimiwa Mbunge na ninaomba tu nisema kwamba hakuna ambaye amesimama hapa na kusema, anasema yeye kwamba anachodhani labda shida ya ruhusa ya safari hizi ni vibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba kama fedha za kusafiria zipo kama zinavyojionesha katika vitabu ambavyo tunavyo ninaamini kabisa kwamba jambo hili liko ndani kabisa ya uwezo wetu na uwezo wako na si jambo la kuleta mgogoro mkubwa sana miongoni mwetu na ninaamini kabisa sisi kama Serikali tukishatenga hizi fedha, fedha hizi zitatumika kwa kuzingatia mahitaji yaliyotengwa kwa mujibu wa bajeti ambayo Bunge limeomba na limeidhinishiwa na fedha hizi zikiwa zimeshatolewa kwenye Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama Waheshimiwa Wabunge wanaona kwamba, yako matatizo mengine yanatakiwa kujadiliwa ndani ya Serikali na kupata ufumbuzi, sisi kama Serikali hatuna shida. Tuko tayari na tutakutana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba niwahakikishie kwamba, hakuna shida wala mgogoro mkubwa ambao utaweza kutusababisha kulichukulia jambo hili kama ni jambo kubwa ambalo lina shida ndani ya Bunge na ndani ya Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, lakini kabla hatujaendelea nilazimike kidogo, kwa sababu kwa kweli hili ni la Bunge zaidi kuliko Serikali. Kwa hiyo, ni vizuri zaidi kutumia *forum* nyingine za Kibunge kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Kwanza picha inayotolewa kwamba hawasafiri kabisa, si picha sahihi, mara ya mwisho nilikuwa mimi mwenyewe na Mheshimiwa Susan, tulikuwa St. Petersburg, kule Russia, eeh! Hao ni Wajumbe wa *Inter Parliamentary Union. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wale Wajumbe wa *SADC PF* mara ya mwisho nilikuwa nao Namibia; Wajumbe wa *PAP* mara ya mwisho mlienda Johannesburg; Wajumbe wa *ACP* mara ya mwisho mlienda Brussels na Wajumbe wa *CPA* mara ya mwisho walienda Nigeria. *(Makofi)*

Kwa hiyo, safari zimekuwepo lakini wakati mwingine inaweza zikakosekana kwa sababu fulani fulani. Inawezekana wakati wa safari umefika, lakini fedha kutoka Hazina kwa wakati huo haijaingia na tarehe ya mkutano ikapita. Haya ni mambo tu ya kiufundi ya ndani. Ndiyo maana nikasema haya ni yetu wenyewe, ni bora tusimtwishe sana Mheshimiwa Waziri, hawezi kujua baadhi ya mambo mengine kama hayo madogo wadogo. *(Makofi)*

Pia niseme kwa kweli wanaosafiri miongoni mwa Waheshimiwa Wabunge ni kikundi kidogo sana, yaani sijui kama wanazidi 20; ni hao hao wa makundi hayo niliotaja wa Mabunge mengine. Bunge la Afrika, Bunge la *PAP, IPU, SADC PF, CPA* na *ACP,* hakuna safari. Ndiyo! Kwa hiyo, kelele zote mnazosikia ni za hao hao ambao ninyi wenyewe mliwachagua hapa kuwa wawakilishi. Wakati mwingine nao inabidi watulie kidogo, mbona ninyi hamwendi kokote! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Hamidu Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Nne ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ilianzisha mpango wa uendelezaji wa miradi ya gesi, lakini ilikwenda sambamba na mradi mkubwa wa *LNG* pale Lindi na Serikali ya Awamu ya Tano ukaendeleza ule mradi. Kuanzia mwaka 2017 mpaka mwaka huu wa 2018 ule mradi kama ume-*cease*, hatuoni maendeleo ya ule mradi na ni mradi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichokuwa kibaya zaidi ni kwamba gesi imegunduliwa karibu na mpakani na Msumbiji; na Msumbiji wameanza kufanya *LNG* na gesi ni bidhaa inayoweza kuhama kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Sasa hatari iliyopo ni kwamba sisi tunaweza tukawa tunaamini kwamba gesi bado ipo ya kiwango hicho, lakini wenzetu wa Msumbiji kwa sababu tayari wameanza

kuendeleza ule mradi na wanafanya mpakani kabisa na Tanzania, inawezekana wao wakaichukua gesi yote iliyoko Tanzania na mwisho wa siku tukija kushtuka gesi hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua, Mradi wa *LNG* umekwama wapi? Naomba maelezo ya kina juu suala hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati, ufafanuzi tafadhali.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru suala la Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na hali halisi ya mradi wa *LNG,* ingawa wakati wa bajeti yetu tutaeleza zaidi lakini ni vema nikaeleza kwa ufupi na asubuhi nilidokeza kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa mradi wa *LNG* haujakwama popote. Ni vizuri sana Mheshimiwa Mbunge akajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili, hii miradi ya gesi na miradi ya madini inafuatana sana; huwa inakwenda kwa mtandao wa *vain*. Kwa hiyo, ni kweli kabisa Tanzania tuna gesi na Msumbiji nao wana gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haina sababu kwamba kwa vile nao Msumbiji wanaendeleza mradi wa *LNG*, mradi wa *LNG* Msumbiji sasa unafanya wa Tanzania ukwame. Mradi wa Tanzania uko pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi nimeelezea hali halisi, hatua tuliyofikia. Yako mambo ambayo yamekamilika na yako mambo yanayoendelea. Mradi wa *LNG* tulianza hapa nchini mwaka 2015 na kazi zilizokuwa zinafanyika zilikuwa zinaonesha *physical work* mwanzoni. *Physical work* zilikuwa zinajumuisha kupatikana kwa eneo. Kwa hiyo, kulikuwa na bubujiko bubujiko la watu kuonekana wapo *site*. Jambo la pili, ilikuwa ni kufanya tathmini ya udongo wa mradi. Kwa hiyo, ilikuwa inaonekana wataalam na wakandarasi

wako *site*. Jambo la tatu, ilikuwa ni tathmini ya wananchi walioko pale kwa ajili ya fidia. Kwa hiyo, ilikuwa inaonekana makampuni yanapitapita yako *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua tuliyofikia sasa hivi ni kujadiliana sasa namna ya uwekezaji ambapo watu huwaoni *site*. Kwa hiyo, haina maana kwamba mradi umetelekezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana watalaam wetu *(Government Negotiating Team)* walikutana na *Statoil* na leo saa 8.00 wanakutana na *DG Shell* kujadiliana uendekelezaji wa mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huu mradi haujasimama. Katika bajeti yetu tutaeleza zaidi ni kiasi gani cha fedha tumetenga na Waheshimiwa Wabunge tukiwaomba sana mpitishe ili mradi huu tuuharakishe zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi tu haujakwama. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, sisi tunachotarajia kama Bunge mwakani hatutaki kusikia kiswahili cha kujadiliana, sijui kufanya hivi; kwa sababu kwa kweli ni uchumi mkubwa. Gesi ni uchumi mkubwa utakaotusaidia sana.

Kwa hiyo, kwenye bajeti ya mwakani, maneno yako haya tunayachukua mwaka huu, lakini mwakani, kwa kweli kama bado mnajadiliana kidogo patakuwa moto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jitu Soni, aah, Mheshimiwa Bobali bado? Bado nini tena? Msumbiji haiwezi kuchukua gesi huku. Haya Mheshimiwa Bobali. *(Kicheko)*

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakubaliana kabisa na maneno yako kwamba hii aina ya *commitment* ambayo Serikali wanaifanya leo, basi tuione kwenye vitendo mwakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tathmini imefanyika muda mrefu sasa na mjue kwamba yale maeneo ni ya wananchi na wananchi wameacha kuyaendeleza. Sasa tunapoendelea kusema kwamba bado majadiliano yanafanyika, watu hawapo *site* na wananchi hakuna wanachokiona, inaingia shida nyingine sasa hivi kwamba kuna watu wengine wanakwenda, mtu amekaa muda mrefu wanakwenda kununua yale maeneo ya wananchi tena. Ndiyo jambo ambalo sasa hivi nataka kulisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo hayo uliyoyasema, ni vema Mheshimiwa Waziri akatoa *commitment* hapa kwamba ikifika mwaka mmoja hakuna tena, wananchi hawajalipwa, basi wananchi waendeleze watakavyoona. Kwa sababu tukiacha kuendelea tu hivi hivi tutawatia umaskini, mtu atashindwa kuendeleza mashamba yale, kuna mikorosho pale, watu hawaendelezi mashamba yao ya mikorosho wakisubiri kulipwa, hakuna sasa kinacholipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka niongezee hapo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bobali, nakushukuru sana. Na mimi nafikiri yote uliyoongea tunakubaliana sote, ndiyo maana tumesema, Mheshimiwa Waziri *commitment* ni hii tunayomwambia.

Sisi tumemwambia kwamba mwakani lugha hiyo tena tusiisikie. Sasa mnataka atuambie nini? Apime nini tena hapo? Ndiyo Bunge tumeshaagiza hivyo. Kwa kweli kutoka rohoni kabisa na mimi naamini kabisa ni mchapakazi, hawalali, lakini *they have to speed up,* haya maneno yatatuweka mahali ambapo hatutaeleweka kabisa. Lazima hili jambo la gesi lieleweke, linafanyikaje na kadhalika. Watu usiku na mchana, hii Wizara ilikuwa moja, sasa zimekuwa mbili tofauti, kwa hiyo, ina maana *speed* inapaswa iongezeke na Watanzania wote wanatarajia hayo kwa kweli.

Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuiuliza Serikali kutokana na Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo mratibu wa shughuli zote Serikali, naye ndiye Mkuu wa Serikali, ni lini sasa Serikali italeta mabadiliko ya sheria hapa Bungeni ili Waziri wa Fedha aweze kutoa msamaha wa kodi katika miradi ya kitaifa, lakini pia katika miradi inayohusu jamii ambayo ina maslahi ya jamii ambayo miradi mingi inakwama kutokana na msamaha huo kutokupatikana? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jitu unapouliza swali, hebu fafanua kidogo. Miradi ya kitaifa ya aina gani? Miradi ya kijamii ya aina gani? Ili Mheshimiwa Waziri aweze kuelewa unachokiuliza.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, miradi ya kijamii kwenye Majimbo yetu au katika taasisi mbalimbali tunaweza tukapata wafadhili ambao wanataka kutoa fedha zao lakini hawapo tayari kulipa kodi. Ile ni miradi ambayo ni moja kwa moja katika hospitali zetu, zahanati, *ambulance* au barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika miradi ya Kitaifa ni fedha ambazo nchi ziko tayari kutoa mkopo kwa nchi yetu. Kwa mfano, miradi ya kitaifa ya maji, lakini inakwama kutokana na kwamba fedha zile zinatakiwa zilipiwe kodi ambapo wanatoa kwa gharama nafuu na riba nafuu na kwa muda mrefu. Sasa jambo hilo lingekuwa halipo na Mheshimiwa Waziri angekuwa anaruhusiwa kutoa msamaha wa kodi kwa mfumo maalum ambapo haiwezi kutumika vibaya, ingekuwa ni maslahi kwa Watanzania wote, lakini pia kwa Serikali yenyewe kwa sababu miradi yote ambayo imekwama ingekuwa sasa haijakwama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ufafanuzi tafadhali.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nijaribu

kutoa ufafanuzi. Jambo la kwanza, Bunge lako hili linakumbuka kwamba miaka michache iliyopita tulikuwa na changamoto kubwa sana kwamba kiasi cha misamaha ya kodi ambacho kilichokuwa kinatolewa kilikuwa ni kikubwa mno kulinganisha na nchi nyingine zinazotuzunguka. Bunge hili hili likafanya uamuzi kwamba ni muhimu sana tupunguze misamaha ili kuziba mianya ya uvujaji wa mapato kupitia eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ninamwelewa Mheshimiwa Mbunge aliyetoa hii hoja, kwamba yako maeneo ambayo yana shida kidogo. Mwaka 2017 Bunge hili kwa upande wa *VAT* liliruhusu kwamba Waziri wa Fedha anaweza akatoa misamaha, lakini ni muhimu na lazima apate Kamati ambayo inamshauri kuhusu kutoa msamaha huo na hayo yanafanyika kwa miradi ambayo inapata fedha za wafadhili kutoka nje. Bado sehemu ya kodi ya mapato ambapo naweza nikatoa msamaha kama Baraza la Mawaziri litaridhia hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo mengine madogo madogo ambayo yafaa niseme tu kwamba namwomba Mheshimiwa Jitu asiharakishe mchezo, kwa sababu mapendekezo ya mabadiliko ya sheria zote za kodi yatawasilishwa wakati wa kuleta hapa *Finance Bill, 2018* na mabadiliko hayo ni pamoja na maboresho ya misamaha ya kodi. Avute subira kidogo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Mheshimiwa Jitu vuta subira.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mwisho ni Mheshimiwa Omary Mgumba.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu

kutaka ufafanuzi kwa Serikali kuhusu uendelezaji wa zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la *export levy* lilikuwa ni kuwakatisha tamaa wale wafanyabiashara wanaouza korosho nje ya nchi bila kubanguliwa hapa nchini. Suala hili lilianza tangu Serikali ya Awamu ya Pili mwaka 1995 wakati tunafufua zao hili la korosho baada ya mihangaiko tuliyoipata katika miaka ya 1970 na 1980. Mwaka 1995 iliwekwa 3% ya *export levy* kwa ajili ya kufanya hiyo *discourage*; mwaka 2000 tukaweka 5%, baada ya kuona korosho bado inaenda ghafi nje ya nchi; mwaka 2006 tukaweka 10%, bado korosho inaenda nje ya nchi haibanguliwi hapa nchini; mwaka 2009 ambapo tulifikia uzalishaji wa tani 100,000 na hapa ilikuwa zaidi ya tani 40,000 ilikuwa inabanguliwa ndani hapa. Ikabidi tuongeze kutoka asilimia 10 mpaka asilimia 15 mpaka sasa na inaingiza mapato mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimeona katika hotuba ya Waziri Mkuu na uliona mjadala ulivyokuwa kwamba hizi fedha za *export levy* zinaingia lakini hazirudishwi kutimiza yale malengo mahususi yaliyokusudiwa. Kwa mfano, lengo kubwa lilikuwa kwa ajili ya kufanya utafiti, kwa ajili ya kutoa ruzuku, kwa ajili ya kuongeza uzalishaji kupitia miche pamoja na pembejeo, lakini pia kutoa ruzuku kwa wabanguaji wa ndani ili waweze kupunguza gharama za uzalishaji; vilevile kujenga miundombinu ya kuhifadhia zao la korosho kama maghala na vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea sasa hivi, zile hela za *export levy* zimekwenda Hazina, hazitekelezi yale yaliyokusudiwa. Nataka *commitment* ya Serikali kwa ajili ya kuendeleza zao la korosho na viwanda vya ndani na kuhakikisha hii korosho inabanguliwa hapa nchini kutoa ajira na kuongeza thamani na uchumi wa nchi yetu. Nini *commitment* ya Serikali katika suala hili la *export levy? (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anachoeleza Mheshimiwa Mbunge, hii asilimia 65 ya *export levy* imewekwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina na tatizo lililojitokeza ni kwamba kwenye mfumo wa mapato, fedha hizi zilikuwa zinaonekana lakini kwenye mfumo wa matumizi fedha hizi tofauti na mifuko mingine hizi fedha zilikuwa hazionekani. Kwa hiyo, kilichofanyika kwa mwaka huu ni kuziwekea utaratibu mzuri ili kuhakikisha kwamba fedha hizi za umma zinaonekana kwenye matumizi ili tuweze kujiridhisha na matumizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alilieleza kwamba tayari Hazina imesha-*release* shilingi bilioni 10 ambazo zinapitia *TFC* kwa ajili ya ununuzi wa *sulphur,* lakini pia viatilifu vingine na fedha zilizobaki zitafuata pia utaratibu huo. Kwa hiyo, *commitment* ya Serikali ni ile ile kwamba fedha za mfuko, *export levy* zitaendelea kutumika lakini zifuate utaratibu ulioainishwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mgumba, nimekuona.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini bado halijakaa sawa sawa. Kama nilivyosema, lengo kubwa la *export levy* ilikuwa ni kuhakikisha korosho yote inayolimwa hapa nchini inabanguliwa ndani ya nchi. Sasa amesema kwamba hizi pesa ambazo zilizohifadhiwa kwenye Mfuko Mkuu na zilizotolewa shilingi bilioni 10 tu, lakini zimekusanywa zaidi shilingi bilioni 60. Sasa labda anatuhakikishia vipi wadau wa korosho na wakulima wa korosho, hizi hela kama zimehifadhiwa ziko maalum kwa ajili ya uzalishaji, je, zitarudishwa baada ya utaratibu huu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mgumba huulizi maswali tofauti na pale mwanzoni? Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nirudie tena, fedha hizi ni za umma. Kwa hiyo, utaratibu wa kuziweka na kuhakikisha

kwamba matumizi yale ni matumizi yanayokubalika kwa mujibu wa kanuni na taratibu, ndiyo kinachofanyika. Kwa hiyo, shilingi bilioni 10 zimeshatoka na hizo nyingine zizingatie utaratibu. Kama utaratibu wa matumizi ukizingatiwa, hakuna tatizo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Upande wa masuala ya kisera tumekamilisha. Mheshimiwa Pauline Gekul ulisema una kifungu maalum *(specific)* hapo hapo.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nimeshaona hizo shilingi milioni 700 ni kwa ajili ya wafanyakazi kutoka Dar es Salaam kuhamia Dodoma.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts* ……….Sh. 1,145,624,083/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning* …..…..…..Sh. 517,433,172/=
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit* ……….........Sh. 295,814,028/=
Kif. 1005 – *Government Comm.Unit*.............Sh.178,411,206/=
Kif. 1006 – *Procurement Manag. Unit* ....... Sh. 299,483,102/=
Kif. 1007 – *Legal Services Unit* …..….......…Sh. 194,541,135/=
Kif. 1008 – *Mgt. Information Syst. Unit*..........Sh. 242,932,170/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 – *Civil Affairs & Contingencies...*Sh. 2,534,157,678/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Naomba kupata ufafanuzi wa *Sub Vote* 27210 ya *Social Assistance Benefit in Cash*. Baada ya kupitia randama nimegundua kwamba fedha hizi ni za maafa, lakini zimepungua kutoka shilingi 3,600,000,000 za mwaka 2017 mpaka shilingi 2,000,000,000 mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba kumekuwa na matatizo mengi sana ya maafa katika nchi yetu. Japo Serikali yetu imeondoa suala la wananchi ambao wanapata njaa kwamba wajitegemee, watajua wenyewe, walime, wasilime, hawahangaiki na mahindi ya njaa tena, lakini pia kumekuwa na maafa yanayotokana na *natural calamities.* Kumekuwa na mafuriko, maeneo mengi tumeona, Kagera, Korogwe mwaka jana tu kwa Mheshimiwa Chatanda, tumeona Ukonga na maeneo mengi, Kilosa tumeona mwaka 2017, lakini pia hata kwangu Babati maafa yalitokea, wafanyabiashara *stand* mali zao zikaharibiwa na mvua za mafuriko, lakini Serikali imekuwa haipeleki hizi fedha na kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliona miaka iliyopita, Kagera wananchi walilia na Mheshimiwa Mbunge mmoja wa uongozi wa juu alilia. Majibu aliyopata ni kwamba kama unaona wananchi wako wanastahili kupewa mabati...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pauline, hoja yako ni kwamba kwa nini hela zimepungua, si ndiyo?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Nilikuwa naboresha tu hoja yangu, lakini nisipopata majibu kwa nini Bunge lisiongeze fedha hizi kutoka shilingi bilioni mbili zikaongezeka na nchi hii ni kubwa na maafa haya yamekuwa yakitokea wananchi hawategemei, nakusudia kutoa shilingi ili Waheshimiwa Wabunge tujadili, tusibaki kulalamika wakati sisi tunapitisha bajeti, wananchi wetu wanapata matatizo, Serikali inatenga shilingi bilioni mbili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipate majibu ya kina.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikianza kutoa majibu kwenye masuala ya kisera nilisema kwamba baada ya kuundwa kwa sheria ya mwaka 2015, mfumo wa uratibu wa maafa umebadilika,

sasa unazingatia sheria. Kuzingatia kwetu sheria ni kwamba tunaanza kuziimarisha Kamati za Maafa toka kwenye ngazi za Wilaya, Mkoa na mpaka kuja katika ngazi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukishaanza kutoa uimarishaji wa Kamati za Maafa kwenye ngazi nyingine na ukagatua pia hayo madaraka ya kusimamia maafa kwenye ngazi nyingine ina maana pia hata ule mzigo mkubwa uliokuwa kwenye ngazi ya Taifa pia na wenyewe lazima upungue, hiyo ni sababu ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili, Mheshimiwa Mbunge hapa amesema kitu cha muhimu sana. Huko nyuma kweli tulikuwa na ukame, lakini tulikuwa na utaratibu wa kugawa vyakula katika maeneo ambayo labda yamekumbwa na ukame, lakini kwa sasa hivi kwa kuzingatia hali ya hewa pia tuliyokuwa nayo; na jinsi mwenendo mzima wa taarifa za upatikanaji wa chakula katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu ya Tanzania, ilionekana kabisa kwa bajeti ya Taifa tuliyonayo itakuwa kutenga fedha, tena nyingi kama zilizotumika mwaka 2017, pia hayo siyo matumizi mazuri ya *resources*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba wanapopata majanga yoyote ama maafa katika maeneo yao, zipo hizo ngazi ambazo nimeshazisema. Siyo kwamba kila linalotokea ni kwamba fedha ya maafa ambayo iko Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo itaenda kufanya kazi kule, hapana. Tunakwenda kwa ngazi na kwa utaratibu ambao umebainishwa bayana kwenye sheria ya mwaka 2015 na niendelee kuwaomba Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya waielewe sheria hiyo ili tuweze kusaidiana kusimamia zoezi hili la maafa linapotokea katika eneo lolote lile katika nchi yetu ya Tanzania.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama.

**MWENYEKITI:** Katibu tuendelee.

Kif. 2002 – *National Festival*.....................Sh.376,054,949/=
Kif. 3001 – *Parliamentary and Political Affairs*...................................Sh. 476,979,152/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4001 – *Private Sector Development and Economic Empowerment*..........Sh. 3,518,856,225/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pauline Gekul, imekuona. Fungu lipi?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, 4001 sirudi nyuma japo umenipiga juu kwa juu kwenye hicho kifungu kilichopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee. Naomba nipate ufafanuzi pia wa *Sub Vote* 26311. Fedha hizi kwa mujibu wa randama ni kwa ajili ya Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda mchache uliopita Mheshimiwa Halima Bulembo amezungumzia hili pia kuhusu fedha ambazo zinatengwa kwa ngazi hii ya juu ya Serikali Kuu kwa ajili ya kuwapatia wananchi wajiendeleze kiuchumi. Fedha hizi ni chache sana, ni kwa nini Serikali haioni kwamba kuna sababu ya kuongeza fedha hizi wakati wa Bajeti Kuu ya Serikali wakati Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakapo-*table* bajeti yake? Kwa sababu sasa hivi tunachofanya ni kuangalia maeneo gani ambayo Bunge tunaweza tukaishauri Serikali na wakaongezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi naomba Mheshimiwa Waziri anipatie ufafanuzi, anafikiri hizi shilingi bilioni 2.9

zitawawezesha wananchi gani kiuchumi ilhali akijua Halmashauri zetu hawana vyanzo vya mapato na asilimia 10 ya vijana na wanawake sasa zimekuwa hazitengwi kwa sababu vyanzo vingi vimechukuliwa na Serikali Kuu. Kwa nini asione busara kwamba hizi fedha Bunge tuiweke *pending* tuongeze wakati wa Bajeti Kuu ya Serikali kwa sababu fedha hizi hazitoshi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Unajua maswali ya bajeti imepungua kidogo hapa, fedha hizi hazitoshi, ni magumu kidogo kwa sababu hii ni bajeti. Bajeti ni kupanga na kuchagua, ndicho kilichopo. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Kwanza naomba niseme tu kwamba hii ni ruzuku kwa taasisi ambazo ziko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini hoja ya Mheshimiwa Mbunge anataka kuonesha kwamba tunapoendelea kutenga bajeti kidogo labda kwenye fedha za uwezeshaji wananchi kiuchumi kwenye idara hii ya maendeleo ya sekta binafsi hazitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu kwenye eneo la uwezeshaji wananchi kiuchumi inaratibu pia ile mifuko mingine 17 ambayo nayo pia inatoa mikopo kwa Watanzania kwa mifumo tofauti ikiwemo huo mfuko aliousema wa asilimia 10 kwenye Halmashauri ya Wilaya, ikiwemo mfuko huu ambao uko ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ukiwemo ule mfuko wa *Youth Development Fund* ambao upo pia ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu, pia Mfuko wa Rais wa Kukopesha; tunayo mifuko takribani kama 17, ingawa sasa hivi ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu kama mmefuatilia katika kitabu chetu cha hotuba ya bajeti tunafikiria namna nzuri sasa ya kuunganisha baadhi ya mifuko ili kuwa na nguvu ya kutosha ya kuweze kuhudumia Watanzania wengi kwa kuwapa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi, hela iliyotengwa hapa itaenda kwenye ruzuku za taasisi. Kama ni suala la fedha ya ukopeshaji, bado tuna mifuko mingine takriban kama 17 na yenyewe inafanya kazi hiyo hiyo moja na inaratibiwa na idara hii mahali hapa pia ambapo tumetenga hiyo fedha.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 5001- *Coord. of Govern'nt B'ness*...........Sh. 665,760,631/=
Kif. 7001- *Government Printers*...............Sh. 2,474,420,000/=

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 25 – Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu**

Kif.1001- *Administration and Human Resource Management*..............................Sh. 7,016,012,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba maelezo kwa kifungu kidogo *22016 - travel in country*. Nataka maelezo ni sababu zipi zinazofanya ofisi binafsi ya Waziri Mkuu kuwa na nyongeza ya takribani shilingi milioni 466 ukilinganisha na fedha za mwaka 2017 wakati pia kwenye hili fungu tulilomaliza la Ofisi ya Waziri Mkuu nako kuna *travel in country*?

Nataka tu maelezo, ni kwa sababu gani kuna nyongeza ya *almost half* ukilinganisha na mwaka 2017?

**MWENYEKITI:** Si Mheshimiwa Waziri Mkuu kasema hapa anatembelea nchi nzima, majimbo yote. Mnategemea bajeti isiongezeke! *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mwaka 2017 alikuwa Waziri Mkuu na alisafiri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dada Susan kama alivyosema, nirudie haya ya kwako, lakini nitaongeza pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadri Serikali yetu inavyozidi kufanya kazi, miradi ya maendeleo inavyozidi kuongezeka, uhitaji wa wananchi kukutana na Serikali unavyozidi kuongezeka, ndivyo shughuli za Ofisi ya Waziri Mkuu zinavyozidi kuongezeka na hivyo matumizi ya fedha yamezidi kuongezeka ili kuifanya Serikali ifanye kazi yake sawa sawa na hasa kwenye hii *private vote* ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tumetengeneza mfumo mpya wa uratibu wa shughuli za Ofisi ya Waziri Mkuu na hivyo kumekuwa na ongezeko kidogo la wafanyakazi katika *vote* hii 25 ambayo ni *private office* ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ongezeko hili ni halali kabisa linaendana na mahitaji na linaendana na kazi ambazo tumeweza kuziratibu ili ziweze kufanyiwa kazi kwa mwaka huu wa fedha ambao tunaupitishia bajeti yake.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 15 – Tume ya Usuluhishi na Uamuzi**

Kif. 2001 – *Mediation* ...........................Sh. 790,449,860/=
Kif. 2002 – *Arbitration* ...........................Sh. 867,409,860/=
Kif. 1001 – *Administration and Human Resources Management*............................Sh. 1,535,394,280/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit*........Sh. 110,580,000/=
Kif. 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*.........................Sh. 140,280,000/=
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit*.......................Sh. 144,200,000/=

Kif. 1005 – *Information, Communication and Technology Unit*..................Sh. 140,750,000/=
Kif. 1006 – *Procurement Management Unit*...Sh. 98,960,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi**

Kif. 1001 – *Administration and Human Resources Management*...........................Sh. 2,297,435,364/=
Kif. 1002 – *Planning Monitoring and Evaluation Division*..................................Sh. 277,689,000/=
Kif. 1003 – *Finance and Accounts Unit*........Sh. 340,750,000/=
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit*...................Sh. 287,654,000/=
Kif. 1005 – *Legal Services Unit* ...................Sh. 247,806,000/=
Kif. 1006 – *Procurement Management and Logistic Unit* .........................Sh. 294,148,636/=
Kif. 2001 – *Election Management Division* ..Sh. 297,194,000/=
Kif. 2002 – *Permanent National Voters Registration System Division*.....Sh. 460,551,000/=
Kif. 2003 – *Voters Education and Public Information Division* ..............Sh. 337,403,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 27 – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa**

Kif. 1001 – *Administration and Human Resources Management*...........Sh. 680,113,004/=
Kif. 1002 – *Finance and Account Unit* ........Sh. 189,657,000/=
Kif. 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation*.................................Sh. 61,138,000/=
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit*....................Sh. 105,651,362/=
Kif. 1005 – *Procurement Manag'nt Unit*.......Sh. 120,316,000/=

Kif. 1006 – *Information and Communication Technology*................................Sh. 83,227,000/=
Kif. 1007 – *Government Comm. Unit*..............Sh. 85,445,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1008 – *Registration of Political Parties Unit*....................................Sh. 160,327,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo cha 22008, nimeona zimetengwa shilingi 2,000/= hapa - *Training - Domestic* sasa nataka nijue, ni mafunzo gani ya shilingi 2,000/= kwa vyama vya siasa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lugha nyepesi tunasema ni *token.* Ni fungu ambalo tunaliweka tayari kama pale tutapata fedha kwa ajili ya kazi hii, basi fungu hilo Hazina wanakuwa wanalitambua lipo. Kwa hiyo, watakapoingiza fedha zinaingia moja kwa moja kwenye kifungu husika. Kwa hiyo, huo ndiyo mfumo wa bajeti ambao tunao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pauline.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hiki ni Kitengo cha Usajili wa Vyama vya Siasa. Naomba tu nipate ufafanuzi wa jumla kwamba kitengo hiki kinahusika kusajili vyama, lakini Serikali hii iliyoko madarakani haitaki vyama hivi vifanye kazi.

Naomba nifahamu ni lini mtaruhusu mikutano ya vyama vya siasa? Wakati sisi tunapitisha bajeti hii ili ifanye kazi kwa kitengo hiki wasajili vyama, halafu ninyi mnazuia vyama visifanye kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pauline, ni fungu gani pale limepungua, limeongezeka au limefanyaje? Ni fedha zipi unazozihoji hapa?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1009 – *Election Expenses and Civic Education*.......................................Sh. 134,316,634/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1010 – *Monitoring of Political Parties Unit*................................Sh. 17,637,850,000/=

**MWENYEKITI:** Kule tulishavuka, labda kama upo kwenye fungu alilolitaja Katibu sasa, 1010.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana ni 1009.

**MWENYEKITI:** Tumeshavuka bahati mbaya.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uliniona kabisa wakati nimesimama.

*(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 1011 – *Office of Deputy Registrar – Zanzibar* ........................................ Sh. 151,900,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, peke yake.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kifungu 1011 Ofisi ya Msajili Msaidizi Zanzibar, fungu dogo 22014 – *hospitality supplies and services* zimetengwa shilingi sifuri. Kwa hiyo, naomba maelezo kidogo.

**MWENYEKITI:** *Hospitality.* Mheshimiwa Waitara unataka tuongeze hela ya chai na vitumbua na nini.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Muhimu sana hiyo.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu hili, fedha ambayo haikutengwa hapa, tumekubaliana kwamba itatumika kwenye fungu la *administration* kwa kuwa ita-*serve* katika mafungu mengine yoyote.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 65 – Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu**

Kif. 1001 – *Admin. & HR Manag'nt* ......... Sh. 3,754,616,594/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts* ............. Sh. 241,908,000/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning* ................ Sh. 334,876,000/=
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit* ................... Sh. 140,912,000/=
Kif. 1005 – *Procurement Mgt. Unit*................ Sh. 71,654,000/=
Kif. 1006 – *Gover'nt Comm. Unit*................ Sh. 100,164,000/=
Kif. 1007 – *Inform. & Comm. Tech. Unit*........ Sh. 40,000,000/=
Kif. 1008 – *Legal Service Unit* ..................... Sh. 15,000,000/=
Kif. 2001 – *Labour &Workers Particip*.......... Sh. 6,148,053,153/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 – *Employment Division* ............ Sh. 1,653,047,951/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, nimekuona leo.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufafanuzi kwenye kifungu cha 22012 ambacho kinazungumzia *communications and information* kwenye *employment division*. Hili ni eneo la ajira, lakini

pametengewa sifuri kabisa, maana yake Watanzania wasipate habari yoyote inayohusiana na ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi wa jambo hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu hili linahudumiwa pamoja katika fungu la utawala tukiamini kabisa kwamba kupitia fungu hilo, basi tutaweza kuhudumia pia fungu hili. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge aamini tu kwamba fedha za fungu hilo zipo katika fungu la utawala.

*(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2003 – *Registrar of Trade Unions* ........... Sh. 97,516,000/=
Kif. 2004 – *Arusha Regional Labour Office* ..... Sh. 7,455,000/=
Kif. 2005 – *Dodoma Regional Office* ............ Sh. 7,955,000/=
Kif. 2006 – *Geita Regional Labour Office* ....... Sh. 7,455,000/=
Kif. 2007 – *Iringa Regional Labour Office* ...... Sh. 7,455,000/=
Kif. 2008 – *Kagera Regional Labour Office*..... Sh. 7,455,000/=
Kif. 2009 – *Kigoma Regional Labour Office* ...... Sh.7,455,000/=
Kif. 2010 – *Kilimanjaro Regional Labour Office* ........................................ Sh. 7,455,000/=
Kif. 2011 – *Lindi Regional Labour Office* ........ Sh. 7,455,000/=
Kif. 2013 – *Mara Regional Labour Office* ....... Sh. 7,455,000/=
Kif. 2014 – *Mbeya Regional Labour Office* ..... Sh. 7,455,000/=
Kif. 2015 – *Morogoro Regional Labour Office*.. Sh. 7,455,000/=
Kif. 2016 – *Mtwara Regional Labour Office* .... Sh. 7,455,000/=
Kif. 2017 – *Mwanza Regional Labour Office*.. Sh. 7,455,000/=
Kif. 2018 – *Njombe Regional Labour Office* ... Sh. 7,455,000/=
Kif. 2019 – *Pwani Regional Labour Office* ...... Sh. 7,455,000/=
Kif. 2020 – *Rukwa Regional Labour Office* ......Sh. 7,455,000/=
Kif. 2022 – *Ruvuma Regional Labour Office* ... Sh. 7,095,000/=
Kif. 2023 – *Shinyanga Regional Labour Office*....Sh. 7,215,000/=

Kif. 2025 – *Singida Regional Labour Office* .... Sh. 7,455,000/=
Kif. 2026 – *Tabora Regional Labour Office* ..... Sh. 7,455,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2027 – *Tanga Regional Labour Office* ...... Sh. 7,455,000/=

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani.

**MWENYEKITI:** Mmh!

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, kwenye hivi vifungu vya mikoa vyote, upande wa *travel in country* inaonesha kiwango kinataka kufanana, ni shilingi milioni 5.7.2.2 yaani zimekaa kiaina hiyo. Sasa nataka kuelewa, kusafiri nchini kwa mfano mtu aliyepo Kigoma na huyu aliyeko Dodoma, yaani gharama zinabaki zinafafana? Naomba ufafanuzi tu. Zinafanana kweli kwa sura hiyo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Lakini Mheshimiwa si unaona hata jumla yenyewe ni shilingi milioni saba? Sasa hata ukilalamikia, sijui kama ina uzito wowote. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mavunde.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika mafungu haya yote, hizi ni Ofisi za kazi za mikoa ambazo pia zinahudumiwa na fungu la utawala. Kwa hiyo, linapojitokeza hitaji lingine lolote fungu la utawala huwa lina-*take care* katika eneo hilo. Kwa hiyo, ndiyo maana tumetoa hiyo *flat rate*.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2028 – *Temeke Regional Labour Office* ..... Sh. 7,955,000/=
Kif. 2029 – *Kinondoni Regional Labour Office* ........................................ Sh. 7,955,000/=
Kif. 2030 – *Ilala Regional Labour Office* ......... Sh. 7,955,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2031 – *Social Security Division* ............. Sh. 516,000,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Naomba tu ufafanuzi kwenye *sub vote 22010,* hii fedha hapa ime-*shoot* kutoka milioni 11 mwaka juzi, 2016; shilingi 25,800,000/= mwaka 2018 na leo ni shilingi 102,300,000/=. Tunaomba kujua nini kinachofanyika kwenye kifungu hiki. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni eneo la *Social Security Division.* Unajua kwamba sasa hivi tumefanya kazi kubwa ya kutunga sheria mpya ya kuunganisha mifuko ya hifadhi ya jamii. Kwa hiyo, tuna kazi ya kuimarisha *structure* mpya ya mfuko mpya ambao ni wa watumishi wa umma tuliouunda na watumishi kwenye idara hii watatakiwa kufanya kazi ya ziada ili kuhakikisha kwamba hiyo *structure* mpya ya mfuko mpya inafanya kazi vizuri na ndio maana sasa unaona matumizi hayo yameongezeka. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2032 – *Youth Development* ................ Sh. 350,000,000/=

**MWENYEKITI:** *Okay*. Tuanze na Mheshimiwa Dkt. Semesi, halafu utafutia Mheshimiwa.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Nipo kwenye *items* 21111 na 21113, *sub vote* hii ni muhimu sana kwa ajili ya vijana wetu, lakini naona hawajatengewa *basic salaries instead* wana *personal allowances.* Sasa naomba ufafanuzi kwenye hili. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, mishahara mipya.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA(MHE. ANTONY P. MAVUNDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama itakumbukwa vema, kitengo hiki cha vijana awali kilikuwa katika Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo na sasa baada ya kuhamishiwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu, hivi sasa mishahara yake inapatikana katika fungu la utawala, ndilo hasa lina mishahara katika eneo hilo la Kitengo cha Vijana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rhoda Kunchela, ni Mheshimiwa Devotha Minja, samahani.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nipo kwenye *sub vote* 22013 ambayo inasema *education materials, services and supplies* na hapa tunazungumzia vijana na maendeleo ambapo tunategemea kwamba Serikali ingetenga fedha kwa ajili ya kuelimisha vijana hasa masuala mbalimbali. Ukiangalia miaka ya nyuma huko, zimewahi kutengwa hata shilingi milioni 45, lakini kwa mwaka huu hakuna fedha zozote ambazo zimetengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi wa hilo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfumo wa bajeti tuliouandaa na hasa kwa kazi ambayo tunataka kuifanya kwenye eneo hili la *Youth*

*Development* na ukiangalia kuna malengo pia ya kuanzisha Baraza la Vijana, kwa hiyo, fedha hizo nyingi tumezitenga kwenye fungu la utawala ili kazi hii iweze kufanyika vizuri na isimamiwe vizuri.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Sasa kabla hatujaendelea, kwa mamlaka niliyopewa na kanuni ya 104(1) ninaongeza dakika 30 ili tumalizie kazi iliyo mbele yetu. Katibu.

**Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti UKIMWI**

Kif. 1001 – *Policy, Planning & Research*........Sh. 199,539,194/=
Kif. 1002 – *Finance, Admn. and Resource Mobilization*..............................Sh. 1,067,033,581/=
Kif. 1003 – *Monitoring and Evaluation* ...... Sh. 157,352,752/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 – *Advocacy and Information* ...... Sh. 138,322,917/=

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Semesi.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Nipo kwenye *items* 22012 na 22013. Katika kitengo hiki, mawasiliano na kutoa elimu ni muhimu sana ili kudhibiti janga hili la ugonjwa huu. Sasa naomba ufafanuzi kwa nini hela iliyotolewa pale ni shilingi 400,800,000/= na inasoma sifuri kwenye maeneo hayo ambayo ni muhimu sana kutoa elimu? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Tume hii ya Kudhibiti UKIMWI, tutakapofika kwenye *development budget,* utaona kwamba mafungu

haya pia yanakuwa *supported* na fedha za wafadhili ambazo zinalenga kufanya kazi ambayo inafanana. Kwa hiyo, ndiyo maana tunatenga hivyo, lakini tukifika kwenye *development* utaona yapo mafungu kazi zake zimekasimiwa pia kwenye vifungu hivi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1005 – *National Response* ……………..…. Sh. 494,328,000/=
Kif. 1006 – *Procurement Management Unit* ……………………………………. Sh. 108,772,000/=
Kif. 1007 – *Legal Services Unit* ……………….. Sh. 115,065,000/=
Kif. 1008 – *Manag'nt Information Systems*…..Sh. 70,879,000/=
Kif. 1009 – *Internal Audit Unit*……………….Sh. 140,912,636/=
Kif. 1010 – *Special Programs Unit* ………..…. Sh. 64,884,000/=
Kif. 1011 – *Government Comm. Unit*……..…. Sh. 52,341,920/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 91 – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**

Kif. 1001 – *Admin. &HR Mgt.*…………………Sh. 5,755,101,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 42 – Mfuko wa Bunge**

**MWENYEKITI:** Hapa atakayesimama anatolewa nje. Anayesimama hapa inabidi a-*declare interest,* anataka posho hataki? Katibu tuendelee. *(Kicheko)*

Kif. 1001 – *Admin. &HR Mgt.* ……….Sh. 9,338,530,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pauline, nini tena? Haya bwana. *(Kicheko)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, posho nazihitaji, siyo kwamba sizihitaji, lakini *with due respect* naomba tu nihoji maana kuuliza siyo ujinga, ni kutaka tu kufahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukijadili sana kuhusu Mfuko wetu wa Bunge, wenzetu wa Mahakama wana mfuko wao, na sisi pia tumekuwa tukijadili.

Sasa kwa uelewa wangu ni kwamba hivi vinatoka kwa Serikali Kuu. Hatuna mfuko *per se* ambao unaweza uka-*solve* mambo yetu madogo madogo; mfano, kama juzi tu tulikuwa tunajadili masuala ya *security* kwa Wabunge, Serikali ikachukua ile hoja kwamba wanakwenda kuangalia *implications* zake katika masuala ya *cost.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Bunge hili tulishawahi kuahidiwa tutapewa *laptops,* lakini pia watumishi wetu, wasaidizi wetu, ma-*secretary* na madereva wetu mishahara yao haijawahi kuwa *reviewed* muda mrefu, wamekuwa wakilipwa kiasi ambacho ni kidogo. Kuna masuala ya *gratuity* zetu kukatwa kodi, jambo ambalo kwa muda mrefu inaonekana kama sisi wenyewe kama hatuhangaiki nayo sana.

Naomba tu nifahamu, mfuko wetu huu unaundwa lini na hizi fedha zinawekwa lini ili ku-*solve* mambo madogo madogo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Unaulizwa tu Mheshimiwa Pauline, fungu gani? Wanatafuta hawaoni hapa, wasaidie tu ili waweze kuona vizuri.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo la *administration* la shilingi bilioni tisa. Ni suala la kiufafanuzi. *(Kicheko)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Library & Research Depart*...........Sh. 349,096,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 – *Information &Comm. Techn.* ..... Sh. 608,188,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu kidogo cha 22012 - *communication and information.* Naona mwaka 2017 walitenga shilingi milioni 194 na mwaka huu shilingi milioni 242. Tumekuwa tukielezwa kwamba tutapewa zile *iPads* ili tutoke kwenye *old technologies* za kuweka makaratasi mengi hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia hizi hela zilizotengwa hapa, shilingi milioni 242, ni dhahiri haziwezi kununua hizo *iPads* au *laptops* wakatuwekea hapa. Nataka nijue hizi shilingi milioni 242 zimepangwa katika *communication* ipi? Ni lini sasa tutapata hizo *laptops* ili tuendane na *modern technology?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hili suala sijui tuangalie Kanuni zetu, kwa sababu kwa mujibu wa Sheria yetu ya Bajeti, masuala yote ya Mfuko yanaishia kwenye Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama kuna mtu alikuwa na *interest* yoyote ya masuala ya Bunge, alitakiwa kuja kwenye Kamati ya Bajeti. Kule tukitoka tunakuwa tumemaliza, kwa sababu hapo anayeulizwa aidha anayetakiwa ajibu ni ama Katibu wa Bunge au Spika ambaye amekalia Kiti hapo, kitu ambacho yaani kimantiki haiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndiyo maana nikasema tuangalie aidha Kanuni zetu au turudi. Kwa sababu

Mfuko wa *CAG,* Mfuko wa Bunge na Mfuko wa Mahakama tunamalizana kwenye Kamati ya Bajeti. Sasa tukija hapa tena tunafukua kama vile tunajadili bajeti nyingine za kisekta, nadhani hatutendi haki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nakubaliana kabisa na anachokisema Mheshimiwa Hawa Ghasia, ndiyo utaratibu. Ni kwenye Mabunge yote. Yaani bajeti ya Bunge haiwi *queried* tena, inatakiwa iishie kwenye *Budget Committee,* kwenye Tume ya Bunge kule. Ikishafika Bungeni, inapigwa mara moja tu. Tena wala huwa haiendi kwa mafungu hivi; huu ni utaratibu tu wa hapa, lakini yenyewe huwa inapigwa mara moja. Kwenye Mabunge yote *actually* ndiyo huwa inaanza. Hii ya Bunge ndiyo ya kwanza kabisa inapitishwa hiyo kwanza, halafu ndiyo zinafuata nyingine zote. *(Kicheko/ Makofi)*

Kwa sababu kama Wabunge hatujapata hela, sasa utaidhinishaje za watu wengine kwanza halafu inakuwa haijakaa sawa sawa. Kwa hiyo, nilitarajia tu hapa kidogo tutafanya ile tutekeleze wajibu kwamba apitishe mafungu haya lakini tuna *forum* nyingine za kufanyia kazi. Kwa hiyo, tuendelee kwa utaratibu huu ambao tumeshauriwa na Mwenyekiti wa Bajeti. Katibu taja fungu halafu, twendeni hivyo.

Kif. 2001 – *Budget Office* ..................... Sh. 1,184,920,000/=
Kif. 2002 – *Table Office* ...................... Sh. 83,760,514,000/=
Kif. 2003 – *Parliamentary Committees* .....Sh. 10,748,746,000/=
Kif. 2004 – *Hansard*............................ Sh. 1,063,180,000/=
Kif. 2005 – *Legal Services* ..................... Sh. 1,037,119,000/=
Kif. 3001 – *Private Office of the Speaker* ..... Sh. 759,704,000/=
Kif. 3002 – *Private Office of the Deputy Speaker* .................................. Sh. 408,960,000/=
Kif. 3003 – *Office of the Leader of Opposition* ..................................Sh. 426,888,000/=
Kif. 3004 – *Private Office of the Clerk* ......... Sh. 834,962,000/=
Kif. 3005 – *Finance and Account* ............. Sh. 458,023,000/=
Kif. 3006 – *International Relations and Protocol* ................................ Sh. 2,789,980,500/=

Kif. 3007 – *Inform. Education & Comm.* ........................ Sh. 0
Kif. 3008 – *Internal Audit* .........................Sh. 243,316,000/=
Kif. 3009 – *Procurement Management* ...... Sh. 406,594,000/=
Kif. 3010 – *Security and Defense* .............. Sh. 238,976,000/=
Kif. 3011 – *Estate Management* .............Sh. 1,640,126,500/=
Kif. 3012 – *Zanzibar Directorate* ...............Sh. 207,664,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Hapo barabara, kuulizauliza hapa ni *conflict of interest.* Huwezi kuulizia habari ya posho yako mwenyewe. *(Kicheko)*

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani.

**MWENYEKITI:** Tuendelee Katibu.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kinachofuata ni wapi?

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu utaratibu. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Kitabu Namba Nne. Matumizi ya Maendeleo.

**MATUMIZI YA MAENDELEO**

**Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu**

Kif. 1001 – *Admin. & HR Manag'nt*.......... Sh. 9,000,000,000/=
Kif. 2001 – *Civil Affairs and Contingencies* ....Sh. 463,453,469/=
Kif. 4001 – *Private Sector Dev. & Economic Empowerment*............................. Sh. 0
Kif. 5001 – *Coordination of Government Bussiness*.............................. Sh. 26,927,987,531/=

Kif. 7001 – *Government Printer*...............................Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 42 – Mfuko wa Bunge**

Kif. 1003 – *Information and Comm. Techn.*. Sh. 500,000,000/=
Kif. 2001 – *Budget Office* ......................... Sh. 3,315,613,000/=
Kif. 2004 – *Hansard*........................................... Sh. 0
Kif. 3004 – *Private Office of the Clerk* ........Sh. 2,000,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3011 – *Estate Management* .............Sh. 2,500,000,000/=

**MWENYEKITI:** Kuna Mbunge amesimama? Ndiyo, samahani. Mheshimiwa Molle.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika *sub vote 3011* mwaka 2017 walisema kwamba watatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hasa ngazi katika jengo la utawala. Sasa nilitaka tu kupata ufafanuzi kwamba katika hizi fedha zilizotengwa mwaka huu hizo shilingi 8,000,000,000/=, je, ujenzi wa ngazi katika Jengo la Utawala zitakuwepo kwa mwaka huu?

**MBUNGE FULANI:** Ngazi au *lift*?

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumradhi, ni *lift*. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Nilikuwa nasubiria tu umalize, maana yake ni kwamba tuongeze ngazi? Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kuweka *lift* kwenye

majengo ya Bunge uko katika fedha zile ambazo zimetengwa kwa mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, kwa mwaka ujao, kwa sababu fedha ambazo zinatolewa na Bunge tulipokuwa mbele ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, Serikali kupitia Wizara ya Fedha iliweka *commitment* ya kutoa fedha ya *development* kwa ajili ya kumalizia pamoja na mradi huo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hii inaruhusiwa. Lazima tujue kwamba Waheshimiwa Wabunge sio wote ambao tunaweza kufika kule ghorofa ya nne. Kwa hiyo, ni hoja muhimu sana kwa kweli, wala siyo kwa sababu ya Waheshimiwa labda ambao kuna ugumu wa aina moja au nyingine wa maumbile, lakini nina uhakika *lift* zinahitajika pale. Nayo ni ngazi pia hiyo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Katibu, tuendelee.

**Fungu 61 – Tume ya Uchaguzi**

Kif. 1001 – *Administration and HR Management* .......... Sh. 0
Kif. 1002 – *Planning, Monitoring and Evaluation Division* ................................................Sh. 0
Kif. 1003 – *Finance and Accounts Unit* ......................Sh. 0
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit* ................................Sh. 0
Kif. 1005 – *Legal Services Unit* ...............................Sh. 0
Kif. 1006 – *Procurement Management and Logistics Unit* ...............................................Sh. 0
Kif. 2002 – *Permanent National Voters Registration System Div*................................ Sh. 5,000,000,000/=
Kif. 2003 – *Voters Education and Public Information Division*................................ Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 65 – Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu**

Kif. 1003 – *Policy and Planning* ................ Sh. 1,400,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 – *Employment Division* ............ Sh. 15,000,000,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Sub vote 2002,* kasma ndogo ya 6581 - *Support National Skills Development Programme.* Nilitaka nijue hizi shilingi bilioni 15 zinaenda kutumika katika mgawanyo upi? Kwa maana ya kwamba kwenye majimbo, kiwilaya mmetenga idadi ya watu hawa ambao wanatakiwa kupata hizi *skills;* mmetenga kiwilaya, kimajimbo, kimkoa au ndiyo ile inatokea kwamba una-*concentrate* kwenye mkoa fulani halafu mkoa mwingine au Wilaya nyingine unakuta haipati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata ufafanuzi kwenye hizi shilingi bilioni 15, zitatumika vipi?

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ni mahususi kwa ajili ya Programu ya Kitaifa ya Kukuza Ujuzi, ambayo lengo lake kubwa ni kuhakikisha ya kwamba tunaifanya nguvu kazi ya Taifa letu wawe wana ujuzi wa kutosha, lakini ujuzi ambao vilevile utampa sifa ya kuwa anaweza kuajirika kwa maana ya *employability.*

Aidha, fedha hii haiendi mikoani, lakini inabaki katika uratibu wa Kitaifa na katika programu nyingi ambazo tumezifanya katika eneo hili, ni pamoja na kuwapeleka vijana wetu katika mafunzo mbalimbali ya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile programu hii pia imeandaa baadhi ya miongozo ya kuwawezesha vijana wa vyuo vikuu ambao watahitimu katika vyuo vikuu ambao wanapata taabu sana ya kupata maeneo ya kwenda kufanyia kazi, basi kupitia programu hii pia watapata nafasi ya kwenda kushikizwa sehemu kwa ajili ya kufanya mafunzo kwa vitendo.

Kwa hiyo, ni programu ambayo inaratibiwa kitaifa na lengo lake ni kwa ajili ya kukuza ujuzi wa nguvukazi ya Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2032 – *Youth Development* ............ Sh. 1,000,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 91 – Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya**

Kif. 1001 – *Administration and HR Mgt*....................... Sh. 0

**Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti UKIMWI**

Kif. 1001 – *Policy, Planning &Research*..... Sh. 1,461,174,000/=
Kif. 1002 – *Finance, Administartion and Resource Mobilization* ................................Sh. 3,526,018,000/=
Kif. 1003 – *Monitoring and Evaluation*...... Sh. 1,787,994,337/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 – *Advocacy & Information* .......... Sh. 477,534,277/=

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo tu. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Haya, tuanze Sheikh.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo katika *item* 5494. Lengo langu kubwa ni kwenye *Mainstreaming HIV/AIDS in National Development* ambapo ukiangalia kwenye *local* hakuna kitu, lakini kwenye *forex* kuna shilingi 457,414,277/= inasema ni *National Development* lakini ukiangalia hili suala lote tumewaachia wafadhili zaidi kulikoni sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yetu ilikuwa tunasema tunaandaa mazingira kuona kwamba kwa vyovyote itakavyoonekana, basi kama Taifa nasi tunaandaa uwezo wa ziada. Ni kwa nini basi Mheshimiwa Waziri asituambie mikakati ya ziada kuona hili suala linafanyiwa kazi na wakati alikwishatuahidi kwamba mipango hii ipo katika mchakato wake na huenda tukafanikiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na namwelewa sana Mheshimiwa Masoud. Kwa kweli amekuwa akitukumbusha kila siku suala hili la kutenga *resources* za ndani katika mapambano dhidi ya tatizo la UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuwaambia Waheshimiwa Wabunge ni jambo moja kwamba mapambano dhidi ya tatizo hili la Ugonjwa wa UKIMWI katika nchi yetu ya Tanzania yanaratibiwa kitaifa, lakini yanaratibiwa pia na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye uratibu wa Kimataifa na hasa kwa kupitia *Global Fund,* kunakuwa na fedha ambazo zinatengwa rasmi kusaidia mipango na mikakati ya Kitaifa kwa nchi zote ambazo zimekubaliana kwenye mikataba hiyo ambayo ni ya mapambano dhidi ya UKIMWI. Kwa hiyo, sisi tukishapata fedha hizo ambazo ni

*commitment* ya fedha zinazotoka na siyo *commitment* ya fedha za ufadhili ambazo hazitoki, sijui kama ni matumizi bora ya fedha na ninyi tena mnatenga tena fedha nyingine ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kuanzia sasa hivi kwa sababu bado tuna uratibu huo wa Kimataifa wa mapambano dhidi ya UKIMWI; na kuna *commitment* hiyo ya *donors* kupitia ile mifuko maalum ya kusaidia mapambano dhidi ya tatizo la UKIMWI, kwa hiyo, tumeendelea kutumia fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokisema Mheshimiwa Masoud, tunachokifanya kwa sasa ni kuimarisha nguvu ya ndani kupitia ule Mfuko wa Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(AIDS Trust Fund).* Kwa hiyo, ule sasa ndiyo tunautengea nguvu yetu ya ndani na hata kwenye Kamati tumewaambia mikakati tunayoifanya ili kutenga nguvu yetu ya ndani na hasa kwa kuzingatia matumizi na mwongozo wa fedha ambazo zinakusanywa kwenye ule mfuko ambao umeanzishwa kwa mujibu wa sheria ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa hatuwezi kujitenga na mikakati ya kiulimwengu ya mapambano haya na hatuwezi kukataa pale ambapo mataifa yamekuwa *committed* kutusaidia katika *sectors* ambazo ni *specific.*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1005 – *National Response*……………….Sh.1,839,480,666/=
Kif. 1007- *Legal Services Unit*…………………Sh. 623,050,000/=
Kif. 1008 - *Management Inform. System*.........Sh. 46,100,000/=
Kif. 1009 - *Internal Audit Unit*…………….…...Sh. 99,800,000/=
Kif. 1010 - *Special Programs Unit*…………….Sh. 310,492,480/=
Kif. 1011 – *Government Comm. Unit*............Sh. 128,356,240/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. STEPHEN KIGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**SPIKA**: Bunge linarejea.

Waheshimiwa Wabunge tukae. Mheshimiwa Waziri, Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 104(3)(a) na b) na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake, naomba sasa Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa ni jukumu lenu sasa Waheshimiwa Wabunge kuifanyia uamuzi hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Wote wameafiki. Naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na wengine wote katika Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa na nzuri ambayo mnaifanya. *(Makofi)*

Sisi Wabunge tumetekeleza wajibu wetu wa kuwawezesha kwa kile tulichonacho kidogo, sasa matumaini

yetu ni kwamba mtaenda kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa bidii zaidi, kwa tija zaidi, ili tukikutana mwakani 2019, basi tuwe tunapongezana zaidi kwa kila hali.

Kwa hiyo, tunawatakia kila la kheri kwamba fedha hizi mtazitumia vizuri na vinginevyo tuko pamoja katika utekelezaji wa mambo haya. Na sisi Ofisi ya Bunge, pia mafungu yetu yako kwenu, kwa hiyo, tunawategemeeni pia katika kuhakikisha kwamba mambo yanaenda yanavyotakiwa vizuri.

Sasa Waheshimiwa Wabunge ninalo tangazo moja, leo asubuhi Mheshimiwa Naibu Spika alipokuwa hapa mezani alisoma taarifa yangu kwamba kuna tukio la mlipuko la kifaa cha kielektroniki cha kuchajia simu ya mkononi *(power bank)* ambalo halikusababisha athari yoyote katika ukumbi wa Bunge jana jioni na halikusababisha athari yoyote kwa Waheshimiwa Wabunge.

Napenda kumpongeza *Sergeant-At-Arms* na wasaidizi wake waliokuwepo katika zamu ya jana ambao walifanya kazi kubwa ya kuhakikisha hakukuwa na athari zozote zilizojitokeza. *(Makofi)*

Kipekee nampongeza Polisi *Constable* Rashidi Salum Kapongo kwa ujasiri aliouonesha wakati wa tukio hilo, kwa kuwa yeye alithubutu kuibeba *power bank* iliyokuwa ikiwaka moto na kutoka nayo nje ya ukumbi na kuitumbukiza kwenye maji. Kwa kweli alifanya hivyo kwa kujali kabisa usalama wetu sisi Waheshimiwa Wabunge akaweza ku-*risk* kiasi hicho. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nachukua fursa hii kumpongeza sana askari huyu kwa uharaka ambao umesaidia sana kupunguza athari ambazo zingejitokeza na hii ndiyo aina ya askari ambao kwa kweli tunataka kuwa nao hapa Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa naelekeza Polisi *Constable* Rashidi Salum Kapongo popote pale alipo aingie

hapa ukumbini ndani ya ukumbi wa Bunge ili Waheshimiwa Wabunge mumtambue na muweze kumpongeza. *(Makofi)*

*(Hapa Polisi Constable Rashid Salum Kapongo aliingia Ukumbini)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa makofi hayo, tafsiri yake nafikiri ni kwamba Katibu wa Bunge aangalie namna, eeh... *(Makofi/Vigelegele)*

Pia Mheshimiwa Waziri Mkuu ameona, kwa hiyo, mengine tumwachie Mheshimiwa Waziri Mkuu kama na yeye ataguswa kidogo. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, aidha, tumepokea ushauri kutoka Vyombo vya Ulinzi na Usalama kwamba wakati wa uchunguzi zaidi wa suala hili ukiwa unaendelea, Waheshimiwa Wabunge tuwaombe msiingie wala kutumia *power bank* na chaji za simu ndani ya ukumbi wa Bunge.

Naomba sana msije nazo *power bank* kwenye ukumbi huu tu, simaanishi kwenye eneo la Bunge lote, msiingie nazo *power bank* wala vifaa vya kuchajia simu hivi ndani ya Ukumbi wa Bunge ili kuepuka madhara ya *short* ya umeme na kusababisha moto, kwa kuwa vifaa hivi baadhi yake havina viwango vya maana kiasi ambacho baadhi ya vifaa hivi vinaweza kusababisha milipuko na kuhatarisha maisha ya Waheshimiwa Wabunge pamoja na wageni ambao wanakuwa nasi hapa Bungeni wakati wote. *(Makofi)*

Natarajia kwamba hili mtalizingatia Waheshimiwa Wabunge, la kutokuingia na vifaa hivyo na hasa *power bank.* Tunawaomba sana, maana nyingine zinakusanywa mitaani humo hatuelewi hasa ubora wake. Kama hii ya jana ilikuwa ni *power bank* ambayo ilikuwa inachaji simu mbili kwa mpigo, ikakosa uvumilivu wa kutosha.

Shughuli zetu zimeisha za siku ya leo, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano ambao mmekuwa mkitupatia na mnaoendelea kutupatia. Matumaini yangu ni

kwamba tutaendelea na hali hii hii kwa sababu shughuli za bajeti ya Serikali zinatuchukua kwa muda mrefu. Kwa hiyo, ni matumani yetu kwamba tutafika safari yetu salama.

Waheshimiwa Wabunge, kule Dar es Salaam kuna zoezi linaendelea huko, sasa kidogo Kiti cha Spika kimetikiswa hivi, tunatuhumiwa tuhumiwa mahali kidogo, tumeguswa guswa hivi. Kwa hiyo, natarajia kupata ushauri wenu Waheshimiwa tunafanyaje katika mazingira haya? Maana kuna watoto wetu wako barabarani haiwezekani hata kidogo. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, akina mama wale kwa kweli inabidi tufanye utaratibu tujue nini tutafanya. Pia kuna akina baba wameendelea kujitokeza huko nimesikia na baadhi ya walamikiwa ni akina mama Wabunge, kwa hiyo, hili jambo halina upande jamani.

Basi hawa wamama kama wapo kweli, basi waje kwa Spika au wamwandikie Spika, lakini waniletee na *DNA test,* ile *certificate* ili tuone namna gani ya kuwezesha. Tuna mafungu hapa tumepitisha tunaweza tukawa tunaangalia namna kidogo ya kuweka sawasawa ili Waheshimiwa Wabunge wawe na utulivu katika kufanya kazi za Bunge na siyo kuwa na mawazo wazo mengine mengine.

Waheshimiwa Wabunge, kazi za leo zimekamilika, nawashukuruni sana. Basi kwa hatua hii sasa naomba msimame ili tumalizie kwa kusema naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 2.00 Usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatano, Tarehe 11 Aprili, 2018 Saa Tatu Asubuhi)*